# SUALA LA ARDHI KATIKA RIWAYA TEULE ZA KISWAHILI: TATHMINI YA *KOVU MOYONI* NA *KUFA KUZIKANA*

**MARY KANYUA NJERU**

**Tasnifu iliyowasilishwa katika Shule ya Mafuzu kwa Minajili ya Kutosheleza Baadhi ya Mahitaji ya Shahada ya Uzamili katika Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Chuka**

**CHUO KIKUU CHA CHUKA**
**JULAI 2018**

## UNGAMO NA IDHINI

**Ungamo**

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kuwasilishwa kwa mahitaji ya kutosheleza mahitaji ya shahada au stashahada katika Chuo Kikuu kingine chochote.

Sahihi……………………… Tarehe……………………

Mary Kanyua Njeru

(AM12/11707/13)

**Idhini**

Tasnifu hii imetahiniwa, ikapitishwa na kuwasilishwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa rasmi na Chuo Kikuu.

Sahihi……………………… Tarehe…………………..

Prof. John M. Kobia

Idara ya Fani

Chuo Kikuu cha Chuka

Sahihi ……………………… Tarehe…………………..

Prof. Peter K. Muriungi

Idara ya Fani

Chuo Kikuu cha Chuka

## HATILINZI

© 2018

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili, kuchapisha, kuhifadhi kwa mfumo wowote au kutoa sehemu yoyote ya tasnifu hii bila idhini ya mwandishi au Chuo Kikuu cha Chuka.

# TABARUKU

Naitabaruku kazi hii kwa mume wangu mpendwa Bw. Dennis Kinoti pamoja na binti zetu Shantel Makena Kinoti na Shanel Lulu Kinoti kwa mapenzi yao ya dhati na kwa kuwa mihimili muhimu katika maisha yangu. Kwa heshima na kumbukumbu ya marehemu dadangu Fridah Karegi, mwandani na mshauri wangu tangu utotoni, Mungu ailaze roho yako pema peponi.

## SHUKURANI


Kwanza ninamshukuru Maulana kwa kunipa afya njema na nguvu za kuendeleza kazi hii tangu mwanzo hadi mwisho wake. Shukurani za dhati na maalum ni kwa wahadhiri na wasimamizi wangu Prof. John M. Kobia, Prof. Peter K. Muriungi na Bw. Enock S. Matundura kwa ushauri na uelekezi wa kupigiwa mfano, ambao umeufanikisha utafiti huu. Mola awe nanyi siku zote za maisha yenu. Vilevile, nawashukuru kwa njia ya kipekee wahadhiri wote katika Idara ya Fani katika Chuo Kikuu cha Chuka hasa, Dr. Allan Mugambi na Bw. Kimathi Mwembu kwa mchango wao katika masomo na utafiti wangu. Ninawapa shukurani za dhati wanauzamili wenzangu kama vile Anne Njeri, Augustine Kirimi na James Rwaimba kwa kunichochea, kunihimiza na kunikosoa katika utafiti huu. Vilevile, ningependa kumshukuru Mwalimu Mkuu wa Shule ya Upili ya Kiriani Bw. Mbae Barine pamoja na walimu wengine katika Idara ya Lugha kwa kunihimiza na kushirikiana nami nilipokuwa nikifanya utafiti wangu. Siwezi kumsahau Bw. James Murithi ambaye alinitia shime na kunifaa kwa vitabu na makala mengine niliyohitaji katika kipindi cha masomo yangu.

Mume wangu mpendwa Bw. Dennis Kinoti anastahiki shukurani za pekee kwa kunifadhili kwa hali na mali licha ya majukumu mengi yaliyomkabili kazini. Aidha, uchochezi wake ulinipa ari ya kuendelea na utafiti huu. Ningependa pia kuwashukuru binti zangu Shantel Makena na Shanel Lulu kwa kunipa wakati mtulivu na kunitia shime katika utafiti huu kila nilipokosa matumaini. Kwa dadangu mpendwa Dorothy Kagendo, Mola aendelee kukubariki kwa kusimama nami katika maombi, kunishauri, kunitia shime na muhimu zaidi kuwashughulikia wanangu kila niliposafiri kufanya utafiti wangu.

Shukurani za dhati ziwaendee wazazi wangu wapendwa Bw. Agostino Njeru na Bi. Angera C. Njeru kwa kunilea na kujitoa mhanga kunielimisha hadi Chuo Kikuu licha ya kukabiliwa na changamoto nyingi maishani. Wazazi wangu wa ndoa Bw. Fredrick Micheni na Bi. Caroline Micheni, nawapa shukurani za kipekee kwa mchango wenu katika masomo yangu. Siwezi kamwe kuwasahau ndugu zangu Albert Murithi, John Ndeke na Margaret Kabunge kwa kufuatilia kila hatua niliyopiga katika utafiti huu. Mwisho, ningependa kutoa shukurani za dhati kwa wote walionifaa kwa namna moja au nyingine katika masomo na utafiti huu. Nyote nawaombea baraka za Mwenyezi Mungu.

# IKISIRI

Ardhi ni mojawapo ya rasilimali muhimu katika maisha ya mwanadamu. Suala la rasilimali ya ardhi ulimwenguni hasa nchini Kenya limekuwa nyeti na kuibua mijadala ya kijamii na kiakademia tangu enzi za ukoloni na hata baada ya uhuru. Utafiti huu ulikusudia kuchunguza jinsi suala la ardhi limesawiriwa na waandishi wa riwaya teule za Kiswahili. Riwaya zilizohakikiwa ni *Kufa Kuzikana* (Walibora, 2003) na *Kovu Moyoni* (Habwe, 2014). Msisitizo ulikuwa kuangazia jinsi wasanii wa riwaya hizi walivyoangazia migogoro kuhusu ardhi kuonyesha matatizo yaliyotokana na mikinzano kuhusu rasilimali hiyo pamoja na athari zake. Hii ni kwa msingi kuwa fasihi ni mojawapo ya nyenzo inayoweza kuchangia kuangazia matatizo yanayokumba jamii yoyote iwayo. Aidha, ni chombo muhimu cha kuelimisha, kuhamasisha na kuzindua jamii pana kuhusu matatizo yake. Madhumuni ya utafiti huu yalikuwa kuchunguza jinsi Walibora na Habwe wametumia fasihi kudhihirisha mizozo ya ardhi kwa kurejelea tungo zao, kuchunguza jinsi ambavyo walitumia fani za lugha kuwasilisha athari za mizozo ya ardhi na kubainisha suluhisho walilolitoa kama wasanii walio katika sehemu ya jamii zilizokumbwa na migogoro ya ardhi. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Baadaukoloni ambayo inahusishwa na kazi za Cesaire (1950), Fanon (1961) Said (1978) na Bhabha (1994), ambayo ilitumika ili kufafanua jinsi waandishi wa riwaya teule wamedhihirisha athari za ukoloni katika suala la ardhi. Utafiti huu ulitumia uteuzi wa sampuli wa kimakusudi kama njia ya kutathmini riwaya teule. Data ilipatikana kutoka kwenye matini iliyoteuliwa kimakusudi. Mtafiti alisoma riwaya husika kwa kina na kubaini maneno na mafungu ya maneno yaliyohusiana na suala la ardhi. Aidha, mtafiti alihakiki na kuchunguza jinsi wasanii wa riwaya za *Kufa Kuzikana* na *Kovu Moyoni* wamefafanua matatizo ya ardhi pamoja na suluhisho wanazotoa. Uchanganuzi wa kimaelezo wa data ulifanywa na kuwasilishwa kwa maandishi ya kinadhari. Ilibainika kuwa wasanii wa riwaya teule wamerejelea suala la ardhi nchini Kenya kama tatizo la jamii ambamo riwaya hizo ziliibuka huku wakiwasawiri Wakenya kama wahusika katika kazi zao kwa mujibu wa vipindi mbalimbali vya kihistoria. Vilevile, wameangazia mambo mbalimbali ambayo yanaweza kutumika ili kusuluhisha matatizo ya ardhi nchini. Utafiti huu utawanufaisha wahakiki wa fasihi katika kushadidia mtazamo kwamba, fasihi inaakisi kikamilifu matatizo yanayoibuka katika jamii ilimoibuka. Kwa hivyo, ni chombo madhubuti kinachoweza kutumiwa kutatua matatizo hayo.

## ABSTRACT

Land is an important resource in people`s lives. The land question has been a very sensitive and emotive issue which has elicited social and academic discourses in Kenya since the colonial period and also after independence. This study intended to find out how the sensitive land question has been tackled by the novelists of the selected Kiswahili texts. The novels that were analysed in this study are *Kufa Kuzikana* (Walibora, 2003) and *Kovu Moyoni* (Habwe, 2014). Literature is an important tool to educate and enlighten the wider public about its problems. Based on this, the emphasis was put on how the writers of these novels have focused on the conflicts about land to bring out the problems arising from the contestations over these resources and its consequences. The objectives of this study were to find out how the writers of the selected novels have used their literary work to portray the conflicts over land, find out how they have used stylistic devices in *Kufa Kuzikana* and *Kovu Moyoni* to portray the problems arising from the land issues and to determine the mitigation strategies postulated by the writers of the selected Kiswahili novels as artists in the society faced with land conflicts. The research was guided by Post-Colonial theory which is associated with the works of Cesaire (1950), Fanon (1961), Said (1978) and Bhabha (1994). The theory was used to evaluate how the artists of the selected Kiswahili novels have portrayed the influence of the Colonial master on land issues which have led to frequent conflicts and also offer basis on which the Kenyan society is structured and influenced by access to land. The study analysed and investigated how the writers of *Kufa Kuzikana* and *Kovu Moyoni* have delt with land problems as well as the solutions that they provide. The researcher purposively selected *Kufa Kuzikana* (Walibora, 2003) and *Kovu Moyoni* (Habwe, 2014) for the study. These texts were closely read to get the qualitative data required. Close-textual reading was done focusing on the words and phrases related to the land issues discussed in the novels, use of the stylistic devices to portray the concequences of land issues as well as the solutions that they have given. Data analysis was presented in descriptive prose. The findings of this research show that the writers of the selected Kiswahili novels have focused on land issues in Kenya as an issue in the society in which the novels were created as well as portraying Kenyans as characters in their work in the context of various historical periods. In addition, the writers of the selected texts have focused on various ways that can be used to resolve land conflicts. The study will benefit literary critics in confirming that indeed literature reflects the problems in the society in which it emanates hence can be used to resolve those problems.

## YALIYOMO

**UNGAMO NA IDHINI**..........ii

**HATILINZI**.......... iii

**TABARUKU**..........iv

**SHUKURANI**..........v

**IKISIRI**..........vi

**ABSTRACT**..........vii

**YALIYOMO**.......... viii

**SURA YA KWANZA**..........1

**UTANGULIZI**..........1

1.1 Usuli wa Mada..........1
1.2 Suala la Utafiti..........4
1.3 Madhumuni ya Utafiti..........4
1.4 Maswali ya Utafiti..........5
1.5 Umuhimu wa Utafiti..........5
1.6 Upeo wa Utafiti..........5
1.7 Machukulio..........6
1.8 Maelezo ya Istilahi..........7

**SURA YA PILI**..........8

**MWAUO WA MAANDISHI**..........8

2.0 Utangulizi..........8
2.1 Suala la Ardhi Nchini Kenya Kabla ya Ukoloni..........8
2.2 Suala la Ardhi Nchini Kenya Wakati wa Ukoloni..........9
2.3 Suala la Ardhi Nchini Kenya Baada ya Uhuru..........10
2.4 Athari za Mizozo ya Ardhi..........12
2.5 Suluhisho la Mizozo ya Ardhi..........14
2.6 Suala la Ardhi Katika Fasihi..........17
2.7 Maandishi Kuhusu Kazi za Walibora na Habwe..........19
2.8 Misingi ya Kinadharia..........21
2.9 Muhtasari wa Riwaya ya *Kovu Moyoni* (Habwe, 2014)..........24
2.10 Muhtasari wa Riwaya ya *Kufa Kuzikana* (Walibora, 2003)..........25
SURA YA TATU..........26
3.0 Utangulizi..........26
3.1 Eneo la Utafiti..........26
3.2 Uteuzi wa Sampuli..........26
3.3 Njia za Kukusanya Data..........26
3.4 Uchanganuzi wa Data..........27

**SURA YA NNE**..........28

**JINSI MIZOZO YA ARDHI ILIVYOSAWIRIWA KATIKA RIWAYA ZA *KOVU MOYONI* NA *KUFA KUZIKANA***..........28

4.0 Utangulizi....28
4.1 Chanzo cha Mizozo ya Ardhi....28
4.2 Mizozo ya Ardhi na Siasa....31
4.3 Mizozo ya Ardhi na Ukabila....36
4.4 Mchango wa Serikali katika Mizozo ya Ardhi....37
4.5 Athari za Mizozo ya Ardhi....38
4.5.1 Mauaji....39
4.5.2 Ukimbizi....40
4.5.3 Ubakaji....42
4.5.4 Visasi....43
4.5.5 Kuibuka kwa Wanamgambo....44
4.5.6 Majuto....45
4.5.7 Umaskini....46
4.5.8 Kuzorota kwa Hali ya Uchumi....47
4.5.9 Magonjwa....49
4.5.10 Ukosefu wa Usalama....50
4.5.11 Kuathiriwa kwa Masomo....51
4.6 Hitimisho....52
**SURA YA TANO....53**
**NAMNA FANI ZA LUGHA ZINAVYOWASILISHA ATHARI ZA MIZOZO YA ARDHI KATIKA RIWAYA ZA *KOVU MOYONI* NA *KUFA KUZIKANA*..53**
5.0 Utangulizi....53
5.1 Jazanda....53
5.2 Taswira....56
5.3 Kinaya....57
5.4 Mbinu Rejeshi....58
5.5 Sitiari....59
5.6 Tashihisi....61
5.7 Tashbihi....62
5.8 Barua....63
5.9 Hitimisho....64
**SURA YA SITA....65**
**MCHANGO WA ASASI MBALIMBALI KATIKA KUSULUHISHA MATATIZO YA ARDHI KATIKA RIWAYA ZA *KOVU MOYONI* NA *KUFA KUZIKANA*....65**
6.0 Utangulizi....65
6.1 Mchango wa Serikali....65
6.2 Nafasi ya Dini....68
6.3 Mashirika yasiyo ya Serikali....71
6.4 Viongozi wa Kisiasa....73
6.5 Juhudi za Wananchi....74
6.6 Vyombo vya Dola....75
6.6.1 Korti na Magereza....75
6.6.2 Askari....77

6.7 Vyombo vya Habari ........ 79
6.8 Wapatanishi ........ 81
6.9 Mielekeo Chanya ya Wananchi ........ 82
6.10 Hitimisho ........ 84

**SURA YA SABA ........ 85**

7.0 Muhtasari ........ 85
7.1 Hitimisho ........ 85
7.2 Mapendekezo ya Utafiti wa Baadaye ........ 86

**MAREJELEO ........ 88**

**KIAMBATISHO 1: IDHINI YA UTAFITI ........ 93**

**KIAMBATISHO 2: KIBALI CHA UTAFITI ........ 94**

## ORODHA YA VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| **ANC** | African National Congress |
| **EACC** | Ethics and Anti-Corruption Commission |
| **GoK** | Government of Kenya |
| **IDMC** | Internal Displacement Monitoring Centre |
| **ISS** | Institute of Security Studies |
| **LDGI** | Land Development and Governance Institute |
| **MSF** | Medicine Sans Frontiers |
| **NARC** | National Rainbow Coalition |
| **NCCK** | National Council of Churches of Kenya |
| **NCRC** | National Crime Research Centre |
| **NLC** | National Land Commission |
| **ODM** | Orange Democratic Movement |
| **PNU** | Party of National Unity |
| **SLDF** | Sabaot Land Defence Force |
| **TJRC** | Truth Justice and Reconciliation Commission |
| **TUKI** | Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili |

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.1 Usuli wa Mada

Ardhi ni rasilimali muhimu katika maisha ya mwanadamu. Ni chanzo cha uhai kwa watu wengi na hasa chanzo cha mahitaji yake ya msingi kama vile chakula na malazi. Uwezo wa kumiliki ardhi ni sifa kuu ya maendeleo na mabadiliko ya kisiasa. Isitoshe, maendeleo mengi yaliyowahi kutokea kote ulimwenguni, Kenya ikiwemo yanahusiana kwa njia moja au nyingine na matumizi ya ardhi. Kwa sababu hii, haja ya kuangazia suala la ardhi haliwezi kupuuzwa (Chege, 2013).

Kulingana na Njogu na wenziwe (2015), suala la ardhi ndilo linatawala siasa na uchumi katika mataifa mengi barani Afrika, Kenya ikiwemo. Wanaendeleza madai haya kwa kusema kuwa suala la ardhi limeweza kuelekeza harakati za ukombozi katika maeneo yote barani Afrika. Vilevile, ardhi imehusishwa na mapambano makali wanajamii wanapopigania mamlaka na rasilimali. Kwa mujibu wa Njogu na wenziwe, ni wajibu wa asasi mbalimbali katika jamii kuvumbua jinsi ambavyo mageuzi ya ardhi yanaweza kutekelezwa ili kuhakikisha maendeleo endelevu. Yakitekelezwa vyema, mageuzi ya ardhi pamoja na maliasili nyinginezo zinaweza kuchangia katika kuleta usawa, umoja na maendeleo shirikishi. Vilevile, zinaweza kupunguza umaskini, kulinda haki za wanawake za umiliki wa ardhi na kulinda haki za wafugaji, wasikwao na jamii za asili.

Umuhimu wa ardhi umeangaziwa na Gatimu (2014) anayeeleza kuwa tangu enzi za ukoloni nchini Kenya, suala la ardhi limekuwa nyeti na chanzo cha mizozo ya mara kwa mara. Dai hili linasisitiza umuhimu wa ardhi kwa mkenya, ambaye maisha yake kwa kiwango fulani yanahitaji mapato kutoka kwa ardhi. Vilevile, kilimo ni uti wa mgongo wa uchumi nchini Kenya. Hata hivyo, ni wazi kuwa matatizo yanayotokana na ardhi yameendelea kuwepo kwa ajili ya ulegevu wa mifumo ya kisiasa iliyokuwepo tangu enzi za mkoloni.

Akieleza kuhusu umuhimu wa ardhi, Maina (2015) anasema kuwa nchini Kenya, ardhi inachukuliwa kama kipengele muhimu cha maisha katika jamii yoyote ile. Isitoshe, ardhi ni nguzo kwa rasilimali na harakati muhimu za kibiolojia, inadumisha maishilio ya Wakenya wengi, na inahusu urithi wa kitamaduni muhimu kwa Wakenya wengi. Kwa mujibu wa Maina, suala na mizozo ya ardhi ni mojawapo ya masuala yanayohusu

jamii ya Kenya. Aidha, iwapo itatanguliwa kwa muda mrefu inaweza kuathiri maingiano ya jamii, kusababisha vifo, kuleta athari hasi katika maendeleo na matumizi ya ardhi na hatimaye kuathiri uchumi kwa jumla.

Kutokana na umuhimu wa ardhi kwa maendeleo ya jamii, migogoro ya ardhi ya mara kwa mara imeshuhudiwa katika maeneo mbalimbali nchini Kenya. Kadhalika, migogoro mingi ya ardhi imekuwa ikitokea baina ya wakulima na wafugaji, wakulima na wawekezaji, mtu kwa mtu na kijiji kwa kijiji ambayo wakati mwingine imekuwa ikisababisha watu kupoteza maisha, kupata ulemavu na upotevu wa mali zao (Mwathane, 2010).

Licha ya ardhi kuwa rasilimali muhimu kwa jamii nyingi nchini Kenya, suala la umiliki wa ardhi limezua matatizo katika jamii, yakiwemo, vita vya kikabila, umaskini na ukosefu wa elimu. Hii ndiyo sababu wasanii mbalimbali pamoja na wataalamu wa masuala ya ardhi wamezungumzia suala hili. Aidha, kutokana na kuvumbuliwa kwa maliasili katika sehemu mbalimbali nchini, hasa mafuta na gesi, wanasiasa na viongozi wenye ushawishi mkubwa serikalini wamejipatia mashamba makubwa katika sehemu hizo kwa lengo la ubazazi. Ili kushughulikia tatizo hili sugu, linaloonekana kuliangusha taifa, nyenzo mwafaka itakuwa kuanza kutatua suala la ardhi nchini Kenya kikamilifu.

Migogoro ya ardhi barani Afrika, Kenya ikiwemo imejitokeza katika jamii nyingi na kwa viwango mbalimbali. Migogoro hii imeendelea kukua kwa kasi kati ya makundi mbalimbali ya watumiaji wa ardhi huku ikisababisha athari nyingi na mbaya miongoni mwa wanajamii. Hivyo, imekuwepo haja na msukumo wa kijamii wa kukubaliana na migogoro ya ardhi kila inapotokea kwa lengo la kuepusha ama kudhibiti utokeaji na athari zake.

Hata hivyo, kumekuwa na tume mbalimbali za kushughulikia suala la ardhi nchini Kenya. Kwa mfano, baada ya vita vya kikabila baada ya uchaguzi mkuu wa mwaka 1997, kuliteuliwa Tume ya Akiwumi ya mwaka wa 1998. Tume hiyo ilichunguza uhusiano wa mizozo hiyo na ugawaji na umiliki wa ardhi kote nchini Kenya hasa katika mikoa ya Bonde la Ufa na Pwani. Tume ya Njonjo (1999) ilikashifu utendakazi wa Halmashauri ya Ardhi ya kitaifa. Tume ya Ndung`u iliundwa mwaka wa 2003 ambayo ilichunguza suala la ardhi ambapo waliomiliki ardhi kinyume cha sheria walifaa

kuchukuliwa hatua mwafaka. Katika mwaka wa 2009, Tume ya Ukweli, Haki na Maridhiano (TJRC) iliteuliwa. Kwa mujibu wa Tume hii, Wakenya wengi wanatumia ardhi kama njia mojawapo ya kimsingi ya kuwainua kiuchumi. Vilevile umiliki ardhi na matumizi yake hutawala nyenzo zao muhimu za kuzalisha mali na kuzilinda familia zao, pia huwapa nafasi kiuchumi na kisiasa katika familia zao (Masibo, 2015).

Licha ya juhudi za serikali kupitia tume zilizoteuliwa kuangazia suala la ardhi nchini Kenya kwa miaka mingi, kumetokea mikinzano mingi ambayo chanzo chake ni ardhi. Kwa mujibu wa Nyiri (2014), jamii nyingi nchini Kenya kwa muda mrefu zimejaribu kwa namna yoyote ile kusitiri masilahi yao, njia mojawapo ambayo hutumika ni mizozo ambapo wamepigania ardhi, mamlaka na mifugo miongoni mwa masuala mengine.

Fasihi inaweza kutumiwa katika kuangazia matatizo ya kijamii na mojawapo ya matatizo hayo ni suala la ardhi. Kwa mujibu wa Njogu na Chimerah (1999), fasihi inafungamanishwa na maisha ya binadamu. Kazi ya fasihi huenda isitoe habari kamili kuhusu maisha yalivyo lakini huwapa wanajamii miongozo ya ukweli kutokana na uteuzi na uwasilishaji wa tajriba maalumu za jamii.

Kwa mujibu wa Njogu (1997), fasihi ni kielelezo cha hali halisi katika jamii. Aidha, anasisitiza kuwa fasihi ni amali ya jamii ambapo msanii anachukuliwa kama mmoja katika jamii na mwenye nafasi yake katika jamii hiyo. Kwa hivyo, fasihi ina jukumu kwa jamii katika kiwango cha mtu binafsi na vilevile kiwango cha jamii kwa jumla. Kutokana na maelezo haya, waandishi wa riwaya za *Kovu Moyoni* na *Kufa Kuzikana* wameangazia mizozo ya ardhi nchini Kenya katika nyakati mbalimbali ili kutoa mwelekeo kwa wanajamii kuhusu namna ya kutatua mizozo hiyo na hatimaye kupata suluhisho la kudumu.

Kwa kuwa fasihi ni mojawapo ya nyenzo inayoweza kuchangia katika kuangazia matatizo yanayoikumba jamii yoyote iwayo, utafiti huu ulikusudia kuchunguza jinsi ambavyo suala la ardhi limesawiriwa na waandishi wa riwaya teule za Kiswahili. Hii ilitokana na mtazamo kwamba fasihi inaakisi kikamilifu masuala ya jamii ilimoibuka na inaweza kutumika katika kusuluhisha matatizo ya kijamii pakiwemo suala nyeti la ardhi. Wellek na Warren (1954) wanadai kuwa fasihi huielezea jamii kwa msingi kuwa \`Fasihi ni kioo cha jamii\`. Riwaya zilizohakikiwa katika utafiti huu ni *Kufa Kuzikana* (Walibora, 2003) na *Kovu Moyoni* (Habwe, 2014).

Kwa mujibu wa Gonye na wenziwe (2012), fasihi ni zao la kipindi ambacho inaibuka kwa hivyo huteka vigambo, majanga na mafanikio ya kipindi fulani maalum kwa hivyo huteka mshipa na mpigo wa jamii. Kutokana na maelezo haya, waandishi wa riwaya teule walijaribu kuteka na kueleza kiubunifu kipindi katika historia ya Kenya ambapo suala la ardhi limezua mijadala mingi ya kiakademia na kijamii. Hii ni kutokana na mizozo ya ardhi ambayo imeshuhudia nchini ambapo wao ni wenyeji, huku wakiwasawiri wakenya kama wahusika katika kazi zao. Kwa mfano, mwaka wa 1992 eneo la Molo Kaunti ya Nakuru, 1997 eneo la Likoni katika Kaunti ya Mombasa, 2007 hadi 2008 Bonde la Ufa, 2005 katika Mlima Elgon na vilevile 2014 eneo la Mpeketoni kaunti ya Lamu. Kwa hivyo, mtafiti alichagua riwaya za *Kovu Moyoni* na *Kufa Kuzikana* ili kubainisha jinsi ambavyo waandishi wa riwaya hizo wameangazia mizozo ya ardhi.

### 1.2 Suala la Utafiti

Ardhi ni mojawapo ya rasilimali muhimu katika maisha ya mwanadamu kote ulimwenguni. Nchini Kenya, suala hili limeibua mijadala ya kijamii na kiakademia tangu enzi za ukoloni na hata baada ya uhuru. Vita vya ukombozi kutokana na utawala dhalimu wa ukoloni katika mataifa mengi barani Afrika vilichochewa na msukumo wa utwaaji wa ardhi kutoka kwa wakoloni. Ingawa fasihi ni mojawapo ya nyenzo inayoweza kuchangia katika kuangazia matatizo yanayoikumba jamii yoyote ile, ni wahakiki wachache wa fasihi ambao wamejishughulisha katika kutathmini umuhimu wa fasihi kwa jumla katika kuangazia migogoro inayohusu rasilimali ya ardhi. Hata hivyo, mchango wa riwaya ya Kiswahili katika kuangazia migogoro ya ardhi haujaangaziwa. Utafiti huu unalenga kuziba pengo hilo kwa kuchunguza jinsi ambavyo suala nyeti la ardhi limesawiriwa na waandishi wa riwaya teule za Kiswahili kwa kurejelea *Kufa Kuzikana* na *Kovu Moyoni,* ili kuibua mjadala wa kitaifa kuhusu suala hilo na kuinua viwango vya mishikamano ya kijamii, amani na umoja, masuala ambayo ni muhimu katika maendeleo endelevu nchini Kenya.

### 1.3 Madhumuni ya Utafiti

Madhumuni ya utafiti huu ni:

i) Kubainisha jinsi watunzi wa riwaya za *Kufa Kuzikana* na *Kovu Moyoni* walivyosawiri mizozo ya ardhi.

ii) Kueleza namna watunzi wa riwaya za *Kufa Kuzikana* na *Kovu Moyoni* walivyotumia fani za lugha kuwasilisha athari za mizozo ya ardhi.
iii) Kutathmini mchango wa asasi mbalimbali katika kusuluhisha matatizo ya ardhi kama ilivyosawiriwa katika *Kufa Kuzikana* na *Kovu Moyoni.*

**1.4 Maswali ya Utafiti**

Maswali yafuatayo yalitumiwa kuongoza utafiti huu:

i) Je, watunzi wa riwaya za *Kufa Kuzikana* na *Kovu Moyoni* walisawiri mizozo ya ardhi kwa jinsi gani?
ii) Watunzi wa riwaya za *Kufa Kuzikana* na *Kovu Moyoni* walitumia vipi fani za lugha kuwasilisha athari za mizozo ya ardhi?
iii) Je, ni upi mchango wa asasi mbalimbali katika kusuluhisha matatizo ya ardhi kama ilivyosawiriwa katika riwaya za *Kufa Kuzikana* na *Kovu Moyoni*?

**1.5 Umuhimu wa Utafiti**

Utafiti huu utawanufaisha wahakiki wa fasihi katika kushadidia mtazamo kwamba, fasihi huakisi kikamilifu matatizo yanayoibuka katika jamii ilimoibuka na ni chombo madhubuti kinachoweza kutumiwa kutatua matatizo hayo. Aidha, utatoa mchango wake katika mijadala ya kiakademia kuhusu suala la ardhi. Isitoshe, Utafiti huu utachangia katika uhakiki wa riwaya za Kiswahili kwa kuangazia kazi za waandishi wanaozingatia Nadharia ya Baadaukoloni katika kutunga kazi zao. vilevile, utafiti huu utaongeza maarifa ya fasihi hasa kwa wasomi wanapochambua dhamira, maudhui, mbinu na wahusika katika riwaya ya Kiswahili.

**1.6 Upeo wa Utafiti**

Utafiti huu unashughulikia usawiri wa suala la ardhi katika riwaya teule za Kiswahili. Fasihi ya Kiswahili ni uwanja mpana ambao unahusisha tanzu mbalimbali kama vile riwaya, tamthilia, hadithi fupi na ushairi. Hata hivyo, utafiti huu umejikita katika riwaya kwa sababu tofauti na tanzu nyinginezo za fasihi, riwaya imejizatiti katika kuelezea nyanja nyingi zaidi za maisha. Aidha, ni utanzu ambao huweza kumsogeza msomaji kwenye chanzo cha uhalisi au ukweli wa jambo na kumpa njia ya kuwazia au kujadili jambo kwa upana zaidi. Kwa hivyo, utafiti huu ulijikita katika kushughulikia riwaya teule: *Kufa Kuzikana* (Walibora, 2003) na *Kovu Moyoni* (Habwe, 2014).

Riwaya hizi ziliteuliwa kimakusudi kwa sababu zimeandikwa kwa lugha ya Kiswahili na miongoni mwa maudhui makuu katika tungo hizi ni mizozo ya ardhi na hivyo kuafiki mada ya utafiti huu. Zaidi ya hayo, riwaya za *Kufa Kuzikana* na *Kovu Moyoni* ziliteuliwa kwa kuwa zimelenga mizozo ya ardhi nchini Kenya katika vipindi maalum. Kwa mfano, riwaya ya *Kufa Kuzikana* inaangazia mizozo ya ardhi kwa misingi ya kikabila nchini Kenya baada ya uchaguzi mkuu wa mwaka 1997 katika eneo la Bonde la Ufa na Pwani, nayo riwaya ya *Kovu Moyoni* imeangazia mizozo ya ardhi katika eneo la Mlima Elgon iliyoendelezwa na wanamgambo wa Sabaot Land Defence Forces (SLDF). Kando na riwaya za *Kufa Kuzikana* na *Kovu Moyoni*, utafiti huu pia ulirejelea vitabu na makala mengine ambayo yalishadidia baadhi ya hoja kuu katika kazi hii. Isitoshe, utafiti huu ulijikita katika Nadharia ya Baadaukoloni ambayo ilitumika ili kueleza na kufafanua jinsi dhuluma za kihistoria kutokana na ukoloni zinachangia mizozo ya kila mara inayotokana na suala nyeti la ardhi kama ilivyojitokeza katika riwaya za *Kufa Kuzikana* na *Kovu Moyoni*.

### 1.7 Machukulio

Ilichukuliwa kwamba riwaya zilizoteuliwa zilikuwa na data ya kutosha kuhusu suala la ardhi kwa jumla. Vilevile, ilichukuliwa kwamba riwaya za *Kufa Kuzikana* (Walibora, 2003) na *Kovu Moyoni* (Habwe, 2014) zilizoteuliwa kwa uchanganuzi zilikuwa kiwakilishi tosha cha mtazamo wa waandishi wa riwaya za Kiswahili kuhusu suluhisho la mizozo ya ardhi.

## 1.8 Maelezo ya Istilahi

Utafiti huu ulitumia istilahi zifuatazo ambazo zilifafanuliwa kwa kurejelea matumizi yake katika utafiti:

**Ardhi:** ni rasilimali ya kimsingi ya Kenya na ndio msingi wa maisha ya watu.

**Athari za Mizozo:** Ni mabadiliko yanayoletwa au kusababishwa na mabishano kwa watu.

**Mizozo ya Ardhi:** Ni mabishano yanayosababisha kutosikilizana kwa sababu ya suala la ardhi.

**Maskwota:** Ni watu ambao huishi katika nyumba au shamba bila hatimiliki au idhini.

**Mwanamgambo:** Ni raia anayejitolea kufanya kazi ya ulinzi; askari mgambo.

**Riwaya:** Ni hadithi ndefu ya kubuni, yenye visa vingi, wahusika zaidi ya mmoja na yenye mazungumzo na maelezo yanayozingatia kwa undani na upana, maisha ya jamii.

**Ukimbizi wa Ndani:** Raia wa nchi anayekimbia kwa sababu za kisiasa kutoka sehemu anayoishi au anapowekeza na kufanya makazi yake, baada ya makazi yao kuchomwa na mali yao kuangamizwa, kwenda kuishi kwenye kambi za usalama au wakimbizi.

**Uhalisia:** Ni dhana katika uhakiki wa kifasihi inayosisitiza usawiri wa matukio au maisha katika fasihi kama yalivyo katika maisha ya kila siku.

**Utabaka:** Ni migawanyiko miongoni mwa wanajamii kwa misingi ya uwezo wao wa kiuchumi.

**Usawiri:** Ni namna jambo fulani linavyoonyeshwa au kupambanuliwa.

# SURA YA PILI
# MWAUO WA MAANDISHI

## 2.0 Utangulizi

Sura hii imeshughulikia maandishi mbalimbali ambayo yanahusiana na mada ya utafiti ili kushadidia pengo la utafiti huu. Katika kufanya hivyo, masuala yafuatayo yameangaziwa: Suala la ardhi nchini Kenya kabla ya ukoloni, wakati wa ukoloni na baada ya uhuru, tafiti kuhusu athari za mizozo ya ardhi na suluhisho la mizozo ya ardhi kama lilivyosawiriwa na watafiti, suala la ardhi katika fasihi kwa jumla, tafiti mbalimbali katika riwaya za Walibora na Habwe zilizohusiana na utafiti huu na pia kueleza msingi wa nadharia iliyotumika. Katika sura hii mtafiti amehitimisha kwa kuangazia muhtasari wa riwaya za *Kovu Moyoni* (Habwe, 2014) na *Kufa Kuzikana* (Walibora, 2003).

## 2.1 Suala la Ardhi Nchini Kenya Kabla ya Ukoloni

Kwa mujibu wa Odhiambo (1974), jamii ya Afrika ya Karne ya Kumi na Tisa, ilijitosheleza katika hali ya kiuchumi. Aidha, historia ya Kenya inadhihirisha kwamba kabla ya majilio ya mkoloni, ardhi ilimilikiwa na jamii. Maelezo haya yana umuhimu katika utafiti huu kwa sababu yamesaidia katika kuchunguza asili ya mizozo ya ardhi nchini Kenya. Hii ni kwa sababu kabla ya kuja kwa mkoloni nchini, hapakuwa na matatizo yoyote kuhusu umiliki wa ardhi kwani umiliki wa kibinafsi haukuwepo.

Kwa mujibu wa Gatimu (2014), kabla ya ukoloni nchini Kenya, hakukuwepo mikakati ya kubuni mwongozo kuhusu suala la umiliki na usimamizi wa ardhi. Hata hivyo, sheria za kitamaduni zilimudu mahusiano ya jamii mbalimbali za wakulima na walisha mifugo wa kuhamahama katika usimamizi wa sheria za ardhi. Hali hii ilisababisha jamii ya wakati huo kuwa na amani na utulivu kwa sababu katika nchi nzima kulikuwa na ardhi ya kutosha iliyorithisha mahitaji ya wanajamii.

Njogu na wenziwe (2015) wanatambua kwamba rasilimali ya ardhi ilikuwa chanzo cha mapambano makubwa nchini Kenya wanajamii waliposhirikiana kujikomboa kutoka kwa ukoloni na hasa kupata manufaa yanayotokana na ardhi. Aidha, wanaafikiana na maoni ya Lumumba (2005) anapoeleza kuwa vita vya ukombozi kutokana na utawala dhalimu wa ukoloni katika mataifa mengi barani Afrika, vilichochewa na msukumo wa utwaaji wa ardhi kutoka kwa wakoloni. Maelezo haya yanadhihirisha hali ngumu

ambayo Wakenya walipitia chini ya Wakoloni pakiwemo kukosa haki ya kumiliki ardhi, hali iliyochochea msukumo wa vita vya ukombozi.

### 2.2 Suala la Ardhi Nchini Kenya Wakati wa Ukoloni

Nyukuri (1997) anaeleza kuwa kwa muda mrefu katika historia ya Kenya, suala la ardhi limekuwa chanzo cha mizozo katika maeneo mengi nchini. Aidha, anatambua kuwa asili ya suala la ardhi nchini Kenya ni katika historia ya nyakati za Ukoloni, ambapo Wakoloni walinuia kuifanya sehemu hii ya Afrika kuwa nchi yao. Kwa hivyo, kwa mujibu wa historia, wakoloni walinyakua ardhi kubwa yenye rutuba kutoka kwa Wakenya, huku wakenya hao wakilazimika kuishi kama maskwota. Kwa sababu hii, suala la ardhi likawa kichocheo kikubwa cha vita vya ukombozi. Ndiposa Nyukuri anasema kuwa suala la ardhi lilikuwa sababu kuu ya uasi wa Mau Mau wa kati ya 1952 hadi 1956 nchini Kenya.

Kwa mujibu wa Ake (1996), serikali ya kikoloni nchini Kenya ilikuwa na nguvu na mamlaka kuhusu masuala ya ardhi. Isitoshe, wakoloni waliwashurutisha waafrika kufanya kazi na vilevile walitupilia mbali mifumo yao ya utawala. Hatua hizi zilipele kea kuvunjika kwa mishikamano ya kiasili katika uzalishaji mali, kutengana kwa wanajamii na pia kuzuka kwa tabaka la chini. Maelezo haya yanaonyesha kuwa Wakoloni walitambua umuhimu wa ardhi ndiposa walitumia nguvu kuinyakua kutoka kwa wakenya. Aidha, maelezo hayo yameweka msingi wa utafiti huu kwa sababu umechunguza usawiri wa suala la ardhi katika riwaya za *Kufa Kuzikana* na *Kovu Moyoni* na kueleza ni kwa nini suala la ardhi huzua matatizo mengi nchini Kenya.

Maelezo haya yanadhihirisha kwamba matatizo ya ardhi nchini Kenya yalianza baada ya kufika kwa mkoloni ambaye alinyakua mashamba yaliyokuwa yamemilikiwa na wakenya. Hii ni kwa sababu kufika kwa Mkoloni nchini Kenya kuliibadilisha hali ya umiliki wa ardhi. Aidha, Sheria za umiliki wa ardhi zilizowekwa na mkoloni zilikuwa na nia ya kuwaendeleza wakoloni kiuchumi huku zikiwanyanyasa waafrika kiuchumi na kisiasa. Hata baada ya mkoloni kuondoka, hali hii ilibakia vivyo hivyo kwani idadi kubwa ya ardhi iliachwa mikononi mwa wasomi na washiriki wa karibu wa wakoloni waliochukua hatamu za uongozi kuanzia mwaka 1963. Utafiti huu umechunguza athari za mizozo ya ardhi nchini Kenya kama tatizo ambalo limekuwepo tangu nyakati za

ukoloni nchini ili kuchunguza suluhisho la matatizo hayo kama lilivyosawiriwa na waandishi wa riwaya teule.

**2.3 Suala la Ardhi Nchini Kenya Baada ya Uhuru**

Nyiri (2014) anaeleza kuwa nchini Kenya baada ya uhuru, kulikuwa na msemo wa `uhuru na umoja`, ambao ulisawiri watu wote nchini kuwa na usawa, jambo lililochangia kuwepo kwa amani tele katika kila pembe ya nchi. Miaka miwili baadaye, Kenya ilirejelea migawanyiko kwa misingi ya kikabila kama vile Waluo, Wakikuyu, Wakalenjin na wengine. Mizozo mingi iliyotokea baadaye ilikuwa na msingi katika siasa lakini kila mara ilichukua mielekeo ya kikabila. Kwa mujibu wa Nyiri, miongoni mwa mambo ambayo yanaweza kusababisha mizozo katika jamii ni ubaguzi katika ugawaji wa rasilimali, ndoa za kisiasa na talaka kwa hiari, suala la ardhi na migogoro ya kisiasa.

Njuguna na Mbaya (2009) wanatambua kuwa ardhi imekuwa na itaendelea kuwa boma kubwa la uchumi wa Kenya, ambapo zaidi ya asilimia themanini ya watu nchini hutegemea kilimo katika maisha yao. Rasilimali hii imeendelea kuchukua jukumu adhimu katika maendeleo ya kiuchumi na kisiasa nchini. Kwa hivyo umiliki wake, ugawaji na matumizi yake ni mambo yanayowahusu Wakenya wengi. Ardhi imeendelea kuwa chanzo cha mizozano mingi nchini Kenya ambapo baadhi ya mambo yanayosababisha mizozano hiyo ni kuongezeka kwa idadi ya watu, ulimaji wa kibiashara na ustaarabu. Hata hivyo, mifumo ya kisasa ya umiliki wa ardhi huenda haina uwezo wa kusuluhisha mizozo hiyo (Njogu na wenziwe, 2015)

Suala la ardhi limekuwa ni tatizo kubwa katika nchi ya Kenya, aidha kumekuwa na vurugu katika nyakati mbalimbali nchini zilizohusiana na suala la ardhi. Kwa mfano, kulikuwa na vita katika mkoa wa Bonde la Ufa mwaka 1992, 1997, 2002 na 2007 hadi 2008. Mizozo hii ya ardhi ni dhihirisho la uhasama ambao hauwezi kutatuliwa tu kupitia mfumo wa mageuzi (Kimenyi na Ndung'u, 2005). Huenda jambo hili ndilo lililomchochea Walibora (2003) kuandika kitabu chake *Kufa Kuzikana* ili kuangazia suala la ardhi kama chanzo cha mizozo nchini Kenya na hasa maeneo ya Bonde la Ufa na Magharibi mwa Kenya, ambapo Walibora anaonyesha kuwa tofauti za kikabila huchochea mizozo ya ardhi. Vilevile, Habwe (2014) katika riwaya ya *Kovu Moyoni* anamulika matukio katika Wilaya ya Mlima Elgon mwaka wa 2005. Hata hivyo,

mizozo kutokana na ardhi iliyozua athari kubwa zaidi nchini Kenya ilifikia kilele wakati wa vita vya baada ya uchaguzi mkuu kati ya mwaka 2007 hadi 2008. (Calas, 2008).

Udhalimu wa kihistoria unadhihirika kupitia kuwepo kwa maskwota, mizozo ya ardhi, na masalio ya madai ya ardhi. Sheria za ardhi za baada ya Uhuru za serikali hazijasuluhisha wala kutatua dhuluma hizo. Aidha, Katiba ya Kenya (2010) inatambua suala hili na hivyo ilihitaji serikali kuangazia na kutatua dhuluma za kihistoria pakiwemo suala la ardhi. Hata hivyo, jambo lisilokuwa wazi ni namna na kima cha uwezekano wa kupata suluhisho la kudumu ambalo Walibora (2003) na Habwe (2014) wamesawiri katika riwaya zao.

Hata ingawa hadhi inayohusishwa na umiliki wa ardhi nchini Kenya huzua mizozo ya ardhi, hakuna maelezo kamili ambayo yanaweza kufafanua kikamilifu hali na mwelekeo wa mizozo ya ardhi nchini Kenya, au Barani Afrika kwa jumla. Masuala ya umiliki na matumizi yake huwa miongoni mwa visababishi vya mizozo ya ardhi nchini Kenya na hivyo kuchangia si tu mapigano bali pia umaskini na kuzorota kwa uchumi. (Wakhungu, Nyukuri &Huggins, 2008). Kwa msingi huu, utafiti huu ulinuia kuchunguza namna ambavyo waandishi wa riwaya za *Kufa Kuzikana* na *Kovu Moyoni* walivyosawiri suala la ardhi hasa chanzo na athari za matatizo ya ardhi nchini Kenya na kutathmini suluhisho walilotoa kwa matatizo hayo.

Licha ya kuongezeka kwa matukio ya mizozo ya ardhi nchini Kenya, tafiti za awali katika mada hii hasa katika Kiswahili ni chache. Fasihi ni mojawapo ya nyenzo inayoweza kuchangia katika kuangazia matatizo yanayoikumba jamii yoyote ile. Aidha, fasihi ni chombo muhimu cha kuelimisha, kuhamasisha na kuzindua jamii pana kuhusu matatizo yake. Kwa msingi huo, utafiti huu ulikusudia kuchunguza jinsi ambavyo suala nyeti la ardhi lilivyosawiriwa na waandishi wa riwaya teule za Kiswahili. Riwaya zilizohakikiwa katika utafiti huu zilikuwa *Kufa Kuzikana* (Walibora, 2003) na *Kovu Moyoni* (Habwe, 2014). Msisitizo ulikuwa kuangazia jinsi wasanii wa riwaya hizi walivyoangazia migogoro kuhusu ardhi kuonyesha matatizo yanayotokana na mikinzano kuhusu rasilimali hiyo, athari na pia suluhisho lake.

## 2.4 Athari za Mizozo ya Ardhi

Hermunen (2004) alichunguza sera za matumizi ya ardhi nchini Kenya. Lengo kuu lilikuwa kutathmini sera za matumizi ya ardhi zilizopo na pia mfumo wa mpangilio katika viwango vya kitaifa na pia cha wilaya kupitia mfano wa wilaya ya Taita Taveta. Aligundua kuwa uwazi wa sera za matumizi ya ardhi Kenya ni dhaifu. kwa hivyo, mifumo ya uelekezi na mpangilio wake huwa changamano hasa kwa mwananchi wa kawaida. Kazi yake inahusiana na hii kwa sababu suala la ardhi lililochunguzwa katika utafiti huu ni pana ambapo sera za matumizi ya ardhi ni mojawapo. Tofauti na utafiti huu ni kwamba mtafiti amechunguza namna ambavyo waaandishi wa riwaya za *Kufa Kuzikana* na *Kovu Moyoni* walivyosawiri suala la ardhi.

Akichangia katika suala la ardhi nchini, Miguna (2012) alifafanua jinsi unyakuzi wa ardhi pamoja na mali nyingine ya umma ulivyofanywa nchini Kenya katika kipindi cha siasa za chama kimoja. Anatoa mfano wa unyakuzi wa msitu wa Mau na viongozi wa kisiasa na viongozi wakuu serikalini. Isitoshe, suala la ardhi pia lilibainika kuwa mojawapo ya matatizo sugu yanalolikabili bara la Afrika kwa jumla. Maelezo ya Miguna ni mojawapo ya msingi wa kazi hii kwa sababu mada hii ilichaguliwa kwa sababu ya kuwa suala la ardhi nchini ni nyeti na linaloibua taharuki na hisia tofauti miongoni mwa wanajamii. Hivyo, utafiti huu ulichunguza namna mizozo ya ardhi ilivyoangaziwa na waandishi wa riwaya teule na pia suluhisho lililotolewa.

Messah na Gachaba (2013) walichunguza mambo yanayosababisha tatizo la maskwota katika eneo la Bonde la Ufa nchini Kenya. Walitambua kuwa umiliki wa kibinafsi wa ardhi ndio sababu kuu ya kuwepo kwa maskwota nchini Kenya ambao ndio msingi wa sheria na sera za umiliki wa ardhi. Isitoshe, walitambua ya kwamba uuzaji wa mashamba ya familia na mkuu wa familia bila kushauriana na watu wengine katika familia pia husababisha hali ya kuwa maskwota nchini. Matokeo ya ripoti yao yanahusiana na kazi hii kwa misingi kuwa suala la maskwota lililochunguzwa ni mojawapo ya matatizo yanayotokana na mizozo ya ardhi ambayo pia yamechunguzwa katika utafiti huu. Hata hivyo, tofauti na utafiti huo, utafiti huu ni wa kifasihi ambapo riwaya mbili zimechambuliwa ili kubainisha namna waandishi Walibora katika *Kufa Kuzikana* na Habwe katika *Kovu Moyoni* walivyolisawiri suala la ardhi.

Chege (2013) aliangazia udhaifu wa sheria za ardhi zilizopo hivi sasa katika kushughulikia tatizo la ardhi la maskwota nchini Kenya. Alitambua ya kwamba kunao udhaifu katika sheria za ardhi katika kusuluhisha tatizo la ardhi la maskwota. Aidha, aligundua kuwa kuna udhaifu katika taasisi zinazoshughulikia masuala ya ardhi na hivyo kushindwa kutatua tatizo la ardhi la maskwota. Matokeo ya utafiti wake ni muhimu katika kazi hii kwa sababu inachunguza athari za mizozo ya ardhi na mikakati iliyowekwa ili kuyatatua. Hata hivyo, tofauti ni kwamba kazi hii ni ya kifasihi ambapo matokeo yalipatikana kwa kuchambua riwaya za *Kufa Kuzikana* na *Kovu Moyoni*.

Makunike (2014) alitafiti kuhusu uhusiano uliopo baina ya umiliki wa ardhi na umaskini katika eneo la Mashorland jimbo la mashariki mwa Zimbambwe. Utafiti wake uliongozwa na dhana kwamba katika Zimbambwe, walio maskini huishi sehemu za mashambani. Isitoshe, umaskini sehemu za mashambani ulihusishwa kwa kiwango fulani na ukosefu wa umiliki wa ardhi kutokana na ubaguzi wa kihistoria uliotokana na Wakoloni. Mojawapo ya mambo yaliyoshughulikiwa katika utafiti huu ni matatizo yanayokumba wanajamii yanayohusiana na suala la ardhi kama vile umaskini. Hata hivyo, utafiti huu umejikita katika riwaya za *Kovu Moyoni* na *Kufa Kuzikana* ili kuchunguza namna ambavyo suala hilo la mizozo ya ardhi limejitokeza.

Nyiri (2014) aliangazia athari za mizozo ya kikabila katika ukuaji wa uchumi na maendeleo nchini Kenya. Utafiti wake ulichanganua mizozo ya baada ya uchaguzi mkuu nchini Kenya iliyotokea kati ya Desemba mwaka wa 2007 na Februari mwaka wa 2008. Nyiri alitambua kuwa vita hivyo vilikuwa na athari kubwa kwa uchumi wa Kenya kuliko janga lingine lolote katika historia ya nchi ya Kenya. Aidha, mizozo hiyo itaendelea kuathiri nchi ya Kenya. Kwa hivyo, inabidi mifumo na sheria ziwekwe katika mataifa yaliyo na uwezekano wa kuwa na mizozo kama hiyo ili kuzuia uchumi wa taifa kuzorota. Utafiti wa Nyiri ni muhimu katika kazi hii kwa sababu umeeleza athari za mizozo ya kikabila ambayo chanzo chake ni suala la ardhi. Vilevile, imegunduliwa kuwa kuzorota kwa uchumi wa nchi ni mojawapo ya athari zake. Hata hivyo, utafiti huu umeangazia usawiri wa mizozo ya ardhi katika riwaya za *Kovu Moyoni* na *Kufa Kuzikana* ili kutathmini mitazamo ya waandishi hao kuhusu suluhisho la mizozo hiyo.

M`Ngaruthi (2015) alichunguza usawiri wa mwanasiasa wa Afrika katika Ushairi wa Kiswahili. Alitambua kuwa wahakiki wengine wa kisiasa wanakisia kuwa mataifa mengi ya Afrika yanatawaliwa kwa misingi ya kikabila. M`Ngaruthi anatoa mfano wa mgogoro wa kisiasa na kijamii uliozuka nchini Kenya baada ya uchaguzi wa mwaka 2007. Anaendelea kusema kuwa, mhakiki huyu anayasawiri matukio ya wakati huo kama shinikizo lililokuwemo kwa muda mrefu ambalo hatimaye lilisababisha mlipuko wa uhasama wa kikabila wa tangu jadi. Aidha, M`Ngaruthi anashikilia kuwa mgogoro huo haukusababishwa na uchaguzi wa mwaka 2007 bali wanasiasa walitumia uchaguzi huo kama kisingizio cha kueneza ajenda zao za kikabila. Maelezo haya yanahusiana na kazi hii kwa sababu miongoni mwa uhasama wa kikabila kama ilivyotambuliwa ni migogoro kuhusu mipaka ya mashamba. Utafiti huu umeangazia kwa kina masuala ya ardhi hasa michango ya viongozi na wanasiasa katika kusababisha uhasama wa kikabila unaohusiana na suala la ardhi. Kwa hivyo, utafiti huu umeziba pengo kwa kutoa suluhisho kwa migogoro ya kikabila hasa inayohusiana na ardhi.

### 2.5 Suluhisho la Mizozo ya Ardhi

Manji (2015) anatambua kwamba ardhi ni suala nyeti nchini Kenya. Aidha, anahoji kuwa kote Afrika Mashariki, mageuzi ya ardhi hayajaweza kukabili athari za ubaguzi katika umilikaji wa ardhi. Vilevile, anatambua kuwa tangu miaka ya tisini, sheria mpya za ardhi hazijaweza kusuluhisha kikamilifu malalamishi na dhuluma za kihistoria kuhusu ardhi. Maelezo haya yameufaa utafiti huu katika kueleza sababu za kuwepo na mizozo inayohusiana na suala la ardhi mara kwa mara katika sehemu nyingi barani Afrika, Kenya ikiwemo, jambo ambalo limeangaziwa na wasanii wa *Kufa Kuzikana* na *Kovu Moyoni,* riwaya ambazo zimeangazia mizozo nchini Kenya katika sehemu mbalimbali kuanzia miaka ya tisini.

Kuanzia miaka ya sabini, serikali ya Kenya iliunda tume mbalimbali kutatua matatizo ya ardhi nchini. Hizi ni pamoja na Tume ya Njonjo 1999 ya uchunguzi katika mfumo wa sheria za ardhi ya Kenya, Tume ya Akiwumi ya kukabiliana na vita vya kikabila, Tume ya Ndung`u iliyochunguza utoaji haramu wa ardhi ya umma na Tume ya Waki ambayo ilichunguza ghasia za kisiasa, 2008. Licha ya kuundwa kwa tume hizi, baadhi ya ripoti zake hazikuchukuliwa hatua na ndiposa kesi za ardhi zinaendelea kusababishia waathiriwa na nchi kwa jumla matatizo mengi. Hali hii inashadidia sababu za kuwepo kwa mizozo ya ardhi mara kwa mara. Maelezo hayo yameupa utafiti huu msingi

mwafaka katika kutathmini suluhisho la mizozo ya ardhi kwa kurejelea riwaya za *Kovu Moyoni* na *Kufa Kuzikana.*

Mworia (2009) alitafiti kuhusu mchango wa mwanasiasa wa Afrika katika uzukaji na uenezaji wa mizozo ya kikabila kwa kurejelea vurugu la muda mrefu katika mpaka wa jamii za Tigania na Tharaka nchini Kenya. Aligundua kwamba wanasiasa huchangia pakubwa katika uzukaji na uenezaji wa mizozo na chuki za kikabila. Mworia anatoa mfano wa vita vya kikabila kati ya Watigania na Watharaka katika mwaka 2007 ambapo viongozi wa kisiasa walitumia fursa ya kutoridhika miongoni mwa wanajamii hawa na kusababisha mizozo iliyotokana na masuala ya ardhi, mipaka ya wilaya na ukabila. Mworia pia aligundua kuwa masuala ya ardhi, mipaka ya wilaya na ukabila ndio yalitumiwa na viongozi kama msingi wa kusababisha mizozano katika jamii. Kazi hii imechunguza iwapo kunao uhusiano kati ya suala la ardhi na mizozano katika jamii kwa kurejelea riwaya teule. Vilevile utafiti huu umeangazia suluhisho la mizozo ya ardhi ambalo limetolewa na waandishi wa riwaya za *Kufa kuzikana* na *Kovu Moyoni.*

Kwa mujibu wa Leftie (2009), ili kusuluhisha na kurekebisha maonevu ya kihistoria kuhusiana na suala nyeti la ardhi, ni muhimu sera mpya ya kitaifa ya ardhi kukubaliwa. Vilevile anasema kuwa kukubaliwa kwa sera mpya ya ardhi na Bunge la Kenya ni njia mojawapo ya kutekeleza ajenda ya nne ya mkataba wa kitaifa ulioafikiwa mwaka wa 2008 kufuatia mizozano iliyotokea baada ya uchaguzi mkuu. Ripoti ya Leftie inahusiana na utafiti huu kwa kuwa umechunguza namna ya kusuluhisha mizozano katika jamii hasa inayohusiana na suala la ardhi. Utafiti huu vilevile umechunguza namna ambavyo suala hili la ardhi lilivyosawiriwa na waandishi wa riwaya za *Kufa Kuzikana* na *Kovu Moyoni.*

Mwathane (2010), alichunguza mchango wa masuala ya ardhi kwa mizozo nchini Kenya. Aidha, alijadili jinsi ambavyo kutoangaziwa kwa matatizo ya ardhi kulisababisha vita baada ya uchaguzi mkuu mwaka wa 2007 na vita vya kikabila miaka ya1992, 1997, na 2002. Katika ripoti yake anaeleza ya kwamba, iwapo nchi ya Kenya ilifaulu kupata katiba mpya, basi itawezesha Wakenya kupata majibu kamili kwa matatizo mengi ya ardhi. Matokeo yake ni kuifanya taasisi ya ardhi kuwa imara na hivyo kusuluhisha mizozo ya kisiasa ambayo kila mara uhusishwa na uchaguzi mkuu.

Utafiti wa Mwathane unahusiana na kazi hii kwa sababu utafiti huu umeangazia athari za mizozo ya ardhi katika jamii hasa kwa kurejelea riwaya teule. Hata hivyo, Mwathane alitathmini sera zilizowekwa katika miongo miwili iliyopita ikiwa pamoja na mabadiliko ya ardhi yaliyowekwa Februari 2008, mkataba wa makubaliano baina ya vinara wakuu baada ya uchaguzi mkuu na pia sura inayoeleza masuala ya ardhi katika katiba kielelezo. Tofauti na kazi yake, utafiti huu umetathmini riwaya za *Kufa Kuzikana* (Walibora, 2003) na *kovu moyoni* (Habwe, 2014) kama msingi wa utafiti.

Katika Katiba ya Kenya (2010), ardhi inachukua nafasi muhimu katika taifa. Sura ya Tano ya Katiba imeweka mwongozo wa jinsi masuala makuu yanayohusiana na ardhi yanavyopaswa kushughulikiwa katika nchi. Hizi ni pamoja na kuundwa kwa kanuni za sera za ardhi, uainishaji wa ardhi, kuundwa kwa tume ya kitaifa ya ardhi na udhibiti wa umiliki wa ardhi inayoshikiliwa na watu ambao si raia wa Kenya. Kwa msingi huu, utafiti huu umechunguza mtazamo wa waandishi wa riwaya teule za Kiswahili katika kusuluhisha suala la ardhi nchini Kenya.

Mworia na Ndiku (2012) walichunguza mizozo ya kikabila baina ya Watharaka na Watigania. Walichunguza sababu, athari na suluhisho kwa mizozo hiyo. Uchunguzi huo ulibaini kuwa kumekuwa na mzozo baina ya jamii hizo ambapo mipaka ya mashamba ni suala kuu lililosababisha mizozo katika maeneo hayo. Hii ni kwa sababu hakuna mipaka iliyo wazi baina ya wilaya mpya zilizoundwa. Kwa msingi huo, masuala yanayohusiana na ardhi ni muhimu katika kuelewa sababu za asili na maendeleo ya mizozo ya muda mrefu nchini Kenya. Aidha, uchunguzi huo ulinuia kutafuta suluhisho kwa mizozo ya ardhi baina ya Watharaka na Watigania.

Miongoni mwa mapendekezo ya kusuluhisha ni pamoja na Serikali kuu kuhusika katika utatuzi wa mizozo hiyo, viongozi wa serikali katika jamii hizo kuhusika na vilevile viongozi wa kidini. Kwa hivyo, utafiti huo ulitambua mchango mkubwa wa wanajamii na pia dini katika kusuluhisha mizozo ya ardhi. Utafiti wa Mworia na Ndiku unahusiana na huu kwa sababu umechunguza athari za mizozo ya ardhi na vilevile suluhisho lake. Hata hivyo, tofauti ni kwamba utafiti huu umeangazia mtazamo wa waandishi wa riwaya za *Kovu Moyoni* na *Kufa Kuzikana* kuhusu athari na suluhisho kwa mizozo ya ardhi.

Katika Ruwaza ya Maono ya 2030 ya Kenya, serikali inanuia kufanya marekebisho makubwa katika kilimo. Njia mojawapo itakuwa ni kuwawezesha watu wote kuwa na nafasi sawa ya kumiliki ardhi. Licha ya tafiti nyingi kuhusu suala la ardhi kufanywa na wasomi na pia wataalamu mbalimbali wa masuala ya ardhi, bado mizozo ya ardhi inaongezeka nchini Kenya kila uchao. Hii ndio maana utafiti huu unakusudia kutathmini mchango wa fasihi katika kuangazia masuala ya kijamii kama vile mizozo ya ardhi, kwa kuangazia mtazamo wa wasanii wa riwaya za *Kufa Kuzikana* na *Kovu Moyoni* kuhusu suluhisho kwa mizozo ya ardhi nchini.

Katika utafiti huu, mtafiti anatambua kuwa fasihi ni njia mojawapo ya kuangazia matatizo ya kijamii. Kazi mbalimbali za kifasihi zimeliangazia suala hili nyeti la ardhi na matatizo yake. Hata hivyo, wahakiki wa fasihi ya Kiswahili hawajajishughulisha kikamilifu katika kubainisha mchango wa fasihi ya Kiswahili hasa utanzu wa riwaya kama nyenzo mwafaka ya kutatua tatizo la ardhi nchini Kenya. Kwa msingi huo, utafiti huu unakusudia kuchunguza usawiri wa suala la ardhi katika riwaya teule za *Kufa Kuzikana* (Walibora, 2003) na *Kovu Moyoni* (Habwe, 2014).

**2.6 Suala la Ardhi Katika Fasihi**

Joseph na Lucinda (2001) wanaeleza kuwa sifa za Fasihi ya Amerika ni pamoja na kuangazia masuala ya historia ya Kusini, umuhimu wa familia, nadhari za kijamii na nafasi ya kila mtu katika jamii hiyo, nadhari za kuwepo na haki, masuala ya kidini katika eneo hilo na matatizo au manufaa yanayoletwa na dini, masuala ya ubaguzi wa rangi, suala la ardhi na manufaa yake na vilevile hisia za kitabaka. Isitoshe, wanasema kuwa mapinduzi ya Meksiko yalizua mikondo mipya ya wasanii wa fasihi ambapo wanatoa mfano wa riwaya ya *Los de Abajo* ya Mariano Azuela (1915). Wanaeleza kuwa tajriba yake ya kibinafsi pamoja na sababu zilizowachochea watu kufanya mapinduzi zimesawiriwa katika riwaya hiyo. Maelezo haya yanadhihirisha kwamba waandishi wa Fasihi ya Amerika waliangazia masuala ya ardhi kama mojawapo ya maudhui makuu, hivyo yana umuhimu katika utafiti huu. Hata hivyo, utafiti huu umepiga hatua kwa kueleza athari za mizozo ya ardhi na suluhisho lake kama linavyosawiriwa na wasanii wa *Kufa Kuzikana* na *Kovu Moyoni*.

Gonye na wenziwe (2012) wameangazia usawiri wa suala la ardhi nchini Zimbambwe katika fasihi za baada ya miaka ya elfu mbili. Wamechambua hadithi fupi nne

zilizoandikwa kwa Kingereza na riwaya moja ya Shona kwa lengo la kutathmini mtazamo wa wasanii wa kazi hizo za kifasihi kuhusu ukamilifu wa mageuzi ya ardhi nchini Zimbambwe. Vilevile, walichunguza jinsi ambavyo waandishi wa kubuni wa Zimbambwe hueleza suala la ardhi kwa ubunifu. Kazi hii imeufaa utafiti huu katika kueleza umuhimu wa fasihi katika kuangazia masuala ya kijamii mathalan suala la ardhi. Hata hivyo, inatofautiana kwa sababu utafiti huu umeangazia mchango wa riwaya za Kiswahili katika kushughulikia suala la ardhi kwa kurejelea riwaya za *Kufa Kuzikana* na *Kovu Moyoni*.

Chirere (2012) anadai kuwa ardhi ni suala kuu katika historia na fasihi ya Zimbambwe. Anaendelea kusema kuwa fasihi katika Zimbambwe iliyotungiwa Rhodesia inasawiri hali fulani za kimila baina ya wenyeji wa Zimbambwe na ardhi yao, aidha zinadhihirisha mahitaji makuu ya ardhi miongoni mwa watu. Anatoa mfano wa riwaya ya 'Waiting for The Rain' iliyoandikwa na Mungoshi (1975). Aidha, anamnukuu Maurice Vambe mwandishi na mhakiki wa fasihi huko Zimbambwe, ambaye ameshughulikia masuala ya fasihi ya Zimbambwe kuhusu ardhi katika 'Celebrating Land Resistance'. Anaeleza kuwa kuna haja ya waandishi kushughulikia suala la ardhi zaidi kwani ardhi katika Zimbambwe imetawala mielekeo ya kisiasa tangu wakati wa vita vya mapinduzi mnamo mwaka wa 1890. Vilevile, Chirere anasisitiza kuwa kuna haja ya waaandishi wa kubuni kuakisia masuala ya mageuzi ya ardhi yaliyopo.

Maelezo haya yameweka msingi katika utafiti huu ambapo umuhimu wa ardhi umeangaziwa sio tu nchini Kenya bali katika mataifa mengine ulimwenguni hasa Zimbambwe. Isitoshe, maelezo ya Chirere yanadhihirisha kuwa ardhi kama rasilimali muhimu huzua mizozo mingi katika jamii. Hivyo, anaona umuhimu wa fasihi katika kuliangazia suala hili nyeti. Hata hivyo, utafiti huu umeangazia namna ambavyo wasanii wa riwaya za Kiswahili nchini Kenya walivyosawiri suala la ardhi mfano wa *Kovu Moyoni* na *Kufa Kuzikana*.

Tugume (2013) alichunguza haki za kibinadamu zinavyodhihirishwa katika riwaya za Ngugi wa Thiong'o, Alex La Guma na Chinua Achebe. Aidha alitathmini namna ambavyo mzungu alikiuka haki za waafrika za umilikaji wa ardhi na utumwa katika riwaya za Ngugi na La Guma. Alitambua kuwa ubaguzi katika ugawaji wa ardhi hugeuza waafrika kuwa makabwela. Wao hushurutishwa kuwa watumwa katika

mashamba na viwanda vinavyomilikiwa na wazungu. Hivyo, ukosefu wa ardhi na hali duni za wafanyikazi huchochea ari ya uzalendo ambayo hatimaye hupevua vita vya ukombozi. Kazi ya Tugume inahusiana na utafiti huu kwa sababu inadhibitisha kuwa vita vya ukombozi ulimwenguni na hasa nchi nyingi barani Afrika vilichochewa na haja ya utwaaji wa ardhi kutoka kwa wakoloni. Hii ndio sababu mizozo ya ardhi ingali inaendelea katika jamii nyingi Afrika, Kenya ikiwemo. Hii ni kwa sababu bado suala hilo halijasuluhishwa hata baada ya wakoloni kuondoka na ndio maana wasanii mbalimbali wamezungumzia suala hilo. Kwa hivyo, utafiti huu umeziba pengo la namna ambavyo wasanii wa riwaya za Kiswahili nchini Kenya walivyoshughulikia suala la ardhi.

Masibo (2015) aliangazia uchanganuzi wa diskosi za ardhi katika kazi za fasihi: mtazamo wa waandishi wa Kenya kati ya 1980 na 2012. Aliangazia jinsi wasanii wa matini teule za fasihi walivyotumia diskosi za kifasihi yaani nyimbo na dansi, jazanda, taswira, kinaya, methali, virejeshi na diskosi ya kawaida ili kuonyesha matatizo yanayotokana na mikinzano ya ardhi. Aligundua kuwa wasanii walitumia diskosi za kawaida na vipengele mbalimbali vya lugha kama nyimbo na dansi, jazanda, taswira, kinaya, methali na virejeshi ili kufafanua suala la ardhi nchini kenya.

Kazi ya Masibo imeweka wazi mbinu mbalimbali ambazo hutumiwa na waandishi katika kazi zao kumulika masuala nyeti katika jamii pakiwemo suala la ardhi. Hata hivyo utafiti huu unatofautiana na kazi ya Masibo kwa sababu kando na kuchunguza namna ambavyo waandishi Walibora na Habwe wametumia fasihi kudhihirisha athari za mizozo ya ardhi, umechunguza mtazamo wao kuhusu suluhisho kwa mizozo ya ardhi kwa kurejelea riwaya za *Kufa Kuzikana* (Walibora, 2003) na *Kovu Moyoni* (Habwe, 2014). Zaidi ya hayo, utafiti huu umepiga hatua kwa kuchunguza uhusiano baina ya masuala ya kijamii na fasihi kwa kuzingatia mtazamo kwamba fasihi huakisi kikamilifu masuala ya jamii ilimoibuka, na ni nyenzo mwafaka inayoweza kutumiwa katika kutatua matatizo hayo.

### 2.7 Maandishi Kuhusu Kazi za Walibora na Habwe

Ochieng (2011) ametafiti kuhusu maigizo kama mbinu ya maudhui katika riwaya mbili za Ken Walibora. Riwaya zilizoangaziwa ni *Ndoto ya Amerika* (2001) na *Kufa Kuzikana* (2003). Utafiti wake uliongozwa na nadharia mseto za Uhalisia na Uigizaji

ambapo alibaini kuwa riwaya za Walibora zilizotafitiwa zina sifa za kitamthilia. Matokeo ya utafiti wake yamesaidia katika kuchambua na kuelewa riwaya ya *Kufa Kuzikana* ya Walibora. Tofauti na utafiti wake, kazi hii imechambua riwaya za waandishi tofauti, yaani *Kufa Kuzikana* (Walibora, 2003) na *Kovu Moyoni* (Habwe, 2014) ili kuchunguza namna ambavyo waandishi hao waliliangazia suala la ardhi.

Mayieka (2012) amechunguza masuala ibuka yanayosawiriwa katika riwaya za kisasa ambapo amehakiki riwaya za *Kidagaa Kimemwozea* (Walibora, 2012) na *Mhanga Nafsi Yangu* (2012) ya Mohamed S.A. Alilenga kubainisha jinsi riwaya ya kisasa inavyoangazia masuala ibuka katika jamii ya mwandishi. Vilevile alilenga kufafanua masuala ibuka ya kimataifa yalivyoshughulikiwa katika riwaya za kisasa na kufafanua athari ya masuala ibuka katika jamii ya kisasa. Kazi yake ina uhusiano na utafiti huu kwa sababu zaidi ya kuwa *Kidagaa Kimemwozea* ni riwaya ya Ken Walibora kama ilivyo ya *Kufa Kuzikana*, suala la ardhi ambalo ni msingi wa kazi hii pia ni miongoni mwa masuala yanayoibuka kila uchao katika jamii na hivyo utafiti huu umechunguza namna ambavyo waandishi wa riwaya za kisasa walilishughulikia suala hilo la ardhi, na pia suluhisho walilotoa kwa matatizo yanayohusiana na suala la ardhi. Tofauti ni kuwa uchunguzi huu umejikita katika usawiri wa suala la ardhi katika riwaya za *Kufa Kuzikana* (Walibora, 2003) na *Kovu Moyoni* (Habwe, 2014).

Wafula (2013) alichunguza nafsi neni na usawiri wake katika usimulizi wa maudhui ya migogoro ya kivizazi katika riwaya za Kiswahili za *Vuta n` kuvute* (Shafi, 1999*) kufa Kuzikana* (Walibora, 2003) *Kipimo cha Mizani* (Burhani, 2004) na *Tumaini* (2006) kati ya mwaka 1999 na 2009 kipindi kilichochukuliwa kuwa kilele cha utandawazi. Katika utafiti wake, alibaini kuwa migogoro ya kivizazi mbalimbali kama vile uhusiano wa kijinsia, ndoa, itikadi za kisiasa, maadili ya kitaaluma miongoni mwa nyingine hutokana na mifumo ya kiuchumi, kijamii na kisiasa katika jamii zinazoangaziwa. Utafiti wake umeifaa kazi hii hasa katika uchambuzi wa riwaya ya *Kufa Kuzikana* ili kubainisha namna ambavyo mifumo ya kijamii, kiuchumi na kisiasa huathiri masuala mbalimbali katika jamii suala la ardhi likiwemo. Tofauti na kazi hii ni kwamba imeangazia namna suala la ardhi limesawiriwa katika riwaya za *Kufa Kuzikana* na *Kovu Moyoni.*

Wafula (2015) alichunguza Mwingilianomatini katika *Cheche za Moto* (Habwe, 2008) na *Kidagaa Kimemwozea* (Walibora, 2012). Utafiti ulionyesha namna ambavyo tanzu na matini uhusiana na kutegemeana katika kuwasilisha ujumbe wa mwandishi. Aidha, alibaini kuwa riwaya ya Kiswahili imeendelea kukua na kudhihirisha matumizi ya tanzu na matini mbalimbali katika umbo lake. Kazi ya Wafula inahusiana na utafiti huu kwa sababu waandishi wa riwaya teule, Ken Walibora na John Habwe ndio pia waandishi wa riwaya za *Kufa Kuzikana* na *Kovu Moyoni* ambazo zimetumika katika kazi hii. Zaidi ya hayo, Wafula alibaini kuwa kazi za waandishi hawa wawili zilionyesha uhusiano mkubwa katika masuala mbalimbali waliyoshughulikia. Hata hivyo, unatofautiana kwa kuwa utafiti huu umejikita katika usawiri wa suala la ardhi katika riwaya teule.

Kihara (2016) aliangazia nafasi ya vijana katika riwaya za *Pendo la Karaha* na *Kovu Moyoni* za John Habwe. Kutokana na utafiti wake, alibaini kuwa John Habwe amefaulu vilivyo katika kuwasawiri vijana na nafasi hasi na chanya wanazochukua katika jamii iliyojaa adha ya ubinafsi, uchochole, udhalimu, utabaka, na unafiki miongoni mwa maovu mengine. Aidha, Habwe ametoa mchango wake muhimu katika kuwajenga vijana kihadhi. Utafiti wa Kihara umeifaa kazi hii pakubwa katika uchambuzi wa *Kovu Moyoni,* riwaya ya John Habwe ambayo imetumika katika kazi hii. Aidha, utafiti wa Simon umefaidi katika kupata ufahamu zaidi kuhusu mwelekeo wa uandishi na falsafa ya msanii John Habwe.

### 2.8 Misingi ya Kinadharia

Utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya Baadaukoloni. Kwa mujibu wa Childs na Williams (1997), Baadaukoloni ni dhana inayohusishwa na kazi za Cesaire (1950), Fanon (1961) Said (1978) na Bhabha (1994). Kazi za waandishi hawa zinajumuisha kipindi kilichofuata kile cha ukoloni baada ya zilizokuwa koloni za Uingereza kujipatia uhuru katika miaka ya hamsini na ya sitini. Childs na Williams (1997) wanaeleza kuwa mkoloni alihakikisha kuwa amemwathiri mwafrika kisiasa, kitamaduni na kiuchumi hali iliyosababisha kuibuka kwa tabaka jipya la waafrika walioanza kuwanyanyasa waafrika wenzao.

Maelezo haya yameufaa utafiti huu katika kueleza sababu za kuwepo kwa wananchi walio maskwota huku wengine wachache hasa viongozi wakimiliki vipande vikubwa vya ardhi. Hii inatokana na viongozi walioridhi mamlaka kutoka kwa wakoloni kutumia

sera za umiliki wa ardhi zilizotumiwa na wakoloni kwa manufaa yao wenyewe. Kwa hivyo, utafiti huu umeangazia suala la ardhi kama tatizo la kihistoria ambalo limekuwepo kwa muda mrefu na ambalo lingali linasababisha mizozo ya kila mara katika sehemu nyingi ulimwenguni na hasa nchini Kenya kwa kurejelea riwaya za *Kufa Kuzikana* na *Kovu Moyoni.*

Wamitila (2003), anaunga mkono maelezo ya Childs na Williams (1997) kwa kueleza kwamba Nadharia ya Baadaukoloni inahusishwa na mikabala ya mtazamo wa fasihi ya wasomi na wataalamu wa jamii zilizokuwa chini ya utawala wa kikoloni. Kwa mujibu wa Wamitila (2003), juhudi za kuanzisha mwelekeo mpya zilianza katika miaka ya hamsini katika juhudi za akina Aime Cesaire, Fidel Castro na Albert Memmi. Anaendelea kusema kuwa Moja kati ya kazi ambazo zimekuwa na athari kubwa katika ukuaji wa uhakiki wa ki-Baadaukoloni ni *The Wretched of the Earth* (Fanon, 1961). Hii ni kazi ambayo inayaibua na kuyaweka wazi masuala yanayohusiana na ubaguzi wa kimagharibi na jinsi ubaguzi huo unavyokuwa msingi mkubwa wa kuendelea kushikilia nguvu na kwa njia hiyo kuwalazimisha waliotawaliwa kutumia nguvu kujikomboa.

Kwa hivyo, Fanon anaeleza dhana ya `kupinga tamaduni` za watawala kwa watawaliwa ambapo anadai kuwa hatua ya kwanza ya watawaliwa katika kupata sauti pamoja na utambuzi wao ni kule kurudisha historia yao ya kale. Kulingana na Wamitila, uwezo wa kikoloni ambao umekuwepo kwa karne nyingi umeweza kushusha thamani ya kale ya mataifa yaliyotawaliwa; ambapo wakoloni wanayaona mataifa yaliyotawaliwa kuwa hayajapata ustaarabu. Kutokana na maelezo ya Wamitila, utafiti huu umeeleza sababu za kuwepo kwa mizozo ya ardhi mathalani nchini Kenya katika juhudi za kutafuta utambuzi na historia yao ya kale kuhusiana na umiliki wa ardhi iliyonyakuliwa na wakoloni na hatimaye viongozi walioridhi uongozi baada ya uhuru, kwa kurejelea namna mizozo hiyo ilivyoangaziwa na wasanii wa riwaya teule.

Said (1978) anachunguza jinsi nchi za kimagharibi zinavyoisawiri jamii ya ki-mashariki, picha ilizo nazo kuihusu na jinsi picha hizo potofu zinavyoathiri mahusiano yake. Kwa hivyo, Said anauzindua ulimwengu wa tatu ili usiendelee kudunishwa na utawala wa ulimwengu wa kwanza. Akimnukuu (Said, 1993), Wamitila anatambua kuwa ingawa nchi za Asia, Afrika na Amerika ya Kilatini zina uhuru wa kisiasa bado zinatawaliwa na kutegemea nchi za Kizungu. Hii ni kwa sababu viongozi walioshika

hatamu za utawala baada ya kuondoka kwa Wakoloni wakongwe waliendeleza uongozi wa kiimla na kuwanyanyasa wananchi wenzao. Bado kuna tamaa ambapo watu wanataka kujinufaisha kibinafsi na kuwabagua wenzao kwa misingi mbalimbali pakiwemo suala la umiliki wa ardhi.

Mawazo haya yameufaa utafiti huu hasa katika kuchunguza sababu za kuwepo kwa mizozo ya kila mara kuhusu ardhi nchini Kenya kwani viongozi walioridhi uongozi baada ya ukoloni waliendeleza sera za ardhi zilizoachwa na Wakoloni. Kwa hivyo, wachache hasa walio na ushawishi mkubwa serikalini wakarithi vipande vikubwa vya ardhi huku wengi wakisalia kuwa maskwota. Ndiposa Walibora na Habwe katika *Kufa Kuzikana* na *Kovu Moyoni* wameonyesha kuwa viongozi na watu wengine walio na ushawishi mkubwa serikalini huwachochea wananchi kwa misingi ya kikabila hali ambayo huzua mizozo ya ardhi huku wanaodhaniwa kuwa `wageni` wakifurushwa, jambo ambalo huchipuka mara kwa mara katika misimu ya upigaji kura.

Njogu na Chimerah (1999) wanadai kuwa mizozano mingi katika jamii zilizotawaliwa na Wakoloni ilitokana na hali ya uchumi ulioletwa na Mkoloni ambayo hutokana na utambulisho. Mawazo haya ni muhimu katika kueleza ni kwa nini walio na ardhi kubwa hujiona kuwa tofauti na walio na ndogo kwa sababu ya tofauti zao za kiuchumi. Hali hii hutokana na ugavi wa ardhi usio sawa na hivyo kusababisha mizozano. Aidha mawazo hayo yameufaidi utafiti huu katika kufafanua sababu za kuwepo kwa watu wanaonyakua mashamba kutokana na maskini kwa sababu wana uwezo mkubwa wa kiuchumi, hali inayosababisha maskini hao kusalia kufanya kazi kwa malipo duni katika mashamba yale yaliyonyakuliwa kutoka kwao, jambo ambalo limedhibitika katika riwaya za *Kovu Moyoni* na *Kufa Kuzikana*.

Kwa hivyo, msingi mkubwa wa mtazamo wa Nadharia ya Baadaukoloni ni juhudi za kuzirekebisha `picha` zilizo nazo nchi za kimagharibi kuhusiana na nchi nyingi zinazoelezwa kama `ulimwengu wa tatu`. Nchi nyingi za kimagharibi zimekuwa na mitazamo bezi ya nchi hizo pamoja na raia wake. Picha zao zimejitokeza katika maandishi yao, usemi wao na picha nyingi zinazosambazwa kuhusiana na mataifa hayo.

Kimsingi, Nadharia ya Baadaukoloni hujumuisha uhakiki wa kazi za fasihi kwa lengo la kuelewa uhusiano uliopo baina ya mataifa yaliyotawaliwa na yaliyotawala na jinsi

mkoloni alivyomwathiri mwafrika wakati na baada ya ukoloni. (Njogu na Chimerah, 1999). Kwa hivyo, Nadharia ya Baadaukoloni imetumiwa ili kufafanua jinsi wasanii wa riwaya za *Kovu Moyoni* na *Kufa Kuzikana* walivyodhihirisha athari ya ukoloni katika suala la ardhi nchini Kenya na vilevile kuonyesha msingi ambao jamii ya Kenya imejengeka kuhusu athari zinazotokana na umiliki wa ardhi.

Kutokana na mitazamo mbalimbali ya Nadharia ya Baadaukoloni, mihimili ifuatayo inajitokeza;

i) Maingiliano baina ya mtawala na mtawaliwa husababisha muungano wa kaida ya kitamaduni unaosababisha kuiga na kuivuruga tamaduni ya mtawaliwa na kuzaa utamaduni wa kiuhuluti.
ii) Hatua ya kwanza ya watawaliwa katika kupata sauti pamoja na utambuzi wao ni kule kurudia historia yao ya kale
iii) Harakati za kuupinga ukoloni ni hatua muhimu kwa sababu ukoloni ni mfumo wa kimawazo ambao upo na unaendelea hata kama ukoloni mkongwe uliondolewa.
iv) Mikinzano mingi katika jamii zilizotawaliwa na wakoloni ilitokana na hali ya uchumi ulioletwa na mkoloni.

Kutokana na mihimili iliyotajwa hapo juu, Nadharia ya Baadaukoloni imesaidia kuangazia zaidi suala la ardhi si tu kama mojawapo ya maudhui katika fasihi bali kama suala nyeti katika jamii halisi na mazingira halisi kiwakati na kihistoria. Zaidi ya hayo, imesaidia kuangazia suala la ardhi kwa kuchunguza athari za mkoloni katika suala hilo. Isitoshe, Nadharia ya Baadaukoloni imechangia katika utafiti huu kwa kuchunguza jinsi Wakenya waliorithi ardhi baada ya Ukoloni walivyohusiana na wale hawakuweza kuiridhi, hasa maskwota. Vilevile, imeufaa utafiti huu katika kutathmini sera kuhusu ardhi zilizotumiwa na waliochukua hatamu za uongozi baada ya ukoloni kwa kurejelea riwaya za *Kufa Kuzikana* na *Kovu Moyoni*.

### 2.9 Muhtasari wa Riwaya ya *Kovu Moyoni* (Habwe, 2014)

*Kovu Moyoni* ni hadithi inayosimulia matukio katika kijiji cha Siloko katika nchi huru ya Tandika. Inahusu mapambano ya mjane mmoja dhidi ya utawala dhalimu unaolinda na kulifadhili genge la wanamgambo la vijana wanaoshambulia na kupora kijiji cha Siloko kwa kisingizio cha kuondoa watu wasio wenyeji. Serikali ambayo Boke

anatarajia imlinde na mali yake inafeli katika jukumu lake la kimsingi na badala yake inalinda kundi lenye uwezo mkubwa la wanyakuzi wa ardhi na mibabe wa kivita.

### 2.10 Muhtasari wa Riwaya ya *Kufa Kuzikana* (Walibora, 2003)

*Kufa kuzikana* ni hadithi inayotokea katika nchi ya Kiwachema ambapo makabila mawili yanayozozana, Wakorosho na Wakanju wanaishi pamoja. Mhusika mkuu, Akida, mwanafunzi mwenye miaka kumi na mitano ni mkanju ilhali Tim, rafiki wake wa dhati ni Mkorosho. Ni hadithi ya migogoro, migongano, vikwazo na vizingiti katika uhusiano wao.

Vita vya kikabila vinapozuka baina ya Wakanju na Wakorosho, serikali inaamua kutotoa matangazo yoyote kuhusiana na mzozo huo. Hata hivyo, Wanaungana pamoja katika kujua hatima ya jamaa zao huko kijijini. *Kufa Kuzikana* ni riwaya inayodhihirisha kuwa ukabila ni virusi ambavyo vimewega wengi na kuwapokeza mengi yenye majuto, kite na kwikwi lakini licha ya hayo, muhimu ni ule moyo wa kusamehe, kupendana na kusonga mbele pamoja.

# SURA YA TATU
# MBINU ZA UTAFITI

## 3.0 Utangulizi

Sura hii imeangazia mbinu za utafiti zilizotumiwa katika utafiti huu. Imeeleza kuhusu mahali pa utafiti, utaratibu wa usampulishaji na kiwango cha sampuli, jinsi ya kukusanya data na namna ya kuchanganua data.

## 3.1 Eneo la Utafiti

Utafiti huu ulifanyiwa maktabani kwa kusoma na kuchanganua kwa kina riwaya teule za *Kufa Kuzikana* (Walibora, 2003) na *Kovu Moyoni* (Habwe, 2014). Isitoshe, vitabu mbalimbali vilisomwa ili kupata msingi na maelezo zaidi kuhusu Nadharia ya Baadaukoloni. Mtafiti alitumia maktaba mbalimbali za kitaifa na zile za vyuo vikuu kama vile Chuka, Nairobi, Moi na Kenyatta. Maktabani pia tasnifu za wasomi mbalimbali waliotumia Nadharia ya Baadaukoloni zilisomwa pamoja na vitabu na majarida yaliyohusiana na suala la utafiti huu.

## 3.2 Uteuzi wa Sampuli

Hata ingawa riwaya za Kiswahili ni nyingi, riwaya za *Kufa Kuzikana* (2003) na *Kovu Moyoni* (2014) ziliteuliwa kimakusudi. Sababu ya uteuzi huo ni kwamba zimeangazia suala la mizozo ya ardhi kama maudhui yake makuu. Kwa mfano, *Kovu Moyoni* ni riwaya iliyoangazia mzozo uliokuwepo katika eneo la Mlima Elgon eneo Kaunti ya Bungoma nchini Kenya mwaka 2005. Nayo riwaya ya *Kufa Kuzikana* imeangazia vita vya kikabila ambavyo asili yake ni ardhi vinavyotokana na uchochezi wa viongozi kama ilivyotendeka katika uliokuwa Mkoa wa Bonde la Ufa nchini Kenya mwaka 1992 baina ya Wakalenjin na Wakikuyu. Vilevile, uchambuzi wa riwaya teule umelenga kuchunguza namna ambavyo wasanii wa riwaya teule wametumia fasihi kudhihirisha mizozo ya ardhi, fani za lugha ambazo wasanii wametumia ili kudhihirisha athari za mizozo ya ardhi na pendekezo wanalotoa ili kusuluhisha matatizo ya suala la ardhi.

## 3.3 Njia za Kukusanya Data

Vitabu teule katika utafiti huu ni *Kufa Kuzikana* (Walibora, 2003) na *Kovu Moyoni* (Habwe, 2014) ambavyo vimesomwa kwa kina. Mambo ambayo yamechunguzwa ni namna waandishi walivyoangazia suala la ardhi katika riwaya teule. Data

iliyokusanywa ni maneno na vifungu vya maneno vilivyoonyesha mizozo ya ardhi kwa kuangazia matamshi ya wahusika na namna walivyoathirika, jinsi ambavyo fani za lugha zilidhihirisha athari za mizozo ya ardhi katika maneno na vifungu vya maneno na vilevile juhudi za wahusika za kusuluhisha matatizo ya ardhi kupitia vifungu hivyo katika riwaya teule.

### 3.4 Uchanganuzi wa Data

Data iliyopatikana kupitia kusoma riwaya za *Kufa Kuzikana* (2003) na *Kovu Moyoni* (2004) imechanganuliwa kwa njia ya maelezo kwa mujibu wa madhumuni ya utafiti. Uchanganuzi huo umeongozwa na Nadharia ya Baadaukoloni ili kueleza namna Walibora na Habwe walivyoafiki malengo yao ya kuangazia suala la ardhi kwa kubainisha namna walivyotumia fasihi kudhihirisha mizozo ya ardhi, jinsi walivyotumia fani za lugha kudhihirisha athari za mizozo ya ardhi na suluhisho wanazotoa kwa matatizo ya ardhi.

# SURA YA NNE

# JINSI MIZOZO YA ARDHI ILIVYOSAWIRIWA KATIKA RIWAYA ZA *KOVU MOYONI* NA *KUFA KUZIKANA*

## 4.0 Utangulizi

Madhumuni ya kwanza katika utafiti huu yalikuwa kubainisha usawiri wa mizozo ya ardhi katika riwaya za *Kovu Moyoni* (Habwe, 2014) na *Kufa Kuzikana* (Walibora, 2003). Usawiri wa mizozo ya ardhi umefafanuliwa kwa kuchunguza msimamo na mtazamo wa watunzi wa riwaya hizo kuhusu ardhi kwa kuzingatia chanzo cha mizozo ya ardhi, uhusiano uliopo baina ya mizozo ya ardhi na siasa, athari za mizozo hiyo, uhusiano uliopo baina ya mizozo ya ardhi na ukabila, na mchango wa serikali na viongozi wengine katika kusababisha mizozo ya ardhi.

## 4.1 Chanzo cha Mizozo ya Ardhi

Katika *Kovu Moyoni,* Habwe amebainisha chanzo cha mizozo ya ardhi kama inavyojitokeza katika kifungu kifuatacho:

> Vijana wengi walipiga uhuni na kushiriki katika ulevi na baadhi yao walifanya biashara ndogondogo za haramu. Vijana hao walikutana katika vikundi vidogo vidogo na wakaanzisha siasa fulani. Siasa za **kunyakua ardhi ambayo walidai kuwa ilikuwa ni yao na iligawanywa vibaya kwa kupitia kwenye misingi ghushi**. Wazo hili hatari lilichipuka kupitia miongoni mwa vijana wa Kisululu waliodhania kuwa ndilo kabila asilia la sehemu hiyo. (*Kovu Moyoni*, uk 15, msisitizo wangu)

Kwa mujibu wa kifungu hiki, mojawapo ya chanzo cha mizozo ya ardhi ni ugavi wa ardhi. Hii inabainika wakati kundi la `jeshi la vijana` kutoka katika kabila la Kisululu waliodhania kuwa ndilo kabila asilia la eneo la Rama liliundwa ili kutekeleza mashambulizi dhidi ya watu waliodhaniwa kuwa `wageni` katika eneo hilo. Walibora katika *Kufa Kuzikana* anaonyesha chanzo cha mizozo ya ardhi kwa kuandika:

> Nilimwonyesha baba karatasi ile akatua kitambo na kusema, "Mwanangu tangu mdogo nimevisikia vitisho hivi. Vishindo vya mashua havishtui bahari." Mzee Zablon, babake sahibu wanguTim, alikuja kwetu siku hiyo. Alikuwa ni mkorosho. Shamba lake lilipakana na letu. **Mara mbili tatu wamegombana na baba juu ya mpaka wa shamba.** lakini hawakuwa na uhasama mkubwa sana kati yao. (*Kufa Kuzikana*, uk 5-6, msisitizo wangu)

Kutokana na kifungu hiki, mizozo ya ardhi huzuka watu wanapozozana kuhusu mipaka ya mashamba. Jambo hili linadhihirika kupitia mhusika Akida anayeeleza kuwa baba yake na Mzee Zablon walizozana mara kwa mara kuhusu mipaka ya mashamba kwani yalipakana. Hata hivyo, Akida anaeleza kuwa licha ya kuzozania mipaka ya mashamba yao, hapakuwa na uhasama mkubwa sana kati ya baba yake na Mzee Zablon.

Kwa mujibu wa Nadharia ya Baadaukoloni, mizozano mingi katika jamii zilizotawaliwa na Wakoloni ilitokana na hali ya uchumi ulioletwa na Mkoloni. Hali hii hutokana na ugavi wa ardhi usio sawa na hivyo kusababisha mizozo. Kwa hivyo, inadhihirika kuwa mizozo ya ardhi huzuka mara kwa mara katika jamii kutokana na dhuluma za kihistoria kuhusu ugavi wa ardhi na pia mipaka ya mashamba, suala ambalo lilianza tangu jadi. Vilevile, inadhihirika kwamba sababu za kuwepo kwa mizozo ya mara kwa mara ni kwa sababu suala hilo la kihistoria halijaweza kusuluhishwa kikamilifu.

Licha ya kuwepo sheria za kitamaduni, haki za kumiliki ardhi za jamii hazijalindwa. Kwa hivyo, ili kuibuka na suluhu la kudumu kuhusiana na mizozo ya ardhi nchini Kenya, Serikali pamoja na mashirika mengine yanayohusika katika kushughulikia masuala ya ardhi yanapaswa kuwajibika. Isitoshe, kutambua ardhi ya jamii katika Katiba ndio msingi wa mageuzi ya sheria za kumiliki ardhi Kenya. Zaidi ya hayo, ni muhimu kutambua kuwa wakati umefika wa taasisi za ardhi kushirikiana na kufanikisha sheria za kumiliki ardhi. Sababu nyingine ya kuwepo kwa mizozo ya ardhi inajitokeza katika vifungu vifuatavyo:

> . . .wadadisi wa mambo wanasema, ingawa makabila hayo mawili yamekuwa na chuki baina yao**, huenda vita hivyo vimechochewa na watu wenye ushawishi mkubwa kisiasa.** Mapema wiki hii wahariri wakuu wa magazeti mawili nchini Kiwachema walitiwa nguvuni baada ya kuchapisha habari za vita hivyo. (*Kufa Kuzikana,* Uk 61, msisitizo wangu)
>
> Gurudumu la ukombozi lilikuwa limeanza kuteremka. Gurudumu lililokuwa hapo Lumbasa **lilitiwa grisi na mheshimiwa Mwamba**. Vijana waliozunguka barabarani bila kazi waliamini sasa watafaidika. (*Kovu Moyoni*, uk 54, msisitizo wangu)

Kutokana na nukuu hizi, mizozo ya ardhi hutokana na uchochezi wa viongozi wa kisiasa na pia watu wenye ushawishi mkubwa serikalini. Kwa mfano, Walibora katika *Kufa Kuzikana* anaeleza kuwa hata ingawa makabila ya Wakanju na Wakorosho yalikuwa na chuki baina yao, huenda mizozo iliyokuwa Wilayani Korosho ilichochewa na watu wenye ushawishi mkubwa kisiasa. Vilevile katika *Kovu Moyoni,* Habwe anadhihirisha kuwa chanzo cha mizozo ya ardhi

iliyoshuhudiwa Rama ilitokana na uchochezi wa mwanasiasa maarufu, Mwamba aliyechochea vijana kuunda `Jeshi la Vijana` lililotekeleza mashambulizi hayo.

Aidha, ukweli wa jambo hili unadhihirika kupitia matamshi haya:

> Mzee Zablon, babake sahibu wangu Tim, alikuja kwetu siku hiyo. Alikuwa Mkorosho. Shamba lake lilipakana na letu. Mara mbili tatu wamegombana na baba juu ya mpaka wa shamba, **lakini hawakuwa na uhasama mkubwa sana kati yao. Nakumbuka walivyoandamana pamoja kwenda kwenye madarasa ya ngumbaru, mikutano ya hadhara na hamkani nyingine.** "Ndugu yangu Sululu umeyasikia? Ilani imesambazwa kote Korosho kwamba Wakanju wahame." (*Kufa Kuzikana*, uk 5- 6, msisitizo wangu)

Dondoo la hapo juu linaonyesha kuwa, kabla ya mbegu ya chuki kwa misingi ya kikabila kupandwa katika jamii, watu wa kabila mbalimbali waliishi kwa amani na utangamano. Hii ndiyo maana Mzee Zablon na Sululu katika *Kufa Kuzikana* waliokuwa wa makabila tofauti wanatembeleana na kuandamana pamoja kwenda kwenye madarasa ya ngumbaru, mikutanao ya hadhara miongoni mwa shughuli zingine. Hali kadhalika, Habwe anadhihirisha kuwa kabla ya uchochezi watu wa makabila tofauti waliishi kwa Amani. Anaandika:

> …Boke alikumbuka walivyouza shamba lao la nyumbani ili kununua shamba la Rama. Walichokijia Rama ni kwamba walipapenda. **Watu walikuwa marafiki wakubwa. Ilikuwa nchi yenye rutuba**. Ardhi ilizaa mihogo, viazi na mahindi ya ajabu. Boke alikuwa hajawahi kuona ardhi ya aina hiyo maishani mwake. (*Kovu Moyoni*, uk 8, msisitizo wangu)

Inabainika kuwa kabla ya chuki kutokana na uchochezi watu waliishi kwa amani. Hii ndiyo maana Katika *Kovu Moyoni,* mhusika Boke anakumbuka jinsi yeye na mumewe mzee Kanja waliuza shamba lao la nyumbani ili kununua shamba la Rama kwa kuwa walipapenda na watu walikuwa marafiki wakubwa. Kwa mujibu wa Kimenyi na Ndung'u (2005), mizozo ya ardhi katika eneo la Bonde la Ufa mwaka 1992, 1997, 2002 na 2007 hadi 2008 ilichochewa na Wanasiasa nchini Kenya hasa wakati wa uchaguzi mkuu. Muchiri (2016) anaafikiana na madai hayo kwa kusema kuwa watu ambao wanapaswa kuwaongoza na kuwaelekeza Wakenya ndio hutumia matamshi ya uchochezi huku wakiwatumia vijana kueneza chuki dhidi ya wale wanaodhaniwa kuwa `wageni` miongoni mwao. Kwa hivyo, inadhibitika kuwa miongoni mwa vyanzo vya mizozo ya ardhi ni uchochezi wa watu wenye ushawishi mkubwa kisiasa.

Ardhi ni rasilimali muhimu kwa maendeleo ya jamii. Hutumika kuendeshea shughuli za kilimo, ujenzi wa makazi, ufugaji na shughuli nyinginezo. Kutokana na umuhimu wake, baadhi ya viongozi kwenye vitongoji na vijiji wamekuwa wakijigawia ardhi bila kuzingatia sheria, sera na

kanuni zilizopo za ugavi wa ardhi. Hali hiyo imekuwa ikichangia kuibuka kwa migogoro ya ardhi mara kwa mara katika maeneo mbalimbali nchini, ambapo mipaka ya ardhi na uchochezi wa wanasiasa kwa misingi ya kikabila ni miongoni mwa sababu zinazochangia kushamiri kwa migogoro hiyo. Kwa sababu hiyo, juhudi zinahitajika katika kukuza uelewa wa wanakijiji juu ya mifumo ya kisheria katika masuala ya haki za ardhi, uwezo wa uwekezaji mkubwa wa kilimo na uhusiano na ustawi wa wakulima wadogo, kilimo endelevu na maendeleo endelevu ya nchi kwa ujumla.

### 4.2 Mizozo ya Ardhi na Siasa

Katika riwaya za *Kovu Moyoni* na *Kufa Kuzikana*, wanasiasa, viongozi na wafanyibiashara mashuhuri wanalaumiwa kwa mizozo ya ardhi kama inavyojitokeza katika mifano ifuatayo:

> … msimu wa kura ulipofika, **wanasiasa walianza kugombana kwa ajili ya kura. Matokeo yake ni kuwa kulizuka machafuko si haba.** Emoro alifukuzwa katika kishamba chake alichokinunua kwa jasho lake lote. Emoro alitoka hapo Muhoroni kama mtu aliyeoga huku akiwa na nguo mwilini. Alikuwa wazimu si wazimu, nini si nini. ... (*Kovu Moyoni*, uk 4, msisitizo wangu)
>
> … siku moja mbunge wa kwetu Johnstone Mabende alihutubia Mkutano wa hadhara katika kituo cha biashara cha Baraki. Nakumbuka mpaka sasa alivyosema*; "***hatutaki `madoadoa`hapa. Wakanju sharti wahame warudi kwao Kanju."** mheshimiwa Mabende alishangiliwa kwa hoihoina nderemo na Wakorosho. (*Kufa Kuzikana,* uk 2, msisitizo wangu)

Kwa mujibu wa dondoo zilizonukuliwa, watunzi hawa wanadhihirisha kuwepo uhusiano wa moja kwa moja baina ya mizozo ya ardhi na siasa. Katika *Kovu Moyoni,* inadhihirika kuwa mizozo ya ardhi ilichacha kipindi cha Uchaguzi Mkuu baada ya wanasiasa kugombana. Mhusika Emoro anafukuzwa katika kishamba chake alichokinunua kwa jasho lake. Aidha, katika *Kufa Kuzikana,* mbunge Mabende alihutubia watu huko Baraki na kusema kuwa hawakutaka `madoadoa`. Aliwataka Wakanju wahame warudi kwao Kanju. Hii inaonyesha matumizi ya matamshi ya chuki na uchochezi kutokana na wanasiasa dhidi ya watu ambao hawakuwaunga mkono kisiasa kwa manufaa yao wenyewe. Nyiri (2014) anachangia suala hili kwa kusema kuwa mizozo ya baada ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2007 hadi 2008 ilikuwa imepangwa kabla ya uchaguzi huo na utekelezaji wake ulidhihirisha kuwa wanasiasa, wanabiashara mashuhuri, na viongozi wengine walikuwa chanzo cha ghasia hizo.

Kwa mujibu wa Nadharia ya Baadaukoloni, ingawa nchi za Asia, Afrika na Amerika ya Kilatini zina uhuru wa kisiasa bado zinatawaliwa na kutegemea nchi za kizungu. Hii

ni kwa sababu bado kuna tamaa miongoni mwa viongozi walioshika hatamu za uongozi baada ya kuondoka kwa Wakoloni. Hii ndio maana Wanasiasa na viongozi wengine walio na ushawishi mkubwa Serikalini huwachochea wananchi hasa nyakati za Uchaguzi Mkuu kwa misingi ya kikabila kwa manufaa yao binafsi. Hali hii husababisha mizozo ya ardhi nchini na hatimaye athari nyingi kwa wananchi. Waandishi wa riwaya *za Kovu Moyoni* na *Kufa Kuzikana* wanadhihirisha hali hii katika kazi zao ambapo wanasiasa na viongozi wakuu Serikalini wanachochea wananchi na hasa vijana ili kuzua vurugu nyakati za misimu ya upigaji kura. Matokeo yake ni mizozo mingi ambayo kiini chake ni suala la ardhi.

Kwa hivyo, inadhihirika kuwa wanasiasa huwa nguzo kuu katika mizozo ya ardhi hasa wakati wa kura dhidi ya wapinzani wao, na vilevile kupitia matamshi ya uchochezi katika kampeni wakati wa uchaguzi mkuu. Hivyo, ni wajibu wa viongozi wa kisiasa kuwa nyenzo ya kuhubiri amani miongoni mwa wananchi badala ya matamshi ya chuki kwa kutambua kuwa kuna maisha baada ya uchaguzi, na kwamba wananchi ni muhimu kuliko mtu binafsi. Katika *Kovu Moyoni,* mchango wa wanasiasa katika mizozo ya ardhi unadhihirika kutokana na maelezo haya:

> Tumejumuika hapa kuzungumzia masuala ya maendelao. Mimi ningependa mgombea kiti cha ubunge cha eneo bunge letu awe Msululu. **Jamii ya Sululu ndiyo inayostahili kugombea kiti hiki sio Kaisuku au haya Makabila mengine… ili kufanikisha wito huu tutabuni Jeshi letu la Vijana kuhakikisha kuwa siasa tutaidhibiti sisi wenyeji.** Ni kweli si kweli" (*Kovu Moyoni*, uk 53, msisistizo wangu)

Kwa mujibu wa dondoo hili, wanasiasa na viongozi wengine hutumia vijana wasio na kazi kuhubiri injili yao ya chuki kwa wageni na kusababisha mateso mengi kwa familia nyingi. Jambo hili linaendelezwa na mwanabiashara maarufu anayejulikana kama Mwamba anayeitisha mkutano ambapo anahubiri chuki kwa misingi ya kikabila. Isitoshe, anachochea vijana kuunda kundi linalojulikana kama 'Jeshi la Vijana' ambalo linatekeleza mashambulizi huku likiwafurusha wanaodhaniwa kuwa `wageni` hapo Rama.

Katika *Kufa Kuzikana*, mchango wa wanasiasa unajitokeza kupitia kifungu kifuatacho:

> . . .wadadisi wa mambo wanasema, ingawa makabila hayo mawili yamekuwa na chuki baina yao, **huenda vita hivyo vimechochewa na watu wenye ushawishi mkubwa kisiasa**. Mapema wiki hii wahariri wakuu wa magazeti mawili nchini Kiwachema walitiwa nguvuni baada ya kuchapisha habari za vita hivyo. (*Kufa Kuzikana*, Uk 61, msisitizo wangu)

Kifungu kilichonukuliwa kinadokeza kuwa vita vilivyoshuhudiwa wilayani Korosho vilihusishwa na watu wenye ushawishi mkubwa kisiasa kama vile mbunge Mabende. licha ya wasanii wa *Kovu Moyoni* na *Kufa Kuzikana* kueleza kwa namna tofauti, inadhihirika kuwa wanasiasa na viongozi wengine walio na ushawishi mkubwa serikalini ndio uhusishwa na mizozo mingi ya ardhi ambapo huwatumia vijana kuendeleza hazima yao ya kisiasa. Kulingana na M`Ngaruthi (2015), mgogoro wa kikabila uliokuwepo nchini Kenya baada ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2007 hadi 2008 haukusababishwa na uchaguzi mkuu bali wanasiasa waliutumia kama kisingizio cha kueneza ajenda zao za kikabila.

Kwa hivyo waandishi wa riwaya teule wanadhihirisha kuwa wanasiasa huwa mhimili mkuu katika kusababisha mizozo ya ardhi. Hivyo, ni muhimu kamati ya bunge inayosimamia masuala ya ardhi isaidie ili ibainike wazi ikiwa kuna mtu au kundi la watu wenye ushawishi mkubwa wanaojitahidi kuvuruga usimamizi bora wa masuala ya ardhi ili wapate kujinufaisha wenyewe kibinafsi. Isitoshe, mchango wa wanasiasa katika mizozo ya ardhi unajitokeza katika dondoo hii:

> Ndori alijaribu kuelewa mambo aliyokuwa ameanza kuyasikia kuhusu vijana wa huko kwao nyumbani. Alikumbuka kweli kulikuwa na **makundi ya vijana waliokosa karo ya kuwasomesha. Vijana waliolewa kila uchao na ambao mtu yeyote mwenye ubaya angewatumia kwa visa vya ugaidi.** Jioni moja ndipo aliposikia kuwa baba yake pia alikuwa ameuawa katika mashambulizi hayo. (*Kovu Moyoni*, uk 67, msisitizo wangu)

Riwaya ya *Kovu Moyoni* inadokeza kuwa vijana waliokosa karo ya kusoma walitumiwa na wanasiasa kutekeleza visa vya ugaidi kama vile kuanzisha mizozo katika jamii. Mhusika Ndori anakumbuka kuwa vijana wa huko kwao nyumbani waliokosa karo ya shule hawakuwa na jingine la kufanya ila kulewa kila uchao na kutumiwa kutekeleza visa vya ugaidi. Hii inaonyesha kuwa umaskini katika jamii unaweza kusababisha kila aina ya mizozo ya ardhi. Serikali ya Kenya ilipoanzisha elimu ya msingi bila malipo mwaka 2003, idadi kubwa ya wanafunzi waliingia katika mfumo wa elimu. Kwa hivyo wanafunzi wenye uwezo mkubwa kimasomo kutoka familia maskini wakawa na nafasi ya kuendelea na masomo. Hali hiyo inaweza kuchangia katika maendeleo ya uchumi wa nchi, kupunguza umaskini na kupunguza visa vya ugaidi kama vile mizozo ya ardhi katika jamii. Riwaya ya Kovu *Moyoni* inafumbata hali hii ifuatavyo:

> … vijana wengine kama vile Sang, walizurura na kulimia watu mashamba. Mikutano ya kisiasa ilipokuja ni **wao waliotumiwa kufanya fujo hiyo yote…. Walikuwa hazina kubwa ya wanasiasa.** Mwanasiasa alipokuwa akitaka vijana wa kuvuruga mkutano walikuwepo tayari kunadiwa kwa pesa kidogo na ulevi kidogo. (*Kovu Moyoni*, uk 70, msisitizo wangu)

Mtunzi wa *Kovu Moyoni* amewasawiri vijana kuwa hazina kubwa ya wanasiasa. Walitumika katika kusababisha kila aina ya fujo. Aidha, inadhihirika kuwa vijana waliotumiwa na wanasiasa ni wale ambao hawakuwa na kazi, ndiposa mhusika Mali ya Mungu anawazia vijana wa Rama waliotembea miji kama Mikindani, Lumbasa, wakiwa wamevaa nguo zilizoraruka, wakivuta sigara na bangi. Baadhi yao waliingilia pombe haramu ikawaharibu kupindukia huku wengine wakisombea watu mizigo ya kila aina na wengine kulimia watu mashamba. Licha ya kuibia watu, walinadiwa kwa pesa na ulevi kidogo ili wafanye fujo katika misimu ya upigaji kura.

Kwa hivyo, waandishi wa riwaya za *Kovu Moyoni* na *Kufa Kuzikana* wanatoa changamoto kwa wanasiasa ambao huwatumia vijana ili kutekeleza hazma yao ya kisiasa, aidha anaweka wazi udhaifu wa mfumo wote wa utawala ambapo serikali ya nchi imeshindwa kushughulikia maslahi ya vijana hasa katika kuongeza nafasi za kazi na kupunguza gharama ya elimu. Kwa mujibu wa takwimu za Umoja wa Mataifa, watu milioni 200 miongoni mwa wakazi wa Afrika ni vijana wenye umri kati ya miaka 15 na 24. Hii ni katika hali ambayo Umoja wa Mataifa unasema kuwa, idadi ya vijana wasio na ajira barani Afrika ni mara mbili zaidi ya watu wazima. Aidha, ukosefu wa ajira miongoni mwa vijana unawafanya washawishike kujiunga na makundi yenye misimamo mikali. Inaonekana kuwa, vijana wasio na ajira ni mawindo mazuri kwa makundi yenye kufurutu ada na yanawashawishi kujiunga nao kwa kiasi kidogo tu cha fedha. Mfano wa hali hiyo ilishuhudiwa katika nchi za jamhuri ya kidemokrasia ya Kongo, Nigeria na Mali. Athari za kukosa kazi kwa vijana ni hali inayoshuhudiwa hivi sasa barani Afrika pakiwemo mizozo ya ardhi. Kwa hivyo, vijana wanapaswa kusaidiwa sambamba na kubadilisha hali ya sasa, ili kuandaliwe mustakabali mzuri zaidi katika bara hilo, Kenya ikiwemo, suala linalopaswa kupewa kipaumbele na serikali za nchi za kiafrika.

Isitoshe, wasanii wa riwaya teule wanasawiri mizozo ya ardhi kama ifuatavyo:

> … Meja-K alielezwa na Mustafa kuwa **mheshimiwa Mwamba alikuwa ametuma malori sita ya silaha. Alifafanua kuwa silaha hizi zilikuwa za kisasa.** Pia alikuwa mara hii amekumbuka kuleta vifaa vya mawasiliano. Vifaa hivi vilisaidia katika kurahisisha mtandao wa mawasiliano katika Jeshi la vijana… (*Kovu Moyoni*, Uk 26, msisitizo wangu)

Katika *Kovu Moyoni*, inadhihirika kuwa viongozi wa kisiasa, hufadhili mizozo ya ardhi kwa njia mbalimbali. Kwa mfano, mheshimiwa Mwamba anafadhili Jeshi la Vijana kwa kuwatumia malori sita yaliyosheheni silaha za kisasa. Vilevile anawatumia vifaa vya mawasiliano, Ili kurahisisha mawasiliano yao hasa wakati wa kutekeleza mashambulizi.

Katika *Kufa Kuzikana*, Walibora anasema:

> …mbunge mheshimiwa Johnstone Mabende, wakereketwa wake na viongozi wa kidini Wakorosho na wasiokuwa Wakorosho *walikuwa* **watuhumiwa wakubwa katika mauaji hayo ya halaiki kioja kilioje kubaini kwamba makasisi waliokuwa wakikaa mbali mijini na majijini kama vile Kasisi John Njalala wakifadhili kisiri mapigano korosho**. Serikali iliyafumbia macho mauaji hayo kwa vile maafisa wa ngazi za juu serikalini walihusika. (*Kufa Kuzikana*, uk 160, msisitizo wangu)

Katika *Kufa Kuzikana*, mbunge Mabende, wakereketwa wake pamoja na viongozi wa kidini wanatuhumiwa kushiriki katika mauaji wilayani Korosho. Kadhalika, makasisi kama vile Kasisi John Njalala alifadhili kisiri mapigano Korosho. Kutokana na vifungu vilivyodondolewa hapo juu, wasanii wa riwaya teule wamedhihirisha wazi kuwa watu walio na ushawishi mkubwa serikalini huwa na mchango mkubwa katika kuzua vita vya kikabila. Katika *Kovu Moyoni,* Habwe anamwangazia mwanasiasa maarufu Mwamba ambaye kwa usaidizi wa walinda usalama waliostaafu wanaaanzisha 'Jeshi la Vijana' kulazimisha wale ambao si wenyeji wa Rama kuondoka.

Aidha, anawasaidia kwa pesa, silaha na ala za mawasiliano ili kufanikisha matembezi na pingamizi kutoka kwa watu. Katika *Kufa Kuzikana,* mchango wa wanasiasa unadhihirika kupitia idhaa ya Kiswahili ya BBC ambapo inaripotiwa kuwa ingawa makabila ya Wakorosho na Wakanju yalikuwa na chuki baina yao, huenda vita vya kikabila Wilayani Korosho vilichochewa na watu wenye ushawishi mkubwa kisiasa. Zaidi ya hayo, viongozi wa kidini pia wanaonekana kufadhili mizozo ya ardhi kwa kushirikiana na wanasiasa hao.

Akichangia katika suala hili, Wachira (2014) anarejelea makabiliano baina ya jamii za Bonde la Suguta nchini Kenya ambapo anatambua kuwa watu wenye ushawishi mkubwa kutoka jamii hizo walizidisha hali kwa kufadhili wizi wa mifugo ambayo baadaye inauzwa katika maeneo mengine ya nchi kwa ajili ya nyama. Aidha, watu ambao baadhi yao wana nyadhifa za juu katika idara za usalama na kisiasa, wanashirikiana na wazee wa vijiji, viongozi wa kidini, maafisa wa utawala wa mikoa na polisi wanaofanya kazi katika maeneo hayo. Hivyo, watu walio na ushawishi ndio hununulia wapiganaji wa jamii zao silaha hasa kwa lengo la kuwawezesha kuiba mifugo. Ripoti ya Wachira (2014) imewalaumu wanasiasa kwa kupepeta moto wa kuzorota kwa usalama eneo hili kwa kutumia propaganda wakiwa na lengo la kushinda uchaguzi. Aidha, inatoa mfano wa mizozo iliyoongezeka katika eneo hilo mnamo 2012 katika kaunti ya Baringo kati ya jamii za Pokot na Tugen, ambapo wanasiasa walichochea mizozo kwa ajili ya uchaguzi wa 2013.

Ili kukabiliana na mizozo ya aina hii, ni muhimu kamati za amani mashinani kufanya kazi kwa kushirikiana na mashirika ya `Non-governmental organization`(NGO) na ya kijamii, ili iweze kutatuliwa kabla haijageuka kuwa makabiliano yanayopelekea mauti, uharibifu wa mali na majeruhi. Zaidi ya hayo, kamati hizo zinaweza kuhimiza mashauriano baina ya jamii za maeneo hayo pamoja na kufahamu kinachozua mizozo ili kukishughulikia. Kadhalika, ni muhimu kuanzishwa kwa miradi ya maendeleo kama vile barabara, shule na hospitali ili kuhakikisha wakazi hasa vijana wana mbinu mbadala za kujikimu kimaisha.

### 4.3 Mizozo ya Ardhi na Ukabila

Watunzi wa riwaya za *Kovu Moyoni* na *Kufa Kuzikana* wanashadidia kauli hii kwa kuonyesha kuwa kuna uhusiano wa karibu baina ya mizozo ya ardhi na ukabila. Kwa mfano:

> … Jamii ya Sululu ndiyo inayostahili kugombea kiti cha ubunge sio makabila haya mengine…pia tungependa kuhakikisha tumepata sehemu yetu ya halali ya mashamba. **Jeshi litahakikisha kuwa watu wasio wenyeji na waliopata mashamba yetu kiharamu wameng`olewa**. Au mnataka wakae nasi tukitaabika? (*Kovu Moyoni*, Uk 53, msisitizo wangu)
>
> Nyie Wakorosho na sisi Wakanju ni ndugu, Meno ya mbwa hayaumani…**sisi Wakorosho tumekuwa tukifanya shinikizo nyie Wakanju mtoke Wilaya ya Korosho…tangu mdogo nikisikia**, Wakanju ni walowezi Watimuliwe warudi kwao (*Kufa Kuzikana*, Uk 29, msisitizo wangu)

Dondoo hizi zinaonyesha kuwa tofauti za kikabila huzua mizozo ya ardhi. Katika *Kovu Moyoni*, Habwe anamwangazia mhusika Mwamba ambaye anawachochea vijana wasio na kazi kwa misingi ya kikabila ili waunde kikundi cha 'Jeshi la vijana'. Vilevile, anawaeleza kuwa wanapaswa kuhakikisha ya kwamba watu wote ambao si wenyeji na waliopata mashamba kiharamu wameng`olewa. Kwa upande mwingine, katika *Kufa Kuzikana,* Walibora anamtumia mhusika Tim ambaye ni rafiki wa kufa na kuzikana wa Akida licha ya kuwa wao ni wa makabila tofauti tofauti. Vita vya kikabila vinapozuka wilayani Korosho, wanahofia kwamba mambo huenda yakawa mabaya zaidi, ndiposa Tim anamwambia Akida kuwa wao Wakorosho wamekuwa wakifanya shinikizo Wakanju watoke wilaya ya Korosho, mambo ambayo amekuwa akiyasikia tangu akiwa mdogo. Kwa mujibu wa Chachali (2008), tofauti za kikabila na kidini ni miongoni mwa vyanzo vikubwa vya machafuko sehemu mbalimbali duniani hususan barani Afrika. Anaendelea kusema kuwa tofauti hizo hustawi vizuri zaidi mahala ambapo kuna manung`uniko kuhusu haki na usawa hasa katika uchumi.

Ghasia za baada ya uchaguzi mkuu nchini Kenya mwaka 2007-2008 zilidhihirisha kuwa ukabila unaweza kuitumbukiza nchi katika vita. Changamoto kubwa kwa demokrasia barani Afrika si fahari ya kuwa na makabila mengi, bali ni kutumia makabila hayo kuendeleza siasa za ubinafsi ambazo zinachochea ukabila. Masuala kuhusu kawi, uchukuzi, kilimo na mawasiliano na ajira kwa vijana yanaibuka kama kauli mbiu katika siasa za Afrika licha ya tofauti za kimawazo. Kwa kuwa demokrasia inatoa nafasi kwa maendeleo na mafanikio, siasa za kikabila lazima zikomeshwe na taasisi za kisasa zenye kushinikiza demokrasia ziimarishwe. La sivyo, bara la Afrika, litaendelea kutumbukia katika athari za siasa za ukabila.

### 4.4 Mchango wa Serikali katika Mizozo ya Ardhi

Riwaya za *Kovu Moyoni* na *Kufa Kuzikana* zinasawiri serikali ya nchi kuwa na mchango mkubwa katika kuzidisha mizozo ya ardhi. Waathiriwa wa mizozo ya ardhi hujihisi kusalitiwa na serikali na huhofia kwamba hawana mtu yeyote wa kulinda maslahi yao. Taswira hii inadhihirika katika dondoo zifuatazo:

> …Boke aliganda pale kitini kama jiwe. Alikumbuka usiku ule yule mwanamume **aliyefaa kumlinda na madaraka yake yote yale alivyomnajisi na hata kumsababishia kuvuja damu. Lakini atafanyaje***?* Yuko bado kazini. Boke aliangua kilio mle ofisini. *"*Usililie hapa, mama. Tena usilete hapa mambo ya uongo," Bwana Mkubwa alisema. (*Kovu Moyoni*, Uk 147, msisitizo wangu)

> …nyumba zetu zinateketezwa na Wakorosho **ilhali askari wa polisi wanatazama tu, bunduki mkononi, hauwapigi mshipa.** Wanawake na mabinti zetu wanabakwa dhahiri shahiri na polisi Wanavifumbia macho vitendo hivyo. Wanajali nini? Wanaona sisi Wakanju si binadamu, si chochote si lolote. Tunauliwa tuputupu." (*Kufa Kuzikana*, Uk 75, msisitizo wangu)

Watunzi wa riwaya hizi wameyarejelea matukio ambayo yanadhihirisha kuwa serikali ya nchi haijawajibika kikamilifu katika kutatua mizozo ya ardhi inayotokana na tofauti za kikabila, bali inachangia katika kuiendeleza. Hali hii inadhihirika katika riwaya teule ingawa kila mwandishi anaeleza hali hii kwa mtazamo wake. Kwa mfano, katika *Kovu Moyoni* Habwe anamtumia mhusika Boke ambaye ni mwathiriwa wa mizozo ya ardhi. Boke anakumbuka tukio la usiku mmoja alipobakwa na Inspekta Onyango, polisi aliyefaa kumlinda na badala yake alichangia katika kumsababishia madhara mengi. Kwa sababu hiyo, Boke anaamua kwenda kumwona mkuu wa kituo cha polisi cha Sabasaba ili kuripoti kisa hicho. Katika *Kufa Kuzikana*, Walibora anamtumia Mzee Uledi ambaye anaeleza hali ilivyokuwa Wilayani Korosho baada ya vita vya kikabila. Anaeleza jinsi nyumba zao ziliteketezwa na wanawake kubakwa ilhali askari wa polisi walitazama tu bila kuchukua hatua yoyote.

Baada ya mashambulizi yaliyofanywa na kikundi cha Sabaot Land Defence Forces (SLDF) katika eneo la Mlima Elgon, Gagnon (2008) anaonya kuwa wanajeshi wa taifa waliwadhulumu watu ambao walipaswa kuwalinda. Kwa hivyo, serikali ya taifa inasawiriwa kuwa na mchango mkubwa katika mizozo ya ardhi hasa kupitia askari wasiowajali wananchi na waathiriwa wa mizozo hiyo. Hiki ni kinaya kwa sababu askari ndio wanaotarajiwa kuwalinda raia. Badala yake, wanawadhulumu na kuwatendea unyama. Isitoshe, mwitikio wa serikali ya nchi kuhusu mizozo ya ardhi unajitokeza kuwa duni kama inavyodhihirika wakati vyombo vya habari vinavyozuiliwa kufanya uchunguzi mizozo inapotokea. Kwa mfano:

> **Serikali ya Kiwachema imepiga marufuku wageni na waandishi wa habari kuzuru eneo la mapigano.** Wadadisi wa mambo wanasema, ingawa makabila hayo mawili yamekuwa na chuki baina yao, huenda vita hivyo vimechochewa na watu wenye ushawishi mkubwa kisiasa. Mapema wiki hii **wahariri wakuu wa magazeti mawili nchini Kiwachema walitiwa nguvuni baada ya kuchapisha habari za vita hivyo. Matoleo ya Jumatano ya magazeti nchini humo yalinaswa yote na polisi**. "Haya," alitamka Tim baada ya habari hizo kwisha. "usipozisikia unaumia, ukizisikia unaumia, yote fahuwa." (*Kufa Kuzikana*, uk 61, msisitizo wangu)

Walibora anasimulia kisa ambapo Serikali ya Kiwachema inapiga marufuku wageni na waandishi wa habari; wa nje na wa ndani pia, kuzuru eneo la mapigano baada ya vita baina ya makabila ya Wakorosho na Wakanju. Inatangazwa kuwa wahariri wakuu wa magazeti mawili nchini Kiwachema walitiwa nguvuni baada ya kuchapisha habari za vita hivyo. Hali kama hiyo ilijitokeza nchini Kenya wakati mhariri wa chapisho la wiki `*The People*`, bwana Bedan Mbugua alikamatwa alipokuwa akifanya uchunguzi kuhusu mizozo ya Molo siku chache baada ya Rais Moi kutangaza `operesheni ya usalama` katika Molo, eneo la Burnt Forest na Londiani Septemba, 2, 1993 (Nyukuri, 1997). Kwa hivyo, waandishi wa riwaya teule wanaweka wazi udhaifu wa Serikali katika kushughulikia mizozo ya ardhi nchini ili jambo hilo liweze kutazamwa upya na kwa umakini. Serikali ya nchi pia inapaswa kuwajibika ili kuwashughulikia waathiriwa wa mizozo ya ardhi kama vile wakimbizi wa ndani wanaopata shida nyingi katika kambi mbalimbali za wakimbizi.

### 4.5 Athari za Mizozo ya Ardhi

Waandishi wa riwaya za *Kovu Moyoni* na *Kufa Kuzikana* wamesawiri mizozo ya ardhi kama iliyosababisha madhara mengi. Miongoni mwa athari za mizozo ya ardhi ni pamoja na mauaji, ukimbizi, ubakaji, visasi kuzorota kwa uchumi na usalama, kukatizwa kwa masomo, umaskini na kuibuka kwa vikundi haramu.

### 4.5.1 Mauaji

Mauaji mengi yalitekelezwa wakati wa mizozo ya ardhi kupitia njia mbalimbali kama vile kuchomwa, kuchinjwa kwa kutumia silaha mbalimbali, kuzikwa wakiwa wangali hai na pia kupigwa risasi. Baadhi ya namna ambavyo mauaji yalitekelezwa yanadhihirika katika vifungu vifuatavyo:

> Hapo Boke aliposimama alikumbuka mashambulizi yaliyohusu mashamba yaliyotokea katika miaka ya nyumahapo Rama. Mashambulizi hayo yalisababisha kuunguzwa kwa sehemu nzima ya Rama huku wageni wakifukuzwa kama swara. Alikumbuka jinsi jirani yake, Emoro, alivyofukuzwa akaingia ndani ya shamba la miwa. **Watesi wake walimfuata na kumchomea humo shambani.** Hadi hivi leo, Boke hukumbuka sauti ya Emoro ikiomba msaada wa kuokolewa. (*Kovu Moyoni*, uk 2, msisitizo wangu)

> … Boke aliona maiti za watu wengi. Kuna wale **waliopigwa risasi**. Kuna wale **waliokanyagwa na wenzao** wakati wakitoroka. Kulikuwepo na ajuza aliyeshindwa na harakati za kukimbia. Alianguka jiweni. Mungu akampumzisha na kero la maisha. (*Kovu Moyoni*, uk 10, msisitizo wangu)

> … mwandishi wa BBC aliyeko Tandika, jiji kuu la Kiwachema, amearifu kuwa watu **takriban themanini wameuawa** na mia tatu wakajeruhiwa, wengine wao vibaya sana, katika vita baina ya makabila ya Wakorosho na Wakanju vilivyoanza siku chache zilizopita. Serikali ya Kiwachema imepiga marufuku wageni na waandishi wa habari. (*Kufa Kuzikana*, uk 61, msisitizo wangu)

Waandishi wa riwaya teule wamerejelea matukio ambapo vifo vingi vilishuhudiwa. Katika *Kovu Moyoni*, mhusika Boke anakumbuka jinsi ambavyo jirani yake Emoro aliuawa kwa kuchomewa shambani huku akisingiziwa kuwa` mgeni` hapo Rama. Vilevile amerejelea tukio lingine baada ya mashambulizi ambapo Boke alishuhudia maiti za watu wengi alipokuwa akikimbilia usalama. Walibora katika *Kufa Kuzikana* anadhihirisha kuwa mauaji mengi yalitekelezwa katika vita baina ya makabila ya Wakorosho na Wakanju kupitia vyombo vya habari hasa idhaa ya BBC ambayo ilitangaza hali ilivyokuwa Wilayani Korosho.

Vilevile, mauaji ya halaiki inajitokeza katika *Kovu Moyoni* kupitia mfano ufuatao:

> Tokea **siku aliyouawa Chifu Ngata ni kama kibiriti cha mauaji na ubakaji kiliwashwa tena Rama**. *Watu waliuawa* na jinamizi la ubakaji likaendelezwa. Kila jamii iliyopoteza mtuilifanya shughuli kumzika mtu wao bila kutaka kutafuta usaidizi wa serikali au kujaribu kueleza sababu ya vifo hivyo. Waliobakwa nao wakazibwa vinywa vyao. **Mauaji na ubakaji vikawa visa vya kawaida.** (*Kovu Moyoni*, uk 49, msisito wangu)

Mfano uliodondolewa umeangazia kisa ambapo Chifu Ngata aliyepinga operesheni ya Jeshi la Vijana ya kutafuta `usawa na haki` Rama aliposhambuliwa na jeshi hilo na kuuawa kikatili. Aidha, kwa mujibu wa *Kovu Moyoni*, ilidhihirika kuwa tokea siku alipouawa Chifu Ngata, mauaji mengine mengi yaliweza kutekelezwa Rama. Kwa hivyo, kwa mujibu wa waandishi wa riwaya hizi, mizozo ya ardhi huchangia vifo vya watu wengi, ama kwa kuchomwa, kupigwa risasi au hata kukanyangwa na wengine wanapokimbilia usalama wao.

Kwa mujibu wa Nyiri (2014), katika mizozo ya baada ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2007 nchini Kenya, ilithibitishwa kuwa kulikuwa na vifo vya watu kati ya 800 hadi 1500. Vita hivyo viliwalenga Wakikuyu, Kabila ambamo Rais Kibaki alitoka huku wakilazimishwa kuondoka katika sehemu za Bonde la Ufa. Vivyo hivyo, awali hali ya taharuki ilitanda katika maeneo hayo kila baada ya uchaguzi Mkuu kama vile mwaka wa 1992 ambapo Waluo na Wakalenjin walipigana na Wakikuyu. Kwa hivyo, mauaji kutokana na mizozo ya ardhi kama yanavyoangaziwa na waandishi wa riwaya teule yana uhalisia katika nchi ya Kenya. Hivyo, ni muhimu maafisa wa CID kwa ushirikiano na Tume ya Maadili na Kupambana na Ufisadi (EACC) kuchunguza na kuwachukulia hatua za kisheria wahusika wa unyakuzi wa mashamba.

### 4.5.2 Ukimbizi

Kwa mujibu wa TUKI (2014), ukimbizi ni hali ambapo mtu au watu huondoka kwao mahali wanapoishi kwa sababu ya kulazimishwa, kufukuzwa au kwa hofu ya kuteswa kwa sababu ya rangi, dini, utaifa, uanachama wa kikundi fulani cha jamii, au maoni ya kisiasa, na kutokana na hofu hiyo hana nia ya kutegemea ulinzi wa nchi hiyo. Aidha, ukimbizi huwajumuisha watu waliokimbia vita au vurugu nyingine katika nchi zao za asili. Kutokana na maelezo hayo, waandishi wa riwaya teule wameangazia mizozo ya ardhi kama mojawapo ya mambo ambayo husababisha ukimbizi katika nchi yoyote ile.

Kwa mfano:

> … hali ya usalama ilizidi kuzoroteka Rama. Kundi la Jeshi la Vijana lilipozidi kushambulia na kikundi cha Kaskasi nacho kilijaribu kuwaangamiza. Watu wengi **walilazimika kuhamia sehemu mbalimbali**. Sela alihamia Maluko, kwa ajili ya usalama wake na wanawe. Milka naye akahamia Zindi. Sela alitembea mwendo mrefu kwa miguu ili kufika Maluko alikokaa dadake (*Kovu Moyoni*, uk 27, msisitizo wangu)

Katika *Kovu Moyoni*, Habwe anarejelea tukio ambapo baada ya mashambulizi Rama, hali ya usalama ilizidi kuzorota. Watu walikimbilia usalama ambapo walihamia katika sehemu tofauti

tofauti kama vile kwa jamaa zao. Katika *Kufa Kuzikana*, ukimbizi unajitokeza kwa namna ifuatayo:

> Imebainika wazi kuwa mheshimiwa Mabende alitaka kuwatimua Wakanju kutoka Wilayani Korosho kwa madai kuwa hawakumpigia kura katika uchaguzi mkuu uliopita. Matokeo yakawa uharabu mkubwa. Kiwachema ikapata **wimbi kubwa la `wakimbizi` wa ndani kwa ndani ya nchi**. Wengi wao wakikimbilia mijini na majijini. Barabara za miji ya Kiwachema sasa zimejaa ombaomba mpaka zikatapika wengine (*Kufa Kuzikana*, uk 160, msisitizo wangu)

Katika *Kufa Kuzikana*, Walibora anaonyesha matokeo ya vita vya kikabila katika nchi ya Kiwachema. Watu wengi walikimbia kwao na kuhamia katika sehemu mbalimbali. Isitoshe, baada ya mizozo hiyo, nchi ya Kiwachema ilipata wimbi kubwa la wakimbizi wa ndani kwa ndani. Kwa mujibu wa vifungu vilivyorejelewa, inadhihirika kwamba baada ya mizozo ya ardhi kuzuka, watu wengi hukimbilia usalama katika sehemu mbalimbali na wengine wengi kusalia bila makao baada ya nyumba zao kuteketezwa, hali inayosababisha kuwepo kwa wakimbizi wa ndani kwa ndani. Walibora pia anaonyesha masaibu yanayowakumba wakimbizi hao kama vile kuanza kuombaomba mijini kwa sababu ya kukosa mahitaji ya kimsingi kama vile chakula na malazi.

Kwa mujibu wa Tume ya Maadili na Kupambana na Ufisadi (EACC, 2014) Tangu Kenya kupata uhuru mwaka wa 1963, kumeshuhudiwa Ukimbizi wa ndani mara kwa mara uliochochewa na siasa, ukabila na mizozo inayohusiana na suala la ardhi pamoja na maafa na miradi ya kimaendeleo. Aidha, mizozo ya kisiasa imeshuhudiwa nchini Kenya tangu Uchaguzi Mkuu wa vyama vingi wa kwanza mwaka wa 1992, na baada ya mtafaruku wa matokeo ya kura Desemba mwaka wa 2007, takriban Wakenya 664,000 walitoroka kwao na zaidi ya 1,300 kuuawa. Kwa hivyo kama inavyosawiriwa na waandishi wa riwaya teule, suala la ukimbizi nchini Kenya ni zao mojawapo la mizozo ya ardhi ambalo linapaswa kushughulikiwa.

Hali kadhalika, waandishi wa riwaya teule wanayaweka wazi masaibu yanayowakumba wakimbizi baada ya mizozo ya ardhi. Kwa mfano:

> … naam ombaomba waliokatakatwa na **ukata wasioulalia wala kuuamkia. Watu ambao paa zao ni anga na mawingu, vyoo vyao ni vijia kati ya majengo marefu, na blanketi zao ni ngozi zao walizopewa na Muumba.** Wachache wenye kujiweza kidogo wamepanga mabanda kwenye maeneo ya madongo poromoka. (*Kufa Kuzikana*, uk 161, msisitizo wangu)

Kutokana na dondoo hili, ni wazi kwamba wakimbizi wa ndani waliokimbilia sehemu mbalimbali hasa mijini kwa sababu ya mizozo ya ardhi wanapitia matatizo mengi pakiwemo ukosefu wa mahitaji ya kimsingi kama vile chakula, mavazi na malazi. Kwa hivyo, suala hili linawekwa wazi ili masilahi ya wakimbizi yaweze kushughulikiwa na serikali ya nchi, kama vile kupewa ardhi na fidia ya pesa jambo ambalo linaweza kuchangia kusitishwa kwa mizozo ya kikabila ambayo imekuwa kwa muda wa miaka mingi tangu Kenya kupata uhuru.

Kwa hivyo, wakati umefika kwa dunia kujikita katika kukabiliana na migogoro isiyokwisha kwenye baadhi ya mataifa inayozaa makundi ya wakimbizi kutokana na vita vinavyosababishwa na ukabila na mfumo mbaya wa siasa. Kadhalika, mfumuko huu wa wakimbizi usipotafutiwa mbinu za kudhibitiwa kwa kuandaliwa mazungumzo ya kusaka suluhu kati ya makundi yanayohitilafiana kutatua matatizo yanayojitokeza, upo uwezekano wa kuzalisha utitiri wa umaskini kwenye mataifa yaliyokumbwa na vita, hasa nchini Kenya.

### 4.5.3 Ubakaji

Ubakaji ni mojawapo ya athari za mizozo ya ardhi. Haya yanadhibitika kupitia dondoo hizi:

> …akakumbuka vile alivyomkaidi na vile kundi la watu kumi na wawili lilivyojimwaya katika nyumba yao. Lilikuwa limejihami kwa bunduki na mishale. Liliomba pesa **na hatimaye kuishia kumnajisi mtu na mwanawe**. (*Kovu Moyoni*, uk 43, msisitizo wangu)
>
> …nyumba zetu zinateketezwa na Wakorosho ilhali askari wa polisi wanatazama tu, bunduki mkononi, hauwapigi mshipa. **Wanawake na mabinti zetu wanabakwa dhahiri shahiri** na polisi wanavifumbia macho vitendo hivyo. Wanajali nini? (*Kufa Kuzikana*, uk 75, msisitizo wangu)

Katika *Kovu Moyoni*, mhusika Boke anakumbuka siku walipovamiwa yeye na binti yake Eddah na kundi la watu kumi na wawili. Baada ya kuomba pesa liliishia kuwanajisi wao wawili. Vilevile, katika *Kufa Kuzikana,* Walibora anamrejelea mhusika Mzee Uledi aliyekuwa amelazwa katika hospitali ya Rufaa ya Tandika akiwa na majeraha baada ya mashambulizi wilayani Korosho. Aidha, anawaeleza Tim na Akinda kuhusu namna mashambulizi hayo yalivyokuwa ambapo wanawake na mabinti zao walibakwa ilhali polisi hawakuweza kudhibiti hali ilivyokuwa. Kwa mujibu wa Maina (2015), Katika mzozo wa ardhi ulioshuhudiwa katika Wilaya ya Mlima Elgon mwaka wa 2005, maovu mengi yalitekelezwa na kikundi cha SLDF ikiwa ni pamoja na mauaji, uporaji wa mali na unajisi. Kwa hivyo, inadhibitika kwamba unajisi ni

miongoni mwa maovu ambayo hutendwa na wavamizi baada ya mizozo ya ardhi kutokea, jambo ambalo huathiri watu wengi hasa wanawake na watoto wa kike.

### 4.5.4 Visasi

Wasanii wa riwaya teule wameangazia visasi kama mojawapo ya athari za mizozo ya ardhi kupitia maneno yaliyonukulia katika dondoo zifuatazo:

> …Eddah alilala hadi asubuhi. Siku nyingi alikuwa akilala porini. Siku nyingi alilala katika miamba na mahandaki. **Aliapa angelipiza kisasi siku moja**. Vipi? Hakujua lakini aliapa lazima atakuja kulipiza kisasi pindi akipata fursa. (*Kovu Moyoni*, uk 24, msisitizo wangu)
>
> ... nilimtazama vizuri mwanamume huyo mwenye majisifu. Nywele kichwani zimemkaa timtim. Mtu wa makamo, mfupi wa kimo…aliendelea kujisifu na kujitanua kifua kwa ushujaa wake vitani. Akaamka punde kwenda haja kwenye vyoo vilivyokuwa upande wa nyuma wa klabu. …**mlango ulipofunguka nilikiinua kipande cha ubao na kumwangushia kipajini kwa nguvu zangu zote.** Akabwagika chini maliwatoni kama gunia la viazi. Hakufurukuta. (*Kufa Kuzikana*, uk 132-133, msisitizo wangu)

Katika vifungu vilivyodondolewa hapo juu, waandishi wanaeleza jinsi ambavyo wahusika walilipiza au kuapa kulipiza kisasi baada ya mashambulizi wakati wa mizozo ya ardhi. Katika *Kovu Moyoni*, mhusika Eddah mwanawe Boke alipitia masaibu mengi baada ya kutekwa na Jeshi la vijana. Siku nyingi alilala porini huku akiwafanyia Jeshi la vijana kazi pamoja na kutoa huduma za kimapenzi. Jambo hili lilimuudhi sana hadi akaapa kuwa angelipiza kisasi pindi atakapopata nafasi. Katika *Kufa Kuzikana*, Akida aliwasikiliza kundi la walevi waliokuwa wakizungumza. Mmoja wao alijigamba kuwa katika vita vya kikabila Wilayani Korosho, yeye mwenyewe aliwaua Wakanju wengi sana. Jambo hili lilimuudhi sana Akida kwani yeye ni Mkanju na pia hakujua hatima ya babake. Ndiposa aliamua kujificha na kumpiga mzee aliyejigamba kwa kipande cha ubao na kumwacha akiwa hali mahututi. Hivyo, inadhihirika kuwa baada ya mizozo ya ardhi kutokea, hali ya hasira na chuki hutokea hivi kwamba baadhi ya watu huanza kulipiza kisasi dhidi ya wavamizi.

Hali ya taharuki katika eneo la Bonde la Ufa lilisababisha mizozo ya mara kwa mara baada ya uchaguzi mkuu nchini Kenya, hasa uchaguzi mkuu mwaka wa 1992. Katika mizozo hiyo, Wakikuyu ndio waliolengwa huku wakilazimika kuhama katika maeneo walimoishi, jambo lililowachochea Wakikuyu kuanza kulipiza kisasi kwa kuwashambulia Waluo na Wakalenjin. (Njogu na wenziwe, 2015). Kwa hivyo, sio haki kwa maafisa wakuu wa usalama kuendelea

kusalia kimya huku watu wakiendelea kuuana. Kadhalika, Serikali kupitia wizara ya ardhi inapaswa kuangazia tatizo la ardhi ambalo limekuwa chanzo cha mgogoro kati ya wakazi katika maeneo mengi nchini Kenya. Vilevile, viongozi wanaweza kushauriana ili kuona jinsi bora ya kutatua mizozo ya ardhi ambayo imesababisha uhasama baina ya jamii mbalimbali.

### 4.5.5 Kuibuka kwa Wanamgambo

Mizozo ya ardhi inaweza kuibua vikundi vya wanamgambo ambavyo huanza mizozo ili kupigana na wanaodhaniwa kuwa wanyakuzi wa ardhi yao. Waandishi wa riwaya teule wameangazia suala hili kupitia dondoo zifuatazo:

> Jamii ya Sululu ndiyo inayostahili kugombea kiti hiki sio Kaisuku au haya makabila mengine. Wageni washughulike na biashara sio utawala wa eneo la Rama. Ili kufanikisha wito huu **tutabuni Jeshi letu la Vijana kuhakikisha kuwa siasa tunaidhibiti sisi wenyeji.** …Pia tungependa kuhakikisha tumepata sehemu yetu ya halali ya mashamba. Jeshi litahakikisha kuwa watu wasio wenyeji na waliopata mashamba yetu kiharamu wameng`olewa (*Kovu Moyoni*, uk 53, msisitizo wangu)

> Nilisikia tena mchakacho. Nikaingiwa utashi wa kuwaona wasemaji. Nikainua kichwa kwa tahadhari kubwa na kutazama baina ya ua. Macho yangu yakatua kwenye **kundi la wanaume kama ishirini hivi**, wenye sura za kutisha. Waliongozwa na mwanamume mtambo wa kimo, mwenye bunduki mkononi na aliyevalia sare rasmi ya Jeshi la polisi nchini kwetu Kiwachema. (*Kufa Kuzikana,* uk 106, msisitizo wangu)

Licha ya kueleza kwa mitazamo tofauti, waandishi wa riwaya teule wamerejelea wakati ambapo mizozo ya ardhi ilisababisha kuibuka kwa wanamgambo. Katika *Kovu Moyoni*, Habwe anamtumia mhusika Mwamba ambaye anahutubia vijana katika jengo la Lumbasa alipowachochea vijana hao kuhusu haja ya kuanzisha ‘Jeshi la Vijana’ ambalo lingepigania mashamba yao. Vilevile, katika *Kufa Kuzikana, Walibora* anaangazia wakati ambapo Akida alipokuwa amejificha shimoni baada ya rafikiye Tom kuvamiwa na washambulizi walipoenda kumzika babake. Analiona kundi la wanaume kama ishirini hivi ambao walikuwa wakiwashambulia watu Wilayani Korosho huku wakiwatimua Wakanju ambao walidhaniwa kuwa wageni mahali pale. Barasa (2013), anaafikiana na madai kuwa mizozo ya ardhi wakati mwingine huibua makundi ya wanamgambo anapoeleza kuwa kuzuka kwa mizozo na kuongezeka kwa Wanamgambo husababishwa na mambo mbalimbali kama vile uhaba wa rasilimali ya ardhi, ukosefu wa ajira miongoni mwa vijana na kukua na kuongezeka kwa umma.

Akieleza kuhusu Nadharia ya Baadaukoloni, Fanon (1961) anayaweka wazi masuala yanayohusiana na ubaguzi wa kimagharibi na jinsi ubaguzi huo unavyokuwa msingi mkubwa wa kuendelea kushikilia nguvu na kwa njia hiyo kuwalazimisha waliotawaliwa kutumia nguvu ili kujikomboa. Kwa hivyo, Fanon anadai kuwa hatua ya kwanza ya watawaliwa katika kujikomboa ni kurudia historia yao ya kale. Haja ya kujikomboa kutokana na utawala dhalimu unajitokeza katika riwaya teule ambapo kunazuka mizozo ya ardhi katika jamii huku wenyeji wakiwafurusha wanaodhaniwa kuwa `wageni` katika jamii hizo.

Hali kadhalika, masuala ya ardhi eneo la Mlima Elgon nchini nchini Kenya yalizua kuibuka kwa wanamgambo wa SLDF mwaka wa 2005, waliochukua silaha wakitaka kurejeshewa ardhi yao ya jadi iliyokuwa ikimilikiwa na serikali. Mamia ya watu wamepoteza maisha yao na maelfu ya wengine kuachwa bila makazi tangu SLDF ilipoanzisha vita. Goffard (2011) anaeleza kuwa wanamgambo wa Mungiki hudhaniwa kuwa kizazi cha miaka ya hamsini, enzi za harakati za Maumau nchini Kenya ambapo Wakikuyu walipigana vita na wakoloni wabriteni chini ya bendera ya `Ardhi na Uhuru`. Kwa hivyo ni wajibu wa Serikali kuendeleza oparesheni kubwa ya kijeshi dhidi ya wanamgambo na makundi mengine haramu ili kukomesha visa vya kigaidi ambavyo hutekelezwa na vikundi hivyo.

### 4.5.6 Majuto

Baadhi ya wahusika katika riwaya za *Kovu Moyoni* na *Kufa Kuzikana* wanakumbwa na majuto mengi baada ya kutenda maovu yaliyohusiana na mizozo ya ardhi. Vifungu vifuatavyo vinashadidia haya:

> Mulota alikaa mwembeni akiwaza kwa nini wale wazee walimwambia na kumtisha vile. **Alikumbuka majuto aliyokuwa nayo kuhusu visa vya Wasululu vilivyomfanya kutaka hata kuacha kazi ya kuwa polisi**. Alikumbuka alivyotumiwa na Mwamba na Meja-K kutesa watu kwa sababu hawakuwa Wasululu. Mulota aliona hali kama ile haifai. Yeye, kama mtu mzima aliye katika taifa huru, alikuwa na uhuru, alikuwa na uhuru wa kuamua mambo aliyotaka. (*Kovu Moyoni*, uk 142, msisitizo wangu)

> Najaribu mara mbili tatu kuingia kwenye majengo ya ghorofa yaliyoko karibu. Walinzi wanaonishuku kuwa mwendawazimu au motto wa kikopo, wananizuia kingie ndani. Haya ni majoka ya mdimu, yanachunga watundao. Au nijitupe mbele ya gari liendalo kasi? Na itakuwaje likinivunja tu, hata linijeruhi vibaya, lakini nisife kama nitakavyo? **Jamani mzigo huu wa kumwua mtu…Hatia ya kumwua mtu, hata kama alikuwa mkosaji…**Acha niende tu kwenye kituo cha polisi na liwe liwalo. (*Kufa Kuzikana* uk 185, msisitizo wangu)

Katika *Kovu Moyoni*, Mulota anaonywa na wazee wake dhidi ya kuoa Eddah ambaye hakuwa Msululu. Aidha, wanamweleza waziwazi kuwa jamii ya kina Eddah ni maadui zao kwani mara kwa mara wamezozania mashamba. Mulota anakumbuka maovu yote aliyotendea `maadui` hao alipokuwa polisi na kujutia makosa yake. Vilevile, anaamua kujiuzuru kutoka kazi kwa sababu ya majuto ya kushiriki katika mashambulizi. Katika *Kufa Kuzikana*, Akida anajutia kosa la `kumuua` Mzee Zablon babake Tom kwa kujigamba kuwa aliwaua wakanju wengi katika vita vya kikabila wilayani Korosho. Majuto haya yanamkosesha amani hadi anaamua kujisalimisha kwa polisi. Kwa hivyo, ni dhahiri kuwa mizozo ya ardhi huweza kuleta majuto mengi na hivyo kukosesha watu amani, na ndio maana waandishi wa riwaya teule wanakashifu visa hivyo.

### 4.5.7 Umaskini

Riwaya za *Kovu Moyoni* na *Kufa Kuzikana* zinadhuhirisha kuwa mizozo ya ardhi husababisha umaskini. Hii ni kwa sababu watu wanaodhaniwa kuwa `wageni`hufukuzwa kutoka makazi yao na kuachwa bila chochote huku wengine wakisalia wajane na watoto mayatima baada ya wazazi wao kuuawa. Kwa mfano:

> … nahodha wa chomboTim, alituelekeza tukapita mawimbi *ya* **chakula haba cha mashindio na kulalia mate,** kwa siasa yake nzuri. Hapakuwa na nafasi ya kuzembea. Kila mtu alipaswa kuchangia kuzumbua riziki. Tim na mimi tukirauka kila alfajiri kwenda **kukoroga zege, kuchimba mitaro, kubeba magunia ya mazao sokoni, kusukuma rukwama, kufanya utopasi na kadhalika, muradi turejee nyumbani na chochote.** Tamari ambaye alikuwa kapata nafuu, alikwenda kuwafulia matajiri nguo majumbani mwao au kuwapigia nyumba deki maadamu tu aje nyumbani na chochote. (*Kufa Kuzikana*, uk 119, msisitizo wangu)

Mfano uliodondolewa kutoka riwaya ya *Kufa Kuzikana* unaonyesha namna umaskini ulivyokithiri baada ya mizozo ya ardhi kutokea. Kwa mfano, Akida anasimulia jinsi yeye, Tim na Tamari walivyoishi kwa kuhangaika huku wakifanya vibarua vya kila aina muradi wapate chakula. Hii ilikuwa baada ya vita kutokea kwao nyumbani Wilayani Korosho ambapo walilazimika kutorokea mjini. Katika *Kovu Moyoni,* Habwe anafumbata umaskini kama inavyojitokeza katika dondoo lifuatalo:

> "Niko shwari, mama," Meja-K alisema. Hakutaka kumweleza mamake jambo la kumletea matata. Aliona mama yake alikuwa tayari amepata mateso mengi wala hakustahili kuteseka zaidi. Meja-K aliendelea kukaa. **Alikosa vitu vya kimsingi. Alikosa hata chakula.** Hapo ndipo akili zake zilipoanza kurudia kwenye ile sehemu ya baba yake ya shamba la bwanyenye. (*Kovu Moyoni*, uk 17, msisitizo wangu)

Kifungu kilichodondolewa kinamrejelea Meja-K na familia yake ambao walisalia wachochole baada ya shamba walilomiliki kunyakuliwa na Chifu Malonza na kuuziwa bwanyenye mmoja kutoka Dunga aliyepanda mipamba. Aidha, ni humu shambani ambamo mama yake mzazi pamoja naye walifanya kazi kama vibarua na kulipwa pesa kidogo na posho kidogo lakini kwa bezo la kupindukia. Vilevile, umaskini katika *Kovu Moyoni* unajitokeza kupitia Meja-K baada ya shamba la babake kunyakuliwa na hatimaye akauawa na kundi la Jeshi la Vijana lililotekeleza mashambulizi huko Rama. Meja-K na mamake wanateseka huku wakikosa mahitaji ya kimsingi kama vile chakula. Aidha mamake anahangaika kila mahali akitafuta haki yake ya shamba lakini hakuna aliyemsikiliza. Kwa hivyo, umaskini uliosawiriwa na waandishi wa *Kufa Kuzikana* na *Kovu Moyoni* ni ule ambao unawakumba wananchi wanaokimbia kwao kwa sababu ya mashambulizi, au ule unaotokana na unyakuzi wa ardhi ya wananchi na mabwanyenye wabinafsi wasiojalia maslahi ya wengine.

Kwa mujibu wa Nadharia ya Baadaukoloni, mizozano mingi katika jamii zilizotawaliwa na Wakoloni ilitokana na hali ya uchumi ulioletwa na Mkoloni ambayo hutokana na utambulisho. Visa vya unyakuzi wa ardhi vimeongezeka katika maeneo mengi nchini Kenya kama vile katika kaunti ya Mombasa na ukanda wa Pwani kwa jumla, ni muhimu Tume ya ardhi nchini, NLC kutolifumbia macho suala hilo. Tabia ya unyakuzi wa ardhi inapaswa kusitishwa mara moja kwa kuwa imesababisha wakaazi wengi kuishi maisha duni na ya uskwota. Vilevile, kwa kuwa baadhi ya viongozi wanaoshirikiana na mabwanyenye katika unyakuzi wa ardhi, hatua ambayo ni unyanyasaji na dhuluma miongoni mwa wananchi, hatua kali za kisheria zinapaswa kuchukuliwa dhidi ya yeyote atakayepatikana na hatia.

### 4.5.8 Kuzorota kwa Hali ya Uchumi

Kila baada ya mizozo ya ardhi kutokea, hali ya uchumi wa nchi huzorota kwa namna mbalimbali. Akieleza kuhusu uhusiano uliopo baina ya mizozo ya kikabila na kuzorota kwa uchumi wa nchi, Nyiri (2014) anarejelea mizozo ya baada ya uchaguzi mkuu nchini Kenya kati ya mwaka 2007 hadi 2008. Anaeleza kuwa uchumi wa nchi uliathirika kwa njia mbalimbali kama vile uhaba wa chakula, ukosefu wa usalama, kuathiriwa kwa shughuli za kilimo, kupunguka kwa uzalishaji wa kiuchumi, unyakuzi wa ardhi, kukatizwa kwa uchukuzi na mawasiliano, uharibifu wa mali na mazingira miongoni mwa mengine. Wasanii wa riwaya za *Kovu Moyoni* na *Kufa Kuzikana*

wameshadidia jambo hili katika kazi zao kwa kuonyesha chanzo na athari zake kwa wananchi. kwa mfano:

> … wafadhili wamezuia misaada na kuongeza msumari wa moto kwenye donda. **Uchumi umevia, na unatarajiwa kudidimia zaidi. Upo mfumko wa bei na uhaba wa bidhaa kila mahali Kiwachema. Mishahara nayo imekuwa kama maziwa ya kuku, muhali kupatikana. Walimu hawana mishahara. Wafanyikazi na mabaraza ya miji hawaijui rangi ya mishahara miezi nenda miezi rudi**. Wametelekeza kazi zao ama wanafanya biashara au wanazumbua riziki kwa kuwabughudhi wachuuzi ili wapewe `kitu kidogo`. (*Kufa Kuzikana*, uk 161, msisitizo wangu)

Kwa mujibu wa *Kufa Kuzikana*, inadhihirika kuwa baada ya vita vya kikabila Wilayani Korosho, hali ya uchumi ilizorota hasa wakati wafadhili walipozuia misaada kwa waathiriwa wa mizozo hiyo. Hali hii ilijitokeza kupitia mfumko wa bei na uhaba wa bidhaa kila mahali Kiwachema na pia kukosekana kwa mishahara ya walimu na wafanyikazi wa mabaraza ya miji, jambo ambalo lilisababisha maovu ya kila aina pakiwemo wafanyikazi hao kuzumbua riziki kwa kuwabughudhi wachuuzi ili wapewe hongo. Kadhalika, Habwe anafumbata kuzorota kwa hali ya uchumi kama inavyojitokeza katika dondoo hili:

> Hao waliofika walikuwa wazee. Mmoja alikuwa na miaka sabini. Mwingine alikuwa na miaka sitini hivi. Wakati mashambulizi yalipokuwa yakivuma hapakuwa na bawabu ambaye angethubutu kuwa shuleni kulinda kitu. **Si ajabu milango, madirisha na vitu vya thamani viling`olewa na miti ikakatwa.** Shule ikawa katika maombolezo makubwa. **Viti, kompyuta, na mifugo, vyote vilikokolewa** vikaingia katika fidia waliyotaka hao Jeshi la Vijana. (*Kovu Moyoni*, uk 105, msisitizo wangu)

Hali ya uchumi kuzorota inadhihirika katika *Kovu Moyoni* baada ya mashambulizi katika kijiji cha Siloko katika nchi huru ya Tandika. Mashambulizi hayo yalisababisha shule ya Lumbasa Academy kufungwa huku walimu, wanafunzi na wafanyikazi wengine wa shule hiyo wakitorokea sehemu mbalimbali kwa sababu ya ukosefu wa usalama. Isitoshe, vitu vya thamani katika shule hiyo kama vile milango, madirisha, viti, kompyuta na mifugo vyote vilichukuliwa na Jeshi la Vijana. Kwa hivyo, kutokana na vifungu vilivyonukuliwa katika riwaya teule, inabainika kuwa mizozo ya ardhi inaweza kusababisha kuzorota kwa uchumi wa nchi unaodhihirika kutokana na mfumko wa bei na uhaba wa bidhaa na kukosekana kwa mishahara ya wafanyikazi. Vilevile, shule na hospitali zinafungwa ama kwa ukosefu wa walimu na wauguzi wanaotorokea sehemu mbalimbali kwa sababu ya usalama wao au kufungwa baada ya kuchomwa na kuibiwa vifaa muhimu vya matumizi.

Kwa hivyo, inabainika kuwa kushamiri kwa mizozo ya ardhi kumekuwa kukisababisha kudumaa kwa uchumi kwa wananchi kwani wakati mwingine wakulima wamekuwa wakishindwa kuzalisha mazao, wafugaji mifugo yao kujeruhiwa, wawekezaji nao mali zao kuharibiwa na wananchi kutokana na kugombea ardhi kwa ajili ya kufanya shughuli mbalimbali za kiuchumi. Hivyo, utatuzi na usuluhishi wa migogoro ya ardhi mapema kutadumisha na kuchangia ukuaji wa uchumi na pia kutadumisha ushirikiano na amani kati ya wakulima na wafugaji na Serikali kwa ujumla. Zaidi ya hayo, usimamizi mzuri wa masuala ya ardhi utasaidia kuondoa urasimu uliopo, vikwazo na mlindikano wa kesi mahakamani.

### 4.5.9 Magonjwa

Kwa mujibu wa waandishi wa riwaya teule, mizozo ya ardhi husababisha magonjwa kwa waathiriwa. Haya yanajitokeza katika dondoo hizi:

> Boke alikubali akalazwa katika kliniki sogevu waliyokuwa nayo watu wa shirika la Chunga Ndugu Yako. Baada ya uchunguzi wakamweleza: "**una matatizo yanayoitwa nasuri, yaani, fistula,"** lotodo alimweleza huku akikisoma kikaratasi kilichoandikwa na askari aliyekuwa akitoa huduma ya dawa. **Ni hali ambayo mgonjwa anashindwa kuizuia mikonjo yake kwa kuwa na jipu au uvimbe wenye uwazi Fulani**. Lotodo alimwangalia Boke aliyeangalia kando huku akielezwa habari za ugonjwa. (*Kovu Moyoni,* uk 103, msisitizo wangu)

> Niliingia ndani taratibu nikaketi kochini. Taathira ya uanana wa Pam kwangu na kwa mtesi wangu ilikuwa hisia ya hatia. Pam hakukemea, hakukaripia yeyote kati yetu. Msuluhishi hasa huyu. Nilijichukia nafsi yangu kwa kuhamaki kwa sababu ya maneno ya Tamari. Nilichushwa na nafsi yangu. **Mbona sikubaini mwenyewe kuwa Tamari ni mgonjwa, nimhurumie wala sio kumwona kama hasimu wa kuhasimiana naye?** (*Kufa Kuzikana*, uk 67, msisitizo wangu)

Katika *Kovu Moyoni*, Boke anaathirika kiafya baada ya kubakwa na makundi mara kadhaa. Zaidi ya hayo, Boke anagunduliwa kuwa na matatizo ya Fistula. Katika *Kufa Kuzikana,* Tamari anaathirika kiakili baada ya kushuhudia mizozo ya ardhi kwa misingi ya kikabila ambapo pia aliponea tundu la sindano walipojaribu kumnajisi akajinasua. Aidha, alitembea kwa miguu na kulala msituni siku kadhaa huku akiona maiti za watu waliouawa. Akichangia kuhusu athari za mizozo ya aina mbalimbali nchini Kenya, Nyiri (2014) anasema kuwa mizozo yoyote ile ambayo imekuwepo nchini imesababisha kuwepo kwa wakimbizi wa ndani nchini, kuenea kwa magonjwa kama vile kipindupindu na Ukimwi, kutimuliwa kwa halaiki, vifo, na kuzorota kwa maendeleo ya kijamii, kisiasa na kiuchumi katika mataifa ya kiafrika kwa jumla. Kwa hivyo,

waandishi wa riwaya teule wanadhihirisha kuwa mizozo ya ardhi husababisha madhara mengi kwa waadhiriwa pakiwemo magonjwa.

### 4.5.10 Ukosefu wa Usalama

Kwa mujibu wa Maina (2015), usalama ni jambo muhimu na la kimsingi ili taifa lolote lile liweze kuendelea na kuangazia uchumi wake. Aidha, kwa binadamu, usalama ni muhimu kwa sababu huleta amani. Kutokana na umuhimu wake, ukosefu wa usalama huwafanya watu kuishi bila utulivu na kwa uwoga. Wayua (2015) anafafanua baadhi ya chanzo cha ukosefu wa usalama kwa kusema kuwa mara nyingi husababishwa na chuki au matamshi ya chuki. Isitoshe, siasa nchini huzua suala la ukabila ambalo hatimaye huleta chuki miongoni mwa makabila ya Kenya. Ndiposa Maina (2015) anasema kuwa mizozo ya baada ya uchaguzi mkuu kati ya mwaka 2007 hadi 2008 ilisababisha athari nyingi kwa Wakenya, pakiwemo ukosefu wa usalama. Waandishi wa riwaya teule wamedhihirisha athari za ukosefu wa usalama kupitia dondoo zifuatazo:

> **Hali ya usalama ilizidi kuzoroteka Rama. Kundi la Jeshi la Vijana lilipozidi kushambulia na kikundi cha kaskasi nacho kilijaribu kuwaangamiza. Watu wengi walilazimika kuhamia sehemu mbalimbali. Sela alihamia Maluko, kwa ajili ya usalama wake na wanawe.** Milka naye akahamia Zindi. Sela alitembea mwendo mrefu kwa miguu ili kufika Maluko alikokaa dadake. (*Kovu Moyoni*, uk 27, msisitizo wangu)
>
> …Baadhi yao wamegeuka sinzia, vibaka, na wezi wa mabavu. Wengine wamegeuka malaya wanachuuza vinofu vyao. Ni maumbufu makubwa yaliyoje kutazama jinsi wasichana na akina mamawanavyopiganiawateja wanaume. **Usalama mijini umezorota. Sura ya miji ni sura ya ombaomba na wahuni watupu.** Wilayani Korosho mambo ni yaleyale ya uharabu. Wakorosho wametaifisha mashamba na mali ya Wakanju. (*Kufa Kuzikana*, uk 161, msisitizo wangu)

Kutokana na vifungu vilivyonukuliwa hapo juu, waandishi wa riwaya teule wameangazia ukosefu wa usalama kutokana na mizozo ya ardhi, jambo ambalo liliathiri wahusika kwa namna mbalimbali. Kwa mfano, katika *Kovu Moyoni,* Habwe ameangazia hali ambapo hali ya usalama Rama ilizidi kuzoroteka baada ya mashambulizi yaliyotekelezwa na Jeshi la Vijana. Jambo hili lililazimisha wahusika wengi kuhamia sehemu mbalimbali kwa ajili ya usalama wao na wanao, kwa mfano Sela alihamia Maluko naye Milka akahamia Zindi. Katika *Kufa Kuzikana,* Walibora anaangazia hali ya usalama iliyozorota baada ya mizozo iliyotokea Wilayani Korosho ambapo baada ya watu kuhamia mijini, walijiingiza katika kila aina ya uozo huko mijini kama vile ukahaba na uhuni kwa sababu ya umaskini. Jambo hili linasababisha hali ya usalama kudorora hadi mijini. Kwa mujibu wa Institute of Security Studies (ISS, 2015), ukosefu wa haki wa

kihistoria kuhusu ugavi wa ardhi katika maeneo mbalimbali nchini Kenya umesababisha mizozo mara kwa mara miongoni mwa makabila tofauti, kama vile eneo la Bonde la Ufa na Pwani, hali ambayo imechangia pakubwa katika kuzoroteka kwa hali ya usalama.

Kutokana na tisho la ukosefu wa usalama katika mataifa mengi barani Afrika, ni jambo muhimu kuandaa mipango ya kuthamini usalama na amani katika mataifa hayo Sanjari na kupambana na umaskini. Suala la usalama limegeuka na kuwa tatizo kubwa kwa nchi za kiafrika ambapo ugaidi umekuwa jinamizi kwa nchi zote za dunia. Kwa hivyo, kuwepo kwa viongozi dhaifu, hali mbaya ya kisiasa, kukosekana kwa nafasi za kazi na pato ndogo kwa vijana na kutosuluhishwa kwa mizozo ya ardhi ni mambo yaliyochangia makundi ya kigaidi kuibuka na kuchangia pakubwa katika kuzorota kwa hali ya usalama.

### 4.5.11 Kuathiriwa kwa Masomo

Miongoni mwa waathiriwa wakuu wa mizozo ya ardhi ni watoto hasa walio katika umri wa kwenda shuleni. Jambo hili huchukua mielekeo tofautitofauti kama linavyodhihirishwa na waandishi wa riwaya teule kupitia dondoo zifuatazo:

> … katika kipindi nilichokaa Falkland **niliwazia sana kuhusu hatima ya elimu yangu na mustakabali wangu kwa jumla**. Nilipitia, kwenye ofisi za wizara ya elimu mara kadhaa kuwashtakia hali wakuu wa elimu. Baada ya `nenda urudi kesho` nyingi, **nikaja kugundua kuwa nafasi yangu katika Shule ya Upili ya Kitaifa ya Kiwachema nilikoitwa, ilikuwa imetwaliwa na mtoto wa tajiri mmoja. Aidha udhamini wangu kutoka kwa wizara, ulikuwa umepotea.** "Umechelewa," aliniambia sekretarimmojawapo katika ofisi za wizara (*Kufa Kuzikana,* uk 126, msisitizo wangu)

> … mawazo ya Mwita yalikwenda tena kwenye ule mtihani wake wa kidato cha nne hapo Rama Boys. Alikumbuka kuvunja rekondi ya shule hiyo katika ubora wa matokeo ya mtihani. Alitazamia kuwa injinia wa kwanza pale Rama. Alitazamia kusaidia kuleta maendeleo katika sekta ya uhandisi**… safari ndefu ya kheri ya Mwita ilikatwa na kuwa 'safari ya majonzi na simanzi tupu.** Nyota ya Siloko na Rama nzima ilizimwa na wingu jeusi la Jeshi la Vijana. (*Kovu Moyoni,* uk 92, msisitizo wangu)

Kutokana na vifungu vilivyodondolewa, inadhihiriki kwamba elimu ya wanafunzi iliathirika kwa namna mbalimbali. Kwa mfano, mhusika Akida katika *Kufa Kuzikana* anakuwa na mawazo mengi kuhusu hatima ya elimu na mustakabali wake kwa jumla baada ya vita vya kikabila Wilayani Korosho ambapo babake aliuawa katika vita hivyo na kusalia yatima. Aidha, anagundua kuwa nafasi yake katika Shule ya Upili ya Kitaifa ya Kiwachema imechukuliwa kwa sababu ya kukaa kwa muda mrefu kabla ya kwenda shule, jambo ambalo linamhuzunisha sana.

Vilevile, Habwe katika *Kovu Moyoni* anaangazia kisa ambapo mhusika Mwita anahukumiwa kunyongwa baada ya kudhaniwa kuwa mwanachama wa Jeshi la Vijana ambao walitekeleza mashambulizi Rama. Baada ya kufuzu katika mtihani wa kidato cha nne na kuibuka kuwa mwanafunzi bora zaidi, Mwita alitazamia kusaidia kuleta maendeleo katika sekta ya uhandisi. Lakini ndoto yake inazimwa ghafla baada ya mizozo ya ardhi kutokea. Akifafanua baadhi ya athari za mizozo katika jamii, Nyukuri (1997) anaeleza kuwa kwa sababu ya mizozo nchini Kenya, maelfu ya watoto wa umri wa kwenda shule walitimuliwa, baadhi yao walitoka shule kwa sababu ya ukosefu wa karo na sababu zingine zinazohusiana na mizozo hiyo. Kwa mfano, Nyukuri anasema kuwa ilikadiriwa ya kwamba kufikia mwaka wa 1994, zaidi ya watoto elfu kumi katika wilaya ya Trans-Nzoia walikuwa wamefurushwa kutokana na mizozo. Kwa hivyo kama wasanii wa riwaya teule wanavyosawiri, mizozo ya ardhi huathiri masomo kwa kiasi kikubwa, ndiposa pana haja ya kutafutiwa suluhisho la kudumu kama jambo la dharura.

## 4.6 Hitimisho

Sura hii imeangazia jinsi mizozo ya ardhi imesawiriwa na waandishi wa riwaya za *Kovu Moyoni* na *Kufa Kuzikana.* Utafiti huu umegundua kwamba miongoni mwa mambo ambayo husababisha mizozo ya ardhi ni ugavi na umiliki wa ardhi usioridhisha na pia wanajamii huzozania mipaka ya mashamba yao yanayopakana. Imebainika pia kuwa suala la mizozo ya ardhi ni suala la kihistoria ambalo lilianza tangu jadi. Vilevile, inadhihirika kwamba sababu za kuwepo kwa mizozo ya mara kwa mara ni kwa sababu masuala ya kihistoria yanayohusiana na ardhi pakiwemo mipaka na umiliki wa ardhi hayajaweza kusuluhishwa kikamilifu kupitia serikali na taasisi nyinginezo zinazohusika katika kushughulikia masuala ya ardhi.

Zaidi ya hayo, imegunduliwa kuwa kunao uhusiano wa karibu baina ya mizozo ya ardhi siasa na ukabila. Kadhalika, matokeo ya utafiti huu yamebaini kuwa mizozo ya ardhi husababisha madhara mengi sio tu kwa watu binafsi bali kwa taifa kwa jumla. Athari hizo ni kama vile vifo, ukimbizi, ubakaji, visasi, kuibuka kwa wanamgambo, majuto, umaskini, kuzorota kwa hali ya uchumi, magonjwa, ukosefu wa usalama na kuathiriwa kwa masomo.

# SURA YA TANO

# NAMNA FANI ZA LUGHA ZINAVYOWASILISHA ATHARI ZA MIZOZO YA ARDHI KATIKA RIWAYA ZA *KOVU MOYONI* NA *KUFA KUZIKANA*

## 5.0 Utangulizi

Madhumuni ya pili katika utafiti huu yalikuwa kueleza namna wasanii wa riwaya za *Kufa Kuzikana* na *Kovu Moyoni* walivyotumia fani za lugha kuwasilisha athari za mizozo ya ardhi. Kwa mujibu wa Wamitila (2003), fani ni dhana ambayo hutumiwa kuelezea muundo au mpangilio wa kazi fulani ya kifasihi au hata sehemu zake. Aidha, fani huelezea mbinu na mtindo wa kuyawasilisha yaliyomo au maudhui. Kwa mujibu wa melezo ya Wamitila, wasanii wa riwaya za *Kovu Moyoni* na *Kufa Kuzikana* wametumia fani za lugha mbalimbali kudhihirisha athari za mizozo ya ardhi. Fani hizo ni kama vile jazanda, taswira, mbinu rejeshi, taharuki, tashhisi, kinaya, sitiari na barua.

## 5.1 Jazanda

Kwa mujibu wa Wamitila (2003), jazanda ni istilahi ambayo hutumiwa kuelezea hasa sifa za matumizi ya picha katika kazi za kifasihi. Kwa hivyo mbinu hii huwa inatumiwa na waandishi kusawiri mambo mbalimbali fiche yanayojitokeza katika jamii. Waandishi wa riwaya teule wametumia Jazanda kama ifuatavyo:

> "Ninawapongeza kwa juhudi zenu. Ninawapongeza kwa uzalendo wenu pia. Kufuatia juhudi zenu tumefaulu kutoa **gugumaji ndani ya maji yetu**. Limetoka na sasa tunataka tubaki na **maji safi**. Gugumaji lina hasara nyingi. Nyinyi mnajua. **Limenyonya maji yetu**. Limetambaa kote. Hatuwezi kulivumilia. Lazima tuling`oe na tulikate bila huruma. Wafadhili wengi wako nyuma yetu. Watu mashuhuri hapa Rama pia wako nyuma yetu na muhimu Zaidi, umma uko yetu. (*Kovu Moyoni*, uk 27, msisitizo wangu)

Katika dondoo la hapo juu, mhusika Meja-K aliyekuwa kiongozi wa wanamgambo wa Jeshi la Vijana anawahutubia vijana hao. Anawapongeza kwa kufaulu kuling`oa `gugumaji` katika `maji` yao ili wabaki na` maji safi`. Gugumaji katika muktadha huu ni watu wanaodhaniwa kuwa wageni katika Rama ambao wameshambuliwa na kuondolewa kwa kusingiziwa kuwa walinyakua mashamba ya wenyeji wa hapo. Kwa mujibu wa Muchiri (2016), wanasiasa na viongozi wengine kama inavyosawiriwa katika riwaya ya *Kovu Moyoni*, hutumia vijana hasa wale ambao hawana ajira kuhubiri injili yao ya chuki dhidi ya `wageni`. Hivyo, husababisha mateso yasiyokadirika miongoni mwa familia nyingi. Kwa hivyo, wanasiasa wanapaswa kuonywa dhidi ya kuchochea wakazi kuhusu ardhi kwa manufaa ya kibinafsi.

> Boke alikubali akalazwa katika kliniki sogevu waliyokuwa nayo watu wa shirika la Chunga Ndugu Yako. Baada ya uchunguzi wakamweleza: "**una matatizo yanayoitwa nasuri, yaani, fistula."** Lotondo alimweleza huku akikisoma kikaratasi kilichoandikwa na askari aliyekuwa akitoa huduma ya dawa. Ni hali ambayo mgonjwa anashindwa kuizuia mikojo yake kwa kuwa na jipu au uvimbe wenye uwazi fulani," Lotodo alimwangalia Boke aliyeangalia kando huku akielezwa habari za ugonjwa. (*Kovu Moyoni*, uk 103, msisitizo wangu)

Katika dondoo lililonukuliwa, mhusika Boke anapata ugonjwa wa fistula baada ya kubakwa mara kadhaa na Jeshi la vijana na vilevile askari wa Jeshi la taifa. Boke anapougua Fistula ni jazanda ya matokeo ya mashambulizi ambapo waathiriwa wa mizozo ya ardhi hupitia masaibu mengi. Kwa mfano, waathiriwa wengi wa mizozo ya kikabila baada ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2007 walisalia kuwa wakimbizi wa ndani na kuishi kwa hali ya umaskini huku wakitegemea misaada ya vyakula, mavazi na malazi. Ndiposa Boke anakuwa na harufu mbaya sana hivi kwamba watu wanamtoroka.

Boke katika *Kovu Moyoni* anawakilisha maelfu ya Wakenya ambao wameteseka kwa sababu ya vita vya kikabila ambavyo msingi wake ni suala la ardhi. Kunajisiwa kwake kunaweza kuelezwa kuwa jazanda ya unajisi ambao Wakenya hupitia kila mara ambapo wanasiasa hutamka maneno ya chuki. Watu ambao uhubiri `uwingine`wamenajisi umoja wa Wakenya na kuwaacha na ugonjwa wa Fistula wakiwa na uvundo mbaya wa chuki na vita. Aidha Boke anapotibiwa ugonjwa wa Fistula na kupona ni jazanda ya kufika mwisho kwa masaibu yanayowakumba Wakenya kutokana na mizozo ya ardhi ikiwa mikakati mwafaka itazingatiwa.

Katika *Kufa Kuzikana*, Walibora anasema:

> … Siku moja mbunge wa kwetu Johnstone Mabende alihutubia mkutano wa hadhara katika kituo cha biashara cha Baraki. Nakumbuka mpaka sasa alivyosema; … hatutaki **`madoadoa`** hapa. **Wakanju sharti wahame warudi kwao Kanju.** Mheshimiwa Mabende alishangiliwa kwa hoihoi na nderemo na Wakorosho. (*Kufa Kuzikana,* uk 2, msisitizo wangu)

Katika *Kufa Kuzikana*, `madoadoa`ni kiwakilishi cha Wakenya ambao wanaishi mahali ambapo sio kwao asilia. Huenda walinunua vipande vya ardhi na kuanza kuishi mahali hapo. Kwa hivyo mheshimiwa Mabende aliyekuwa mbunge wa Baraki anawakilisha wanasiasa ambao huchochea wenyeji wa maeneo wanayowakilisha dhidi ya `wageni`hasa wanaposhukiwa kuwa hawawapigii kura kila baada ya Uchaguzi Mkuu, kama ilivyotokea nchini Kenya baada ya uchaguzi mkuu mwaka wa 1992 na kati ya 2007 hadi 2008. Kwa hivyo, wanasiasa wanafaa kusitisha kuangazia suala la ardhi kwenye kampeni za kisiasa na badala yake kuachia Tume ya

Kitaifa ya Ardhi (NLC) jukumu la kusuluhisha matatizo ya ardhi nchini kwa kuzingatia Katiba, Sheria mbalimbali za ardhi na Sera ya Ardhi ya 2009.

Vilevile matumizi ya Jazanda yanajitokeza katika *Kufa Kuzikana* kama ifuatavyo:

> … siku moja katika mwaka wangu wa pili Wilayani Sangura, nilikuwa nikiisikiliza redio na Mzee Muyaka nje ya nyumba yake. **Redio ikitangaza kuwa Waziri Johnstone Mabende ameuawa kwa kupigwa risasi na mtu asiyejulikana.** Alikuwa anahudhuria dhifa ya jioni kwenye hoteli moja kubwa Jijini Tandika wakati wa kufikwa na maafa hayo. Nilipomtazama mwajiri wangu usoni niliona hajali wala habali. (*Kufa Kuzikana*, uk 173, msisitizo wangu)

Kwa mujibu wa dondoo hilo, Walibora katika *Kufa Kuzikana* anatumia jazanda ya kifo cha Waziri Mabende kuwakilisha kufika tamati kwa visa vya uchochezi kutokana na wanasiasa ambavyo huzua mizozo ya kikabila. Hii ni kwa sababu ndiye amesawiriwa kuwa mwanzilishi wa mizozo hiyo. Kwa hivyo, kwa mujibu wa mwandishi, ili kukomesha visa vya chuki kutokana na uchochezi wa viongozi, wananchi hawana budi kuwaondoa mamlakani viongozi kama hao. Hivyo, Walibora anadhihirisha kuwa licha ya mizozo ya ardhi kuwa sugu na kuendelea kuathiri watu katika maeneo mengi Barani Afrika, bado kunayo matumaini ya kupata suluhisho la kudumu, na hatua ya kwanza itakuwa ni kuwakomesha wanasiasa dhidi ya uchochezi kwa raia.

Habwe anaonyesha athari za mizozo ya ardhi kupitia mfano ufuatao:

> "…Wageni?" Bi. Ngata aliuliza huku akiangalia kovu la Boke la shavuni alilopata siku moja aliposhambuliwa. **Kovu hilo lilipona. Lakini hufika wakati mwingine likawasha, likaanza kutumbuka usaha**. "Wageni!" Boke alijibu swali la mwenzake huku amemtumbulia macho makali. "Lo! Mungu ni wa ajabu," Bi. Ngata alisema akimtazama mwenzake huyo. (*Kovu Moyoni*, uk 113, msisitizo wangu)

Kupitia kifungu kilichodondolewa, kovu la Boke la shavuni alilopata siku moja aliposhambuliwa ni jazanda ya uchungu moyoni mwa Wakenya wengi ambao walidhulumiwa wakati wa mizozo ya ardhi. Aidha, ni dhihirisho kwamba mbegu ya chuki miongoni mwa Wakenya kwa misingi ya kikabila ilipandwa na wanasiasa na viongozi wengine na ndiposa mwandishi anaonyesha kwamba licha ya kuwa Kovu la Boke lilipona, hufika wakati mwingine likawasha na kuanza kutumbuka usaha. Kama anavyosema Muchiri (2016), Serikali ya Kenya haijadhihirisha kuwajibika kikamilifu katika kushtaki wale ambao waliharibu mali, wakatimua familia, wakanyakua mashamba na kuua wengine tangu mzozo wa 1992 hadi sasa. Kwa hivyo kovu la Boke linapowasha na kutoa usaha ni kiwakilishi cha chuki iliyopandwa kwa Wakenya na hutumbuka kila msimu wa kura na kuzua mizozo ya kikabila.

## 5.2 Taswira

Taswira ni dhana ambayo hutumiwa kuelezea neno, kirai au maelezo ambayo yanaunda picha fulani katika akili ya msomaji. Aidha, taswira zinaweza kuwa za kimaelezo au za ki-ishara. (Wamitila, 2003). Waandishi wa riwaya teule wametumia taswira kwa namna mbalimbali ili kudhihirisha athari za mizozo ya ardhi. Kwa mfano:

> … "wakati umeisha", alifika Mzee Baya aliyetumiwa kunyonga wafungwa. Alimtayarisha Mwita kwa kumvalisha nguo nyeupe na kumshauri aombe dua kama alitaka**. Dakika thelathini zilipita mara, wakasikia king`ora kikilia kwa huzuni…** king`ora kililia mara tatu ishara ya kwamba **Mwita alikuwa amenyongwa tayari**. mama yake alipewa nguo zake akaondoka katika gereza la Raka. (*Kovu Moyoni*, uk 132)

kifungu kilichonukuliwa kinadhihirisha taswira ya hali ilivyokuwa katika jamii wakati wa mizozo ya ardhi. Katika *Kovu Moyoni,* Habwe ameangazia tukio la kuhuzunisha ambapo Mwita mwanawe Boke anahukumiwa kunyongwa kwa kushukiwa kwamba alikuwa mwanachama wa kikundi cha Jeshi la vijana. Juhudi za Boke za kumtetea hazikufua dafu kwa sababu hatimaye walimnyonga. Baadaye ndipo inapogunduliwa kuwa waliyemnyonga sio Mwita aliyekuwa mwanachama wa Jeshi la Vijana. Habwe anatupa picha ya udhaifu wa viongozi na utawala kwa jumla ambapo wananchi wengi uhukumiwa na kuteswa bila hatia iwapo uchunguzi mwafaka hautafanyika. Walibora naye anadhihirisha athari za mizozo ya ardhi kupitia dondoo hili:

> … nilifuta ukungu uliotuama kwenye kioo cha dirisha la gari, na kutazama nje vizuri. Katika upeo wa macho yangu sikuona isimu ya mtu. Kumejiinamia jii. **Mabaki ya nyumba zilizoteketezwa moto ndiyo mandhari yaliyolaki macho yangu. Kuta zilizogeuka nyeusi kwa masizi, zilisimama wima bila paa kama viwiliwili vya binadamu visivyokuwa na vichwa. Baadhi ya mitambaapanya ilitema moshi mweusi** uliojipetapeta kwenye anga ya asubuhi na kutangamana na ukungu uliotanda kila pembe. (*Kufa Kuzikana*, uk 93, msisitizo wangu)

Katika *Kufa Kuzikana,* Walibora anachora picha kamili ya athari za mizozo ya kikabila Baraki Wilayani Korosho kupitia mhusika Akida. Anashuhudia jinsi ambavyo nyumba za watu zilichomwa na kwamba hakukuwa na dalili za mtu yeyote kuwa anaishi mahali pale kwa kuwa ama waliuawa au wakakimbilia usalama wao. Kwa hivyo, dondoo hilo linatupa taswira ya kiwango cha uharibifu uliotekelezwa nchini Kenya wakati wa mizozo ya kikabila baada ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka wa 1992 na pia 2007 hadi 2008 katika eneo la Bonde la Ufa, ambapo nyumba zilichomwa na Wakikuyu wakatimuliwa kutoka maeneo hayo.

### 5.3 Kinaya

Mbinu ya kinaya hutumiwa na waandishi kusawiri kinyume cha uhalisia wa mambo. Aidha, ni onyesho la kinyume cha matarajio kuhusu mkondo ambao matukio yanapaswa kuchukua. (Wamitila, 2003). Waandishi wa riwaya za *Kovu Moyoni* na *Kufa Kuzikana* wametumia kinaya kwa namna mbalimbali ili kudhihirisha athari za mizozo ya ardhi. Wanasema:

> "Haki, Bwana mkubwa. Mimi hivi nafukuzwa katika shamba langu. Mume wangu ameuawa. Mwanangu, Mwita alishikwa na Jeshi la Vijana. Alipokuwa akitoroka alishikwa na askari wa taifa. Mimi mwenyewe nimenajisiwa mara tatu. Mara mbili na magenge. Na mara nyingine na nyinyi wenyewe*;* **nyinyi mliopewa jukumu la kunilinda dhidi ya uhasama kama huo.***"* Boke alisema maneno yake akavuta pumzi… (*Kovu Moyoni*, uk 85, msisitizo wangu)
>
> Nilimkuta kwake amekaa mlangoni kashika tama na kununa. Kovu lake kipajini limechanganyika na mapeto na kumharibu sura kuliko wakati wowote mwingine…**mwuaji kapewa kazi ya kulinda uhai wa watu**," alisema. "Unamaanisha nini?" "we` hujasikia Mbunge wa Korosho Mabende kapewa wadhifa wa waziri wa usalama wa ndani." Nilikuwa sina mwao na hilo. "Mabende!" nilimaka. (*Kufa Kuzikana,* uk 162-163, msisitizo wangu)

Katika *Kovu Moyoni*, Boke anachukua hatua ya kutafuta haki yake ambapo anafunga safari kuelekea katika kituo cha polisi. Anamweleza mkuu wa polisi kuhusu masaibu yake. Alimweleza jinsi ambavyo alikuwa anafukuzwa katika shamba lake, mume wake akauawa, mtoto wake Mwita alikuwa ameshikwa na Jeshi la Vijana na alipokuwa akitoroka akashikwa na askari wa taifa. Vilevile, alieleza ya kwamba yeye mwenyewe alinajisiwa mara tatu, mara mbili na magenge na mara nyingine na askari wa taifa. Katika *Kufa Kuzikana*, Akida anampata Jerumani akiwa amenuna kuliko kawaida kwa sababu alikuwa amepata habari kuwa Mbunge wa Korosho Mabende alikuwa amapewa wadhifa wa Waziri wa usalama wa ndani. Jerumani anashangaa jinsi ambavyo mwuaji anapewa kazi ya kulinda uhai wa watu. Hii ni kwa sababu Mabende alidhaniwa kuwa mmoja wa waanzilishi wa mizozo wilayani Korosho. Kwa hivyo, ni kinaya kwamba askari wa taifa ambao wanapaswa kumlinda Boke ndio wanaomnajisi.

Vilevile, inakuwa kinaya kwamba mbunge Mabende anaongoza mashambulizi licha ya kuwa ndiye anapaswa kuleta amani Wilayani Korosho. Inadhihirika kuwa wasanii wa riwaya teule wanawakejeli viongozi kama wanaoangaziwa ambao husaliti wananchi wanaoongoza kwa kutenda kinyume na matarajio. Gagnon (2008) alitambua ya kwamba wakati wa mizozo ya ardhi Wilayani mlima Elgon mwaka wa 2005, wanajeshi wa taifa la Kenya walitumwa huko ili kuleta hali ya usalama. Badala yake waliwadhulumu wenyeji wa eneo hilo kupitia mauaji na pia unajisi. Hivyo, ni wajibu wa Serikali kuhakikisha kwamba polisi wamewajibika katika kazi yao.

Kadhalika, kunahitajika mageuzi katika idara ya polisi kwa haraka kwa kutambua kuwa kikosi hicho ni nguzo kuu katika mchakato wa kusuluhisha mizozo katika jamii na pia kurejesha amani nchini. Kinaya pia kinajitokeza kupitia kifo cha Meja-K. Hii inadhihirika kupitia mfano ufuatao:

> Kitendawili cha maisha kikajiri. ***Shimo alilotupa nafsi za watu akatupwa yeye pia. Mashamba aliyopigania akayaacha na wengine.*** Ukuni ukaungua badala ya mpishi. Mpishi akabaki anapika na kustarehe lakini ukuni ukachomeka na kuwa kaa. (*Kovu Moyoni*, uk 121, msisitizo wangu)

Meja-K alikuwa kiongozi wa Jeshi la vijana. Aidha, aliaminika kuwa na uwezo mkubwa na mamlaka kwani ndiye aliyesababisha mauaji ya halaiki Rama. Ndiposa inakuwa kinyume na matarajio ya watu anapopigwa risasi na watu wa kikundi cha jeshi la taifa. Vilevile, anatupwa katika shimo kama alivyotupa nafsi za watu wengi. Kwa hivyo, wananchi wanapaswa kuuasi ukabila na uchochezi wa wanasiasa ambao ni chanzo cha mizozo ya ardhi kwa kutambua kuwa mizozo hiyo ni chanzo cha umaskini uliokithiri katika mataifa mengi barani Afrika.

## 5.4 Mbinu Rejeshi

Hii ni mbinu anayoitumia mwandishi kuyaelezea matukio yaliyotokea wakati wa nyuma ya wakati wa hadithi. (Wamitila, 2003). Waandishi wa riwaya teule wamerejelea matukio ya hapo awali kupitia wahusika katika kazi zao ili kudhihirisha athari za mizozo ya ardhi. Haya yanadhibitika kupitia vifungu vifuatavyo:

> … hapo Boke aliposimama **alikumbuka mashambulizi yaliyohusu mashamba yalivyotokea katika miaka ya nyuma hapo Ram*a*.** Mashambulizi hayo yalisababisha kuunguzwa kwa sehemu nzima ya Rama huku wageni wakifukuzwa kama swara. Alikumbuka jinsi jirani yake, Emoro, alivyofukuzwa akaingia ndani ya shamba la miwa. Watesi wake walimfuata na kumchomea humo shambani. Hadi hivi leo Boke hukumbuka sauti ya Emoro ikiomba msaada wa kuokolewa. (*Kovu Moyoni*, uk 2)
>
> …Vita vilikuwa vimekwisha. Tulikwenda na babangu. **Sitayasahau mambo tuliyoyaona. Marundo na marundo ya maiti**. **Haidhuru tuliwatambua watu wa aila yetu.** Tingatinga ilitumika kuchimba shimo kubwa na kuzifukia maiti hizo pamoja. Nilishindwa kula kwa siku nyingi halafu. (*Kufa Kuzikana*, uk 197, msisitizo wangu)

Kupitia dondoo za hapo juu, waandishi wa riwaya teule wamerejelea matukio ya hapo awali ili kufafanua athari za mizozo ya ardhi. Katika *Kovu Moyoni*, Boke anayarejelea mashambulizi ya awali ambapo anakumbuka jinsi Jirani yake Emoro alitimuliwa kutoka kwa kishamba chake alichokinunua. Aidha, anakumbuka jinsi ambavyo watesi wa Emoro walivyomfuata alipokimbia na kumchomea katika shamba la miwa alikojificha. Kupitia mbinu rejeshi hii, inadhibitika kuwa mizozo ya ardhi ilianza kitambo ambayo hulipuka mara kwa mara kwani suluhisho la kudumu

halijapatikan. Isitoshe, katika *Kufa Kuzikana* Walibora anadhihirisha kiwango cha uharibifu na maovu yaliyotokana na mizozo ya kikabila. Mhusika Tim anamweleza Akida jinsi ambavyo mama na ndugu zake waliuawa. Vilevile, walishuhudia maiti za watu wengi ambao waliwajua walipokuwa hai. Kupitia mbinu rejeshi hii, inafahamika ya kwamba mizozo ya ardhi husababisha madhara mengi pakiwemo nyumba kuchomwa na mauaji ya watu wengi wasiokuwa na hatia. Isitoshe, mbinu rejeshi inayoangazia athari za mizozo ya ardhi inajitokeza katika kifungu kifuatacho,

> Kwa kweli Nifreda alikubali baba yake alikuwa jamali wa sura. Maulana alimtunukia sura nzuri na moyo mzuri. Hakujua kuchukia au kuteta. **Kumbukizi ya siku ile waliyovamiwa na Jeshi la Vijana ilimjia tena Nifreda.** Nifreda alijaribu kujizuia kufikiri hata kwa kutaka kuimba wimbo ambao haukutoka. (*Kovu Moyoni*, uk 47, msisitizo wangu)

Katika mfano uliodondolewa, Nifreda mwanawe Chifu Ngata anakumbuka siku ambapo walishambuliwa kwao nyumbani na Jeshi la Vijana ambapo baba yake alidungwa visu mwili mzima huku familia yake ikishuhudia. Licha ya kuwaomba msamaha, waliishia kumkata ulimi kinywani na kisha baadaye kumwua. Hatimaye Jeshi hilo liliwafanyia mabinti zake vitendo vya janaa.

Mifano ya Mbinu rejeshi iliyorejelewa katika vifungu vya hapo juu inamulika athari za mizozo ya ardhi kama vile mauaji, mali kuharibiwa na unajisi miongoni mwa madhara mengine. Kwa mujibu wa Njogu na wenziwe (2015), kushamiri kwa migogoro ya ardhi kumekuwa kukisababisha vifo, ulemavu, ukimbizi na pia kudumaa kwa uchumi kwa wananchi. Aidha, wakulima wamekuwa wakishindwa kuzalisha mazao, wafugaji mifugo yao kujeruhiwa na pia wawekezaji mali zao kuharibiwa. Kwa hivyo, ni muhimu viongozi watumie nafasi walizonazo katika kusaidia kutatua changamoto ya migogoro ya ardhi ili kuwezesha wananchi kuweza kuishi kwa amani na utulivu kwa ajili ya manufaa ya vizazi vya sasa na vijavyo vya taifa.

### 5.5 Sitiari

Hii ni mbinu ya kiulinganishi lakini ulinganishi huo haujitokezi waziwazi. Sitiari huhusisha vitu viwili ambavyo ni tofauti kitabia na kimaumbile. Katika msingi huu wasanii wa riwaya teule wametumia sitiari mbalimbali kama inavyodhihirika katika mifano ifuatayo:

> `…mkimbizi huyo angeishi vipi baada ya kufanyiwa dhuluma na huyo Chifu Senge? Aliuza shamba la nyumbani ili kuhamia Rama lakini kumbe anaingia kwenye **pango la nyoka. Moto wa Jehanamu** ulimuunguza, akajuta. Leo ndio sababu chifu Senge anapikia jiko si lake. Analala kitanda kisicho chake.

> Anasikiliza na kutazama televisheni isiyo yake. Lakini ana furaha. Anajipenda**.** (*Kovu Moyoni*, uk 32, msisitizo wangu)

Katika *Kovu Moyoni,* Habwe anarejelea tukio ambapo mkimbizi aliyeuza shamba lake la nyumbani na kuhamia Rama alivyonyang`anywa nyumba yake nzuri ya ghorofa na Chifu Senge. Chifu aliingia akarithi kila kitu, mifugo, samani na vyombo. Hata na shamba kubwa la ngano la huyo mkimbizi akarithi. Akichangia kuhusu Nadharia ya Baadaukoloni, Wamitila (2003) anatambua kuwa ingawa nchi za Asia, Afrika na Amerika ya Kilatini zina uhuru wa kisiasa bado zinatawaliwa na kutegemea nchi za Kizungu. Hii ni kwa sababu viongozi walioshika hatamu za utawala baada ya kuondoka kwa Wakoloni wakongwe waliendeleza uongozi wa kiimla na kuwanyanyasa wananchi wenzao. Bado kuna tamaa ambapo watu wanataka kujinufaisha kibinafsi na kuwabagua wenzao kwa misingi mbalimbali pakiwemo suala la umiliki wa ardhi. Hii ndio maana Habwe anatumia istiari ya `pango la nyoka`kumaanisha mahali palipokuwa na hatari hasa kwa kuwadhulumu watu. Walibora katika *Kufa Kuzikana* anasema:

> … "naam. Ati aje amzike babake kwetu Baraki? Wakanju wana haki gani kumzika mtu Baraki. **Wao ni magugu sharti wang`olewe, zao linawiri**." Upumbavu wake umemtokea puani. Pengine hajafa, nimpige mkuki kichwani sio? (*Kufa Kuzikana*, uk 106, msisitizo wangu)

Kifungu cha hapo juu kinaangazia tukio ambapo Wakanju wanarejelewa kuwa `magugu`kumaanisha ya kwamba ni mimea isiyohitajika katika shamba na hivyo huzuia mimea iliyopandwa kunawiri vizuri, ndiposa Wakanju walipaswa kung`olewa ili shamba liweze kunawiri. Hii ni kwa sababu licha ya kuwa waliishi katika mashamba waliyonunua wenyewe bado walionekana kama `wageni`.

Mfano mwingine wa matumizi ya istiari kudhihirisha athari za mizozo ya ardhi unajitokeza kupitia mfano ufuatao:

> … akaona jinsi jeshi lilivyofika. Lilifika kwa wingi kama siafu washambulizi. Nyuso zao zilijaa hasira. Mioyo yao nayo ilikuwa na ghamidha *ya* **kung`oa gugu nalo gugu hilo lilikuwa Chifu Ngata**. Ngata alikuwa nyumbani siku hiyo na mkewe, Milka na wanawe. Alipomwona huyo Meja-K aliyekiongoza kikosi cha vijana alikuwa amemtishia chifu aliyepinga oparesheni yao ya kutafuta usawa na haki Rama. (*Kovu Moyoni*, uk 47)

Katika kifungu cha hapo juu, Habwe anadhihirisha matumizi ya istiari kupitia neno `gugu` ambalo limetumiwa kumrejelea Chifu Ngata ambaye alikuwa mpenda haki na hivyo alipinga oparesheni ya Jeshi la Vijana. Hii ndio maana jeshi hili lilimuona kama

‘gugu’ kwa maana ya pingamizi au kikwazo katika kufaulu kwao. Kwa hivyo, licha ya kuwa wasanii wa riwaya teule wameeleza kwa mitazamo tofauti, wamedhihirisha matumizi ya istiari ili kuonyesha athari za mizozo ya ardhi kama vile chuki inayotokana na ukabila ambayo matokeo yake ni mauaji, unajisi, ukimbizi na uharibivu wa mali.

### 5.6 Tashihisi

Wamitila (2003) anaeleza kuwa tashihisi ni tamathali ya usemi ambapo vitu visivyokuwa hai au na uhai huwasilishwa au kusawiriwa kwa namna ilivyo sawa na binadamu ya kuweza kufikiri na kuhisi. Waandishi wa riwaya za *Kovu Moyoni* na *Kufa Kuzikana* wametumia tashihisi ili kuibua athari za mizozo ya ardhi. Kwa mfano:

> … Ilikuwa rabsha isiyokuwa na mwombezi. **Kifo kilipanua kinywa chake tayari kumeza mtu. Kwani kilimeza wangapi?** Kwa nje ni mvua ya radi iliyothubutu kushuka chini kwa kelele. Upepo mkali ulivuma kwa nje kana kwamba uligombana na hali ile. Nyumba ya Ngata iliyumbishwa kwa hilo wimbi la upepo na kulalamika… (*Kovu Moyoni*, uk 49, msisitizo wangu)

> … Tulipofika Nduchi tulielekea kwenye nyumba ya maiti ya Hospitali ya Wilaya. Niliyaona mazingira yaleyale ya kuogofya kama niliyoyaona katika nyumba ya maiti Jijini Tandika. **Majokofu yamekula yameshiba maiti, yakatapika wengine sakafuni na kuteuka mnuko mbaya**, **mbaya sana**. Mtumishi mmoja wa hapo, sugu wa mazingira hayo alikuwa ameuchapa na kuichangamkia kazi yake. (*Kufa Kuzikana*, uk 88, msisitizo wangu)

Katika dondoo hizo, waandishi wa riwaya teule wamerejelea visa ambapo mbinu ya tashihisi imetumika kudhihirisha athari za mizozo ya ardhi. Katika *Kovu Moyoni,* `kifo`kimedhihirishwa kuwa na uwezo mkubwa kama vile wa kupanua kinywa chake na kumeza watu. Huu ni wakati ambapo kundi la ‘Jeshi la vijana’ lilimvamia Chifu Ngata ambaye alipinga oparesheni ya kundi hilo katika `kutafuta usawa na haki katika Rama. Alifanyiwa kila aina ya dhuluma na hatimaye akauawa huku mke na binti zake wakinajisiwa hadharani. Katika *Kufa Kuzikana*, majokofu katika nyumba ya kuhifadhia maiti yapewa sifa ya binadamu, kwa mfano, mhusika Akida anaeleza namna ambavyo majokofu yalikuwa yamekula yakashiba maiti, na kutapika wengine sakafuni. Tashihisi hii inatupa picha ya namna ambavyo vifo vya watu wengi vilitekelezwa Wilayani Korosho. Kwa hivyo kupitia mbinu ya Tashihisi, taswira ya athari za mizozo ya ardhi inajitokeza hasa kupitia vifo.

### 5.7 Tashbihi

Hii ni tamathali ya usemi ambapo vitu viwili hulinganishwa kwa njia waziwazi. Aidha, Tashbihi hutambulishwa na matumizi ya viungo kama, mfano wa, mithili ya, ja, kama vile, sawa na kadhalika. Tashbihi mbalimbali zimetumiwa na waandishi wa riwaya teule kama inavyodhihirika katika mifano ifuatayo:

> …mwita, akiwa na mama yake, walisikiliza zogo la hapo mlimani. Waliuona moto mkubwa ukiteketeza nyumba huku watu wakiendelea kulia. Vilio sasa vilishuka bondeni kwa huzuni. **Vilikata maini, vilichoma mioyo kama vijinga vya moto. Eneo zima hili liligeuka na kuwa kama Jehanamu.** Lilimtia Boke tumbo joto. (*Kovu Moyoni*, uk 6)
>
> … “na usimwone kalewa ukafikiri asema uongo”. aliongeza mgonjwa huyo aliyekuwa anahema na kukohoa kama aliyeugua pumu. “**Tumeuenzi ukabila hapa Kiwachema kama mboni ya jicho** na kupokezana uovu huo kizazi baada ya kizazi kama hirizi.” (*Kufa Kuzikana,* uk 75, msisitizo wangu)

Katika *Kovu Moyoni*, \`Vijinga vya moto\` na \`Jehanamu\` ni kauli zilizotumika ili kueleza hali ilivyokuwa Rama. Mwandishi Habwe analinganisha vilio vya watu huko mlimani na Vijinga vya moto kwani watu wengi waliumia sana kutokana na mashambulizi waliyoyapitia. Aidha, katika *Kufa Kuzikana*, mgonjwa aliyelazwa katika hospitali ya Rufaa ya Tandika anawaeleza Akida na rafikiye Tim kwamba watu wa Kiwachema waliuenzi ukabila kama \`mboni ya macho\` kumaanisha kuwa ni jambo wanaloishi nalo na ni vigumu kuliacha, ndiposa anaendelea kusema kuwa ukabila ni uovu ambao umepokezanwa kizazi baada ya kingine.

Kupitia mifano ya tashbihi zilizodondolewa katika riwaya teule, inadhihirika kwamba suala la ardhi kwa misingi ya kikabila ni uovu ambao hupokezanwa vizazi baada ya vizazi hasa nchini Kenya, jambo ambalo linashadidia sababu za kuwepo kwa mizozo ya ardhi ya mara kwa mara katika vipindi tofauti na maeneo mbalimbali nchini. Kwa mujibu wa Samson (2012), ukabila unasababishwa na ubinafsi wa watu katika kutekeleza majukumu ya maendeleo katika jamii ambayo ina watu wenye mtazamo, itikadi, dini, lugha na tamaduni tofauti. Aidha, tofauti hizi husababisha jamii moja kujitenga na nyingine hivyo kuibua matabaka ya watu ambao kila mmoja anajiona ni bora kuliko mwenzake. Kwa hivyo, migogoro isiyoisha baina ya pande hasimu huzuka na hivyo kusababisha vita visivyoisha ambavyo huzorotesha juhudi za kujiletea maendeleo.

Kutokana na maelezo hayo, ni wazi kwamba chanzo cha migogoro na matatizo mengi Afrika leo ni suala la ardhi linaloibuka kwa misingi ya kikabila na kusababisha vita visivyoisha, njaa, umaskini na uharibifu wa rasilimali muhimu kwa maendeleo. Kwa hivyo, wananchi katika taifa wanapaswa kupinga fikra finyu za watu wachache ambao wanakuza ukabila hasa kwa maslahi ya kisiasa ili kudhoofisha juhudi za mabadiliko katika jamii na mshikamano wa watu nchini. Kadhalika, ni wajibu wa jamii hasa viongozi wa nchi kutatua malalamiko ya watu na kuhakikisha kuwa wanapata mahitaji yao bila upendeleo.

### 5.8 Barua

Wasanii wa riwaya teule wametumia mbinu ya barua kuwasilisha athari za mizozo ya ardhi kama inavyojitokeza katika dondoo zifuatazo:

> … ninaandika barua hii nikiwa na furaha tele moyoni, **wakati wa mkesha huu wa kunyongwa kwangu**. Lengo la kukuandikia barua hii ni kukushukuru kwa wema na takrima yako kwetu kama wanao. Ningependa kukusihi usiendelee kulia kwa sababu yangu mimi. Mimi nina raha ya kuondoka katika **nchi ambayo licha ya kuzima azma yangu ya kuwa mhandisi, nimeisamehe kabisa.** Hii ni kwa sababu ni nchi ambayo **haina mizani ya kupima wema na ubaya barabara**; **licha ya kudai kuwa ina usalama, ina amani na haki; haina**. Hata ninapotazamia kunyongwa kesho bado nauliza kosa langu ni lipi? Na ni nani niliyemkosea? Na nilimkosea vipi? (*Kovu Moyoni*, uk 131-132)
>
> …**kuuawa kikatili kwa muke na wadodo wangu wasio na battia** kumeniattua moyo. Mie **nimewaua Wakanju wengi vittani**. Nilikuwa mstari wa mbele katika kikosi cha Wakorosho. Ila sasa nashindwa kuhimili majutto **ya kukuuwa Ndugu yangu Sululu, mutu asie battia**. Samaani Sululu. Zabuon Mapisi. (*Kufa Kuzikana*, uk 198, msisitizo wangu)

Katika mifano ya hapo juu, Habwe katika *Kovu Moyoni* anaangazia barua ya mhusika Mwita kwa mamake Boke. Hii ni baada ya kuhukumiwa kunyongwa kwa madai kuwa alikuwa mwanachama wa Jeshi la Vijana. Katika barua hiyo, inadhihirika kuwa azma ya Mwita ya kuwa mhandisi ilizimwa. Vilevile, inadhihirika kuwa nchi ya Kiwachema ni nchi ambayo haina mizani ya kupima wema na ubaya barabara, na kuwa licha ya kudai kuwa nchi ina usalama, amani na haki, haina. Kwa hivyo, kupitia barua hiyo, nchi ya Kiwachema inasawiriwa kuwa yenye kila aina ya uovu na maonevu pakiwemo unafiki, unyang`anyi na ubaradhuli. Isitoshe, katika *Kufa Kuzikana,* Walibora

anaangazia athari za mizozo ya ardhi kupitia barua ya Mzee Zablon baada ya kujitia kitanzi. Katika barua hiyo, athari za mizozo ya ardhi kama vile kuuawa kwa mke na watoto wake kikatili kunajitokeza wazi. Aidha, kujinyonga kwa Mzee Zablon kulitokana na kushindwa kuhimili majuto ya kumuua Sululu babake Akida, mtu asiye hatia kama anavyoeleza katika barua hiyo.

Kwa mujibu wa Maina (2014), ghasia za baada ya uchaguzi wa Kenya mwaka 2007-2008 zilidhihirisha jinsi ambavyo ukabila unaweza katika muda mfupi kuitumbukiza nchi katika vita vya wenyewe kwa wenyewe. Wanasiasa mara kwa mara hutumia makabila yao kuendeleza siasa za ubinafsi zisizo na msingi, na kwa sababu ya hilo, ukabila ni adui ya kuimarika kwa demokrasia. Kadhalika, ukabila umechangia pakubwa kuwepo mizozo ya ardhi na vita vya wenyewe kwa wenyewe barani Afrika. Hata hivyo, kwa kuwa demokrasia inatoa nafasi kwa maendeleo endelevu na mafanikio, siasa za kikabila lazima zikomeshwe na pahala pake kuchukuliwa na taasisi za kisasa zenye kushinikiza demokrasia.

### 5.9 Hitimisho

Sura hii imeangazia jinsi waandishi wa riwaya za *Kovu Moyoni* na *Kufa Kuzikana* wametumia fani za lugha kufafanua athari za mizozo ya ardhi. Utafiti huu umechunguza fani za lugha ambazo waandishi wa riwaya teule wametumia ili kuibua athari za mizozo ya ardhi. Hii ni kwa sababu katika kazi yoyote ya fasihi wasanii hutumia mbinu mbalimbali ili kuupitisha ujumbe ambao walikusudia kuupitisha na kwa namna walivyokusudia. Hivyo, imebainika kuwa wasanii wa riwaya za *Kovu Moyoni* na *Kufa Kuzikana* wametumia fani mbalimbali za lugha ili kuibua athari za mizozo ya ardhi. Fani za lugha zilizohakikiwa ni pamoja na jazanda, kinaya, taswira, barua, mbinu rejeshi, istiari, tashbihi na tashihisi.

## SURA YA SITA

## MCHANGO WA ASASI MBALIMBALI KATIKA KUSULUHISHA MATATIZO YA ARDHI KATIKA RIWAYA ZA *KOVU MOYONI* NA *KUFA KUZIKANA*

### 6.0 Utangulizi

Katika utafiti huu, madhumuni ya tatu yalikuwa kutathmini mchango wa asasi mbalimbali katika kusuluhisha matatizo ya ardhi kama ilivyosawiriwa katika *Kufa Kuzikana* na *Kovu Moyoni.* Waandishi wa riwaya za *Kufa Kuzikana* na *Kovu Moyoni* wameangazia mchango wa asasi mbalimbali katika kusuluhisha matatizo ya ardhi. Asasi hizo ni pamoja na serikali ya taifa, mashirika yasiyo ya serikali, vyombo vya habari, dini, viongozi wa kisiasa na halmashauri za kushughulikia masuala ya ardhi.

### 6.1 Mchango wa Serikali

Kwa mujibu wa Nyukuri (1997), idhibati ilionyesha kuwa serikali ya Kenya ama ilifanya juhudi kidogo au haikufanya chochote kusaidia waathiriwa wa mizozo ya baada ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 1992 ambao walishindwa kurejea katika ardhi yao ya zamani. Jambo lingine lililodhihirisha mwitikio hasi wa serikali kuhusu mizozo ya ardhi kwa sababu zao za kisiasa ilikuwa kushambulia na kuzuia vyombo vya faraja na watu waliojaribu kusaidia waathiriwa. Hata hivyo, wasanii wa riwaya teule wamesawiri serikali ya nchi yoyote ile kuwa na mchango mkubwa katika kusuluhisha mizozo ya ardhi kupitia njia mbalimbali. Jambo hili linashadidiwa na dondoo lifuatalo:

> …**Jeshi la taifa lilipotia guu lake Rama uhai ulirudi**. Wafanyabiashara walianza kurudi masokoni. Watu waliokuwa kwa jamaa zao wakarudi nyumbani. Msimu wa upanzi uliokuwa umechelewa ulipigwa jeki. Matrekta yalilima katika mashamba. Nayo kelele ya watu wa kuswaga ng`ombe wa kulima ikasikika katika baadhi ya mashamba… (*Kovu Moyoni*, uk 118, msisitizo wangu)

Kutokana na kifungu kilichodondolewa katika *Kovu Moyoni*, Habwe amedhihirisha juhudi za Serikali katika kusuluhisha mizozo ya ardhi kwa namna mbalimbali. Kwa mfano, baada ya mashambulizi kuzidi Rama, Jeshi la taifa linaanza oparesheni ya kudhibiti mashambulizi hayo. Amani inarejea Rama ambapo pia shughuli za watu za kawaida zinarejea kama vile watoto kurudi shuleni, hospitali kufunguliwa tena, wakulima kwenda shambani na kadhalika.

Katika *Kufa Kuzikana*, Walibora anasema:

> Idhaa ya Sauti ya Kiwachema ilitangaza kuwa **serikali ya Kiwachema imebuni Tume ya Haki na Maridhiano** kuhusiana na vita vya kikabila Wilayani Korosho. Viongozi wa kidini waliteuliwa kuwa wanachama wa tume hiyo**.** (*Kufa Kuzikana*, uk 220, msisitizo wangu)

Katika *Kufa Kuzikana*, Walibora anadhihirisha juhudi za Serikali za kusuluhisha mizozo. Serikali ya Kiwachema inabuni Tume ya Haki na Maridhiano kuhusiana na vita vya kikabila Wilayani Korosho. Isitoshe, juhudi za serikali ya nchi zinadhihirika kupitia mfano ufuatao:

> … kulikuwa na fununu kwamba **Jeshi la Taifa lilimtafuta ili kumtia nguvuni na kumfungulia mashtaka. Mawakala wake kama vile Mustafa** walikuwa wametiwa nguvuni wakingojea siku za kesi zao kufanywa…. familia ya Mwamba ilishikwa na wasiwasi iliposikia anatafutwa na polisi kutiwa nguvuni kwa ajili ya maasi ya Rama… (*Kovu Moyoni*, uk 137, msisitizo wangu)

Anayerejelewa katika kifungu kilichodondolewa ni Mwamba aliyekuwa mwanasiasa mwenye ushawishi mkubwa serikalini. Aidha, ndiye aliyekuwa mwanzilishi na mfadhili mkuu wa kundi la `Jeshi la Vijana` ambalo lilitekeleza mashambulizi ya kila aina huko Rama. Kwa mujibu wa vifungu vilivyonukuliwa kutoka katika riwaya teule, Juhudi za serikali katika kutatua mizozo ya ardhi zinadhihirika kwa namna mbalimbali. Kwanza, ni kupitia askari ambao wanaenda katika maeneo yenye mizozo ya ardhi ili kuidhibiti hali hiyo na kurejesha amani. Pili, kupitia asasi za serikali kama vile polisi ambapo watu wote wanaoshukiwa kuwa wachochezi wa mizozo ya ardhi wanatiwa mbaroni na kufunguliwa mashtaka. Jambo linalodhihirika katika *Kovu Moyoni* wakati Mwamba anapotiwa mbaroni pamoja na mawakala wake kama vile Mustafa. Vilevile, Sokomo mwanawe aliyekuwa katika mipangilio ya mashambulizi anatiwa mbaroni. Kadhalika, juhudi za Serikali ya nchi zinadhihirika kupitia uundaji wa tume za kushughulikia masuala ya ardhi kama vile Tume ya Haki na Maridhiano.

Nchini Kenya, Tume ya Kitaifa ya Ardhi (NLC) ilitegemewa kutoa majibu kuhusiana na maswali mengi kuhusu suala sugu la matatizo ya ardhi na masuala mengine ambayo kwa muda mrefu yamevutia hisia ya wengi baada ya kuingizwa siasa. Baadhi ya majukumu ya NLC ni kusimamia ardhi ya umma kwa niaba ya serikali kuu na zile za kaunti, kuanzisha uchunguzi kuhusu dhuluma za kuhistoria kuhusiana na ardhi na kutoa mapendekezo kuhusu njia za kuzikomesha na kupendekeza ada zitakazotozwa ardhi. Zaidi ya hayo, kutokana na mizozo ya ardhi kuzidi kuongezeka kila kukicha, ni vyema

serikali ya nchi kumulika ufisadi kwenye masuala yanayohusiana na umiliki na ugavi wa ardhi kwani yana uzito wa kipekee katika maisha ya watu wote pamoja na Taifa kwa jumla.  Kwa hivyo, inadhihirika kuwa serikali ya nchi inaweza kusaidia katika kusuluhisha mizozo ya ardhi iwapo itawajibika ipasavyo. Hata hivyo, wasanii wa riwaya za *Kovu Moyoni* na *Kufa Kuzikana* wanakashifu serikali na taasisi nyinginezo zinazohusika katika kushughulikia matatizo ya kijamii pakiwemo mizozo ya ardhi kwa kushindwa kutatua matatizo hayo au kukosa kuwajibikia kazi yao. Kwa mfano katika *Kovu Moyoni*:

> … hapo ndipo akili zake zilipoanza kurudia kwenye ile sehemu ya baba yake ya shamba la bwanyenye. Walikuwa wameambiwa wangefidiwa pesa Fulani. Mama yake **alidai hizo pesa miaka na mikaka bila mafanikio.** Mama yake Meja-K, Bi. Kimaka, alikwenda kwa Chifu Ngata miaka nenda miaka rudi. Baadaye kwa afisa wa wilaya. Hatimaye katika halmashauri za mashamba. **Hapana aliyeelewa jambo alilokuwa akilisema.** Wahusika aliowafuata walijifanya kutoelewa kile ambacho alikuwa anakisema. (*Kovu Moyoni*, uk17, msisitizo wangu)

Kifungu kilichonukuliwa kinamrejelea mamake Meja-K aliyehangaika hapa na pale huku akitafuta haki kwa sababu ya shamba lake lililokuwa limenyakuliwa, lakini hakuweza kupata msaada wowote. Hali hii inasawiri taasisi zinazoshughulikia masuala ya ardhi kuwa na udhaifu. Kama wanavyotambua Arua na Eka (2000), mara kwa mara watu huteseka kwa sababu ya maamuzi mabaya ya serikali nchini, ambapo huduma nyingi za serikali huwa haziwafikii watu hasa kwa kukosa mpangilio mwafaka. Mizozo ya kikabila hutokea watu wanapokosa huduma hizi na pia maendeleo katika maeneo yao, aidha, Arua na Eka wanahoji kuwa kunapaswa kuwa na umoja miongoni mwa serikali ili kuweza kuhudumia wananchi. Kwa hivyo, inadhihirika kwamba serikali inayo nafasi nzuri katika kutatua mizozo katika jamii pakiwemo suala la ardhi. Vilevile, katika *Kovu Moyoni, Habwe* anaukashifu mfumo wa utawala ambao hauwezi kusaidia wananchi katika utatuzi wa masuala yanayohusiana na mizozo mbalimbali ya ardhi. Kifungu kifuatacho kinashadidia:

> Meja-K alikumbuka juhudi za babake za kusalimisha Shamba lake. Baba ***mzazi alipanda vilima akashuka mabondeni. Aliingia kila korti. Alibisha kila mlango husika wa serikali lakini hakufaulu kulisalimisha shamba lake.*** Kishamba kilichobaki hakikuweza kuhimili familia yao ya watoto saba. (*Kovu Moyoni*, uk 16, msisitizo wangu)

Katika kifungu hiki, inadhihirika kuwa babake Meja-K alinyang`anywa sehemu kubwa ya shamba lake ambapo Chifu Malonza alimweleza kuwa hakustahili kupata sehemu hiyo ya ardhi. Ikauziwa bwanyenye mmoja kutoka Dunga. Kadhalika, licha ya babake Meja-K Mzee Makoti kutia juhudi na kusafiri kila ofisi za serikali ili kulisalimisha shamba lake, hakufaulu. Kwa hivyo kupitia mfano huu, mwandishi anaweka wazi udhaifu uliopo katika taasisi na idara nyingi za serikali pakiwemo zile zinazoshughulikia suala la ardhi. Nazo ni kama vile Halmashauri ya mashamba na Tume ya Kitaifa ya Ardhi, ili ziweze kuboreshwa iwapo mizozo ya ardhi itaweza kusuluhishwa.

Vilevile, kama ilivyo katika Ruwaza ya Maono ya 2030 ya Kenya, ni muhimu serikali kufanya marekebisho makubwa katika kilimo ambapo njia mojawapo itakuwa kuwawezesha watu wote kuwa na nafasi sawa ya kumiliki ardhi. Aidha, serikali inaweza kusuluhisha mizozo ya ardhi kwa kuzitwaa hatimiliki zilizotolewa kinyume cha sheria pamoja na Wizara ya Ardhi kuzingatia kuhifadhi rekodi za ardhi kwa njia ya digitali. Vilevile, Wizara ya Ardhi inaweza kushirikiana na Tume ya Maadili na Kukabili ufisadi EACC kutathmini rekodi za wizara hiyo.

### 6.2 Nafasi ya Dini

Waandishi wa riwaya teule wamesawiri dini kama chombo muhimu katika kusuluhisha migogoro inayohusiana na suala la ardhi. Haya yanadhihirika kupitia matamshi ya baadhi ya wahusika katika kazi zao. Kwa mfano:

> "sijui, nyinyi ndio mjuao. Nyinyi ndio mliosoma," Boke alisema kidogo kwa dharau huku akiliwa na gegezi la hasira. Mwongera alikuwa ni mtu wa moyo mwema. **Alikuwa mcha Mungu na askari aliyependa kusimama upande wa haki.** Alipendwa sana na wengi hapo kituoni Mamboleo. Alimkaribisha Boke akae nyumbani kwake hadi atakaposaidiwa**.** Wema ulioje**!** Ni nadra kupata watu wema lakini na wachache! (*Kovu Moyoni*, uk 82, msisitizo wangu)

Katika *Kovu Moyoni*, askari Mwongera amesawiriwa kuwa na utu na aliyependa kusimama upande wa haki. Hii ni kwa sababu alikuwa mcha Mungu. Hii ndio maana anajitolea kumkaribisha Boke kwake nyumbani hadi wakati angepata usaidizi. Mwandishi anaonyesha ya kwamba sifa ya kuwa mcha Mungu inaweza kuleta amani katika taifa kwani watu wote watapendana wala hawatabaguana kwa misingi yoyote ile. Namna nyingine ya mchango wa dini inajitokeza kupitia mfano ufuatao:

> ... “Ndugu na dada mmepotea mkawa kama watu wa ulimwengu,” alifoka Kasisi John Jumapili moja. ***“kwa nini mnaruhusu ukabila kuingia kanisani.*** Kisa cha kumkataa mhubiri James Sanya kwa sababu ya ukabila kimetia doa kanisani. …**tuna tofauti gani na makanisa Wilayani Korosho yaliyoshindwa kuwapatanisha watu yakawaacha wakauana burebure***?* Maandiko yanasema; `Mungu si mwenye ubaguzi, bali katika kila taifa mtu ambaye humhofu na kutenda uadilifu akubalika kwake,”. (*Kufa Kuzikana*, uk 121, msisitizo wangu)

Katika *Kufa Kuzikana*, Kasisi John anafokea waumini kwa kuruhusu ukabila kuingia kanisani. Aidha, anakashifu makanisa Wilayani Korosho yaliyoshindwa kuwapatanisha watu yakawaacha wakauana burebure. Kwa mujibu wa dondoo hili, mwandishi anasawiri dini kuwa chombo muhimu katika kusuluhisha mizozo ya kikabila, ndiposa anadhihaki makanisa Wilayani Korosho yaliyoshindwa kutekeleza wajibu huo. Kwa mujibu wa Mworia na Ndiku (2012), wanajamii na pia dini wanao mchango mkubwa katika kusuluhisha mizozo ya ardhi. Kwa hivyo ni wazi kwamba suala la dini limeangaziwa na wasanii wa riwaya teule kama chombo muhimu katika kusuluhisha mizozo ya ardhi. Isitoshe, umuhimu wa dini unajitokeza kupitia mfano ufuatao:

> Chifu Ngata alizikwa baada ya siku mbili. Mazishi yake yalikuwa kama ya mtoto mchanga. Ni watu wachache waliojisabilia nyoyo zao na kuhudhuria mazishi hayo. Watu waliogopa kusema lolote baada ya kuonywa vikali na Jeshi la Vijana. Hata mahubiri yaliyotolewa siku hiyo yalikuwa mafupi. **Padre aliwaonya wanadamu na kuwatahadharisha na matukio ya siku za mwisho**. (*Kovu Moyoni*, uk 49, msisitizo wangu)

Katika mfano uliodondolewa, padre anahubiri katika mazishi ya chifu Ngata aliyeuawa na kundi la Jeshi la Vijana ambapo aliwaonya wanadamu dhidi ya matukio ya siku za mwisho. Kwa hivyo, Habwe katika *Kovu Moyoni* anaonyesha kuwa viongozi wa kidini wanayo nafasi muhimu katika kutahadharisha wanajamii dhidi ya matendo ambayo yanaweza kusababisha mizozo. Zaidi ya hayo, serikali inatambua umuhimu wa dini katika kusuluhisha mizozo ya ardhi kama inavyojitokeza katika mfano ufuatao:

> Idhaa ya Sauti ya Kiwachema ilitangaza kuwa serikali ya Kiwachema imebuni Tume ya Haki na Maridhiano kuhusiana na vita vya kikabila Wilayani Korosho. **Viongozi wa kidini waliteuliwa kuwa wanachama wa tume hiyo.** Tume hiyo ndiyo itakayofufua mamia waliouawa vitani Korosho kuanzia kwa mwalimu wangu Alex hadi kwa babangu Sululu? (*Kufa Kuzikana*, uk 220, msisitizo wangu)

Katika *Kufa Kuzikana,* baada ya mizozo Wilayani Korosho, serikali ya Kiwachema inabuni Tume ya Haki na Maridhiano ya kuchunguza mizozo hiyo ambapo miongoni mwa wanachama wa tume hiyo ni viongozi wa kidini.

Kutokana na vifungu vilivyodondolewa, nafasi ya dini katika kusuluhisha mizozo ya kijamii pakiwemo mizozo ya ardhi inajitokeza kwa namna mbalimbali. Kwa mfano, dini inatekeleza wajibu muhimu katika kuhimiza utu na upendo miongoni mwa wananchi pamoja na viongozi. Hii ndio maana Habwe katika *Kovu Moyoni* anamsawiri Askari Mwongera akiwa mcha Mungu na aliyesimama upande wa haki kila wakati, ndiposa akapendwa sana na watu. Vilevile, umuhimu wa dini unajitokeza kupitia mahubiri ya makasisi kanisani kama vile Kasisi John katika *Kufa Kuzikana* ambaye anashutumu na kukashifu vikali ukabila, na ubaguzi.

Isitoshe, Habwe katika *Kovu Moyoni* anaonyesha umuhimu wa dini katika kusuluhisha mizozo ya ardhi kupitia Padre anayewaonya na kuwatahadharisha wanadamu kuhusu matukio ya siku za mwisho. Kadhalika, inadhihirika kuwa viongozi wa kidini wanao mchango muhimu katika masuala ya kijamii kama vile mizozo ya ardhi kwa kushirikiana na serikali katika uundaji wa tume za kushughulikia masuala ya ardhi. Jambo hili linadhihirika katika *Kufa Kuzikana* ambapo serikali inaunda Tume ya Haki na Maridhiano ya kuchunguza mizozo ya kikabila Wilayani Korosho ambapo viongozi wa kidini wanakuwa miongoni mwa wanachama wake.

Nchini Kenya, mara kwa mara viongozi wa kidini wamekuwa wakitoa mahubiri ya kuhimiza amani wakati na baada ya uchaguzi mkuu katika maeneo mengi nchini. Kwa hivyo ni wazi kuwa waandishi wa riwaya za *Kufa Kuzikana* na *Kovu Moyoni* wamesawiri viongozi wa kidini kuwa na mchango muhimu katika kusuluhisha mizozo ya kijamii pakiwemo mizozo ya ardhi.

Hata hivyo, waandishi wa riwaya teule wanawakashifu viongozi wa kidini ambao hawajawajibika katika kazi yao, na badala yake huchangia katika kuzidisha mizozo ya ardhi. kwa mfano:

> … La kumnasibisha mbunge wetu Mabende na mauaji ya halaiki Korosho sikuliona la ajabu. Lakini kamwe sikuamini habari kwamba **Makasisi kama Kasisi John walifadhili mapigano**. Nililitilia shaka. Mtu wa Mungu? (*Kufa Kuzikana*, uk 162, msisitizo wangu)

Kupitia mfano uliodondolewa, kwa mujibu wa jarida ambalo Akida alikabidhiwa na Jerumani, Makasisi wengi wa mijini na pia vijijini walilaumiwa kwa mizozo Wilayani Korosho. Kwa mfano ilidaiwa kuwa Kasisi Njalala alifadhili mapigano hayo. Ndiposa Nyukuri (1997) anasema kuwa wakati wa mizozo ya baada ya uchaguzi mkuu wa mwaka 1992 nchini Kenya, iligunduliwa kuwa wakristu wengi hawakukemea mizozo hiyo huku baadhi yao wakitajwa na waliohojiwa kuwa wachochezi wa mizozo hiyo. Aidha, watu wengi waliohojiwa walihisi kuwa waumini wa kikristu walikuwa na athari ndogo sana kuhusu namna Wakenya walivyoishi, licha ya kuwa asilimia themanini ya watu nchini kuwa wakristu. Kwa hivyo, walichukuliwa kuwa wanafiki wasiotekeleza kile walichohubiri. Hivyo ni wazi kuwa waandishi wa riwaya teule wanawashutumu viongozi wa kidini ambao hawajawajibikia kazi yao ya kusuluhisha mizozo katika jamii.

### 6.3 Mashirika yasiyo ya Serikali

Mashirika yasiyo ya serikali yanaweza kuchangia katika kusuluhisha mizozo ya ardhi nchini. Wasanii wa riwaya teule wameangazia mchango wa mashirika hayo kama inavyodhihirika katika vifungu vifuatavyo:

> "Mungu ni mkubwa," Boke alisema kwa dhati akizuia machozi," "kama si Mungu hatungekuwa hai. Tumeishi na simba katika pango lake lakini bado tuko hai," Nifreda alisema. Ile hasira yake ilikuwa imeshuka. **Aliajiriwa kazi na Shirika la Chunga Ndugu Yako linalowasaidia watu kurudi nyumbani. Shirika hili limemsaidia kuyaendeleza na kuyamaliza tena masomo yake katika Chuo Kikuu cha Tandika**. "Nikusaidie vipi, mama," Nifreda alimuuliza Boke. Alipomkagua tena akashangaa. Boke alikuwa mwanamke mnene, mwekundu lakini leo amekonda kama ufito wa mwanzi. (*Kovu Moyoni*, uk 98, msisitizo wangu)

> … "Mimi n`tamshikilia," alisema. "Lo! Kila siku tukipita hapa lazima tupate wahasiriwa wanaohitaji kupelekwa hospitali." "Kwani mnapita mkienda wapi?" nikasaili. "**Huwa tunapeleka chakula cha msaada kwa kambi ya `wakimbizi` ya Mukutu. Sisi hufanya kazi na shirika la kutoa msaada, Action Men"**. Nikaingia garini sehemu ya nyuma iliyofunikwa turubai la kijivujivu. (*Kufa Kuzikana*, uk 108, msisitizo wangu)

Katika *Kovu Moyoni*, mhusika Nifreda ni miongoni mwa waathiriwa wa mizozo ya ardhi katika kijiji cha Siloko. Baada ya kupitia dhiki nyingi kutokana na vitendo vya unyama katika mashambulizi anaajiriwa na Shirika la Chunga Ndugu Yako ambalo liliwasaidia watu kurudi nyumbani baada ya hali ya utulivu kurejea. Vilevile, Shirika

hili linamsaidia Nifreda kurudi shuleni ambapo anakamilisha masomo yake ya Chuo Kikuu. Katika *Kufa Kuzikana*, Akida anapombeba Tom baada ya kushambuliwa na kundi la watu huko Baraki alipoenda kumzika babake, wanasaidiwa na watu waliokuwa na gari lililobeba mizigo, wanadai kuwa mara kwa mara wamekuwa wakiwasaidia waasiriwa wanaohitaji kupelekwa hospitalini. Aidha, wanajitambulisha kuwa wa Shirika la *Action Men* ambao huwa wanapeleka chakula katika kambi ya Wakimbizi ya Makutu.

Utafiti wa Nyiri (2014) ulibaini kuwa katika mizozo ya ardhi eneo la mlima Elgon, mashirika yasiyo ya Serikali kama vile National Council of Churches of Kenya (NCCK), Medicine Sans Frontiers (MSF), Shirika la Msalaba Mwekundu na kanisa la katoliki walikuwa na mchango muhimu katika kuwawezesha waathiriwa wa mizozo kurejea kwao. Aidha, kanisa na mashirika hayo walifanya kila waliloweza kuhakikisha kuwa waliofurushwa walirejea katika ardhi yao.

Nchini Kenya mashirika mbalimbali huweza kuhusika katika kutoa misaada ya aina mbalimbali hasa kwa waathiriwa wa mizozo ya ardhi. Kwa mfano, Shirika la Msalaba Mwekundu katika kuwapeleka watu hospitalini, kutoa huduma ya kwanza na pia kupeleka chakula katika kambi za wakimbizi wa ndani. Kwa hivyo vifungu vilivyodondolewa vinashadidia kuwa Mashirika yasiyo ya serikali yanaweza kuchangia katika kuleta suluhu kwa mizozo ya ardhi. Isitoshe, katika *Kufa Kuzikana,* Walibora anaonyesha mchango wa mashirika yasiyo ya Serikali kupitia mfano ufuatao:

> Baada ya kusoma jarida lile nilifafanukiwa na mambo. Kauli ya Jerumani ilinisibu. Nilikuwa kama mtu aliyezinduliwa usingizini. Lilikuwa jarida **lililochapishwa na shirika moja la kutetea haki za kibinadamu.** Jarida hilo lilieleza kwa kina kuhusu mapigano Wilayani Korosho na athari zake. Yamkini waandishi wa jarida hilo walikuwa wamefanya utafiti si haba. (*Kufa Kuzikana*, uk 160, msisitizo wangu)

Kupitia mfano uliorejelewa, Akida anaeleza jinsi ambavyo alifahamikiwa na mambo baada ya kusoma jarida alilokabidhiwa na Jerumani. Aidha, inabainika kuwa jarida hilo lilichapishwa na shirika moja la kutetea haki za kibinadamu, ambalo lilieleza kwa kina kuhusu mapigano Wilayani Korosho na athari zake. Vilevile, ni jarida lililochapishwa kwa siri na kusambazwa kwa siri nchini Kiwachema. Hivyo, Walibora anaonyesha wazi kuwa mashirika kama hayo yanaweza kusaidia katika kuzindua na kutahadharisha watu kuhusu athari za mizozo katika jamii pakiwemo mizozo ya ardhi kwa kuchapisha

majarida ambayo hueleza na kuhamasisha watu kuhusu chanzo, hali, kina na athari za mizozo ya ardhi.

### 6.4 Viongozi wa Kisiasa

Kwa mujibu wa waandishi wa riwaya teule, viongozi wa kisiasa wanao mchango mkubwa katika kusuluhisha matatizo ya ardhi. Kwa mfano:

> … Upepo wa mashambulizi ulipovuma jina moja lilitajwa. Jina la kweli la mwanasiasa huyo aliyelaumiwa na nafsi za wakimbizi ni Tanga, lakini alijulikana sana kwa jina la lakabu, Mwamba…baadhi ya wafuasi wake walimnasibisha na **Tom Kisale aliyekuwa mtetezi wa haki za wafanyakazi nchini Tandika**. Kwa siku kadhaa mwamba alipambana na Ngozi ambaye minong`ono ilisema ni mzaliwa kamili wa Lumbasa… (*Kovu Moyoni*, uk 52. Msisitizo wangu)

Kwa mujibu wa kifungu kilichonukuliwa, inadhihirika kuwa Wanasiasa kama vile Tom Kisale katika *Kovu Moyo*ni husaidia katika kusuluhisha mizozo ya ardhi kwa kuwa watetezi wa haki za watu kama vile wakimbizi, maskwota na vilevile wafanyikazi. Aidha, kutowajibika kwa wanasiasa kunaweza kusababisha mizozo si haba. Hii ndio maana mwanasiasa kwa jina Mwamba anahusishwa na mashambulizi yote ya ardhi Rama kwa kuwatumia vijana wasio na kazi ambao walizurura wakinywa pombe haramu na wale waliofeli mambo ya shule ili kuendeleza ajenda zake za kibinafsi.

Nchini Kenya, mizozo ya umiliki wa ardhi katika sehemu mbalimbali nchini imekuwa changamoto kuu huku wanasiasa wakilaumiwa kwa kutumia tatizo hilo, kujitafutia kura nyakati za uchaguzi. Washikadau mbalimbali wa sekta ya ardhi wanapaswa kuandaa makongamano ambapo masuala ya mizozo ya kihistoria ya umiliki wa ardhi, ufisadi katika sekta ya ardhi, suala la maskwota, hatimiliki miongoni mwa masuala mengine muhimu yanapaswa kujadiliwa. Isitoshe, ni muhimu wabunge pamoja na viongozi wengine wa kisiasa kuweka kando tofauti zao za kisiasa na kuungana pamoja ili suluhisho la kudumu lipatikane kwa haraka. Kwa kuwa kutowajibika kwa wanasiasa nchini huzidisha matatizo mengi katika jamii pakiwemo mizozo ya ardhi, jambo hili huchochea wananchi kutaka mabadiliko na hatua mwafaka ambayo huchukuliwa na wananchi ni kuwaondoa mamlakani. Kwa mfano:

> …lakini tangazo lililonishangaza ni lile kuhusu uchunguzi katika mauaji ya mbunge wetu Johnstone Mabende, aliyekuwa pia Waziri wa Usalama wa Ndani. Redio ilisema uchunguzi wa polisi wa idara ya upelelezi wa jinai ulibaini kuwa **Mheshimiwa Mabende kauawa na afkani mmoja**

> **jina lake Johnson Muyaka.** Mauaji yenyewe aliyatekeleza kwa bunduki aliyoiiba kwa babake katika sehemu ya Binge, Wilayani Sangura. (*Kufa Kuzikana*, uk 220-221, msisitizo wangu)

Kwa mujibu wa *Kufa Kuzikana* mbunge maarufu Johnstone Mabende, aliyekuwa pia Waziri wa Usalama wa ndani anauawa na Johnson Muyaka aliyejulikana kwa jina Jerumani baada ya kuiba bunduku ya babake. Katika *Kufa Kuzikana*, Jerumani anasawiriwa kama mzalendo wa kweli ambaye licha ya kuwa akili punguani, aliudhika sana na unafiki wa viongozi na ndiposa anahuzunika sana wakati alisikia kwamba mbunge Johnstone Mabende kateuliwa kuwa Waziri wa Usalama wa Ndani.

Nchini Kenya, mara kwa mara Wanasiasa wamelaumiwa na kuhusishwa na maovu mengi kama vile mizozo ya ardhi. Kwa mfano Fred Kapondi aliyekuwa mbunge wa eneo la mlima Elgon alihusishwa na mashambulizi ya eneo hilo ambapo zaidi ya watu 1300 waliuawa mwaka wa 2005. (Nyiri, 2014). Aidha kiongozi wa wanamgambo wa SLDF, Matakwei aliuawa kwa kupigwa risasi jinsi ambavyo mhusika Meja K aliuawa katika *Kovu Moyoni*. Kwa hivyo, kupitia mtazamo wa waandishi wa riwaya teule, mara nyingi wanasiasa huhusishwa na mizozo ya ardhi, ndiposa wanawakashifu viongozi kama hao na kuonyesha kuwa njia mojawapo ya kukomesha au kupunguza mizozo hiyo ni kuwaondoa wanasiasa hao mamlakani. Hii ndio sababu katika *Kufa Kuzikana* mbunge Johnstone Mabende anauawa.

### 6.5 Juhudi za Wananchi

Wananchi wenyewe wanadhihirishwa kuwa nguzo muhimu katika kusuluhisha mizozo ya ardhi katika taifa lolote lile. Dondoo zifuatazo zinashadidia maelezo haya:

> Wageni walikaribishwa nyumbani. Mazungumzo ya ukwe yakaanza. **Boke hakuamini yule mpenzi wa mwanawe ndiye aliyetajwa katika mashambulizi mengi pale Siloko. Lakini akakubali ya jana yamepita. Alishughulikia ya leo.** Mambo mengi aliamua kumwachia Mungu. Wageni walitumbuizwa. Wakafanya yote kwa utaratibu na hivyo wakawafungulia njia mwafaka Eddah na Mulota kuoana. (*Kovu Moyoni*, uk 114)
>
> … `Eeh? Unafanya urafiki na Wakanju huku, unaelewa wanatuua sisi Wakorosho. Unasaliti kabila lako? Unamweka Mkanju nyumbani kwako Shauri Moyo! ` **Nikamwambia mimi naamini Bibilia: Bibilia husema adui mpende, usimtende na kisasi mwachie Muumba** (*Kufa Kuzikana*, uk 65, msisitizo wangu)

Katika *Kovu Moyoni*, Mulota ambaye alikuwa askari aliyetoka katika kabila la kiasili la Wasululu, anamchumbia Eddah na baada ya mashauriano na wazazi wanaruhusiwa kuoana. Licha ya changamoto na vitisho kutoka kwa wazee wa kabila lake, Mulota aliendelea kumpenda Eddah kama mke wake. Vilevile katika *Kufa Kuzikana*, Tim aliyekuwa wa kabila la wakorosho aliendelea kuwa rafiki wa Kufa na kuzikana wa Akida aliyekuwa wa kabila la Wakanju.

Aidha, Tim anamfadhili Akida katika kila jambo licha ya pingamizi kutoka kwa dadake Tamari na pia mjombake Tom ambaye alimfuta kazi kwa misingi hiyo. Kwa hivyo, waandishi wa riwaya teule wanadhihirisha kuwa wananchi wenyewe ndio wana uwezo wa kumaliza tofauti zao za kikabila na hivyo kusuluhisha mizozo ya ardhi kwa misingi ya kikabila. Licha ya pingamizi na changamoto nyingi kutoka kwa viongozi na pia wananchi wengine, inadhihirika kuwa iwapo baadhi ya wananchi wanajitahidi na kuvumilia changamoto wanazokabiliana nazo katika harakati ya kuondoa ukabila, hatimaye itawezekana.

### 6.6 Vyombo vya Dola

Kwa mujibu wa TUKI (2014) Vyombo vya Dola ni dhana inayoelezea vyombo vyenye mamlaka vinavyotumiwa na tabaka tawala kuendesha utawala au siasa ya nchi. Vyombo hivi ni pamoja na korti, magereza na askari.

#### 6.6.1 Korti na Magereza

Korti na Magereza ni vyombo vya Serikali ambavyo vimesawiriwa kuwa na mamlaka ya kusuluhisha mizozo ya ardhi katika jamii yoyote iwayo. Kwa mfano:

> Seli ilikuwa na watu wa aina mbalimbali, si wezi, si sinzia, si wapiga kabari, si matapeli, si wabakaji, si wauaji si walanguzi wa dawa za kulevya, si wendawazimu, si wasingiziwa walioundiwa kesi bure bilashi…pia nilishangaa zaidi kukutana na **Kasisi John ndani ya seli. Kadhalika nilikumbuka jarida alilonikabidhi Jerumani lililomnasibisha Kasisi John na mapigano Korosho** (*Kufa Kuzikana,* uk 188, msisitizo wangu)

Kwa mujibu wa dondoo la hapo juu, inadhihirika kuwa korti na magereza ni taasisi za serikali ambazo hutumiwa kuadhibu watu wanaotekeleza maovu ya kila aina katika jamii. Katika *Kufa Kuzikana* gereza imesawiriwa kuwa na manufaa na hatimaye suluhisho kwa mizozo mingi katika jamii, ambapo wanaonasibishwa na mashambulizi

Wilayani Korosho wanatiwa mbaroni na kufunguliwa mashtaka. Kwa mfano, Kasisi John aliyenasibishwa kuhusika katika vita vya kikabila Korosho anakamatwa na vilevile anapatikana na hatia ya kuwajua kimapenzi wasichana wanane ambao hawajafikisha umri wa miaka kumi na mine. Anafungwa jela miaka ishirini huku akifanya kazi ngumu na kuchapwa viboko vinne ili awe ibra kwa wengine. Kwa mujibu wa dondoo lililonukuliwa, inabainika pia kuwa wahalifu wengine katika jamii walikuwa wametiwa mbaroni.

Aidha, waandishi wa riwaya teule wamedhihirisha kuwa iwapo uchunguzi mwafaka hautafanyika kabla ya kuchukuliwa hatua kwa watuhumiwa, basi vyombo hivi vitazidisha madhara badala ya kuwa suluhisho. Vifungu vifuatavyo vinashadidia suala hili:

> King`ora kililia mara tatu ishara ya kwamba Mwita alikuwa amenyongwa tayari. Mama yake alipewa nguo zake akaondoka katika gereza la Raka…**Boke alichukia serikali. Alichukia polisi. Alichukia oparesheni nzima hiyo, akachukia wanasiasa waliotia cheche za moto zilizolipua moto uliowaka Rama**. Wanasiasa ndio waliotia chombo cha mashambulizi pondo hadi kikaingia baharini. (*Kovu Moyoni*, uk 132, msisitizo wangu)

Katika *Kovu Moyoni,* Mwita mwanawe Boke anahukumiwa kunyongwa baada ya kushukiwa kuwa mwanachama wa `Jeshi la Vijana`. Baadaye inagunduliwa kuwa aliyenyongwa hakuwa mwanachama wa kundi hilo bali ni kijana mwingine aliyekuwa na jina kama lake. Tukio hili linadhihirisha udhaifu wa korti na magereza katika kusuluhisha masuala ya kijamii pakiwemo suala la ardhi. Kwa hivyo, inabainika kuwa wasanii wa riwaya teule wanakejeli mahakimu katika korti ambao huchukulia washtakiwa hatua kabla ya kufanya uchunguzi mwafaka. Kwa upande mwingine, korti na mangereza ni vyombo muhimu vinavyoweza kurekebisha tabia zisizokubalika katika jamii hivyo kuwa suluhisho kwa masuala mengi pakiwemo mizozo ya ardhi.

Kwa mujibu wa ripoti mpya ya Taaasisi ya Uendeshaji na Usimamizi wa Ardhi (LDGI) (2014), kuna haja ya kubuniwa kwa mahakama spesheli za kushughulikia mizozo ya ardhi katika kaunti zote nchini. Aidha, ripoti hiyo imewalaumu mawakili kwa utepetevu wa kushughulikia kesi za mizozo ya ardhi huku wengi wakisababisha kesi hizo kukaa mahakamani kwa muda mrefu kufuatia kuhamishwa kiholela kwa kesi. Isitoshe, maafisa wa LDGI wanataka taasisi mbili kuu ambazo ni Wizara ya Ardhi,

Nyumba na Maendeleo ya Miji pamoja na Tume ya Kitaifa ya Ardhi kushirikiana na kuwajibika kwa pamoja ili kutekeleza wajibu wao kisheria.

### 6.6.2 Askari

Askari ni mtu anayelinda na kuihami nchi (TUKI, 2014). Kwa mujibu wa waandishi wa riwaya teule, askari ni muhimu katika kuendeleza utawala katika taifa lolote lile. Wao ndio hutumiwa na serikali katika kuleta amani na usalama katika taifa kila inapokosekana hasa kunapokuwa na mizozo. Kwa mfano:

> Boke alimwazia Inspekta Suko aliyesimama kidete kupinga visa vya Jeshi la vijana. Ilibidi kutoroka kambini kwa kuchelea usalama wake. Ameandikiwa barua ya kumwonya na wanayusi waliokuwa katika Jeshi la Vijana. **Suko alikuwa ni polisi aliyekuwa na moyo adimu…hakuwa na kinyongo. Alifahamu kazi yake ya uaskari.** Kabla ya msimu wa mashambulizi alijulikana katika kambi ya Lumbasa. Aliamka asubuhi na kukimbia kwa minajili ya mazoezi… (*Kovu Moyoni*, uk 13, msisitizo wangu)
>
> Katika kikao changu cha majuma mawili **nilishangazwa na jinsi askari polisi walivyonifadhilia. Hawakunibughudhi au kunitesa**. Sikulala njaa tena. Askari walinichunuku, wakinipokeza mkate na soda kila siku walizodai zililetwa na `ndugu yangu. ` mara nyingine waliniruhusu kuota jua kwenye ua wa kituo cha polisi, ijapokuwa chini ya ulinzi mkali. (*Kufa Kuzikana*, uk 190-191, msisitizo wangu)

Kupitia dondoo zilizonukuliwa, askari katika taifa wanasawiriwa kuwa watu wema ambao wamewajibika katika kuwahudumia wananchi. Hii ndio maana katika *Kovu Moyoni* Inspekta Suko anapinga visa vya Jeshi la Vijana. Aidha, anadhihirishwa kuwa polisi aliyekuwa na moyo adimu. Hali kadhalika, katika *Kufa Kuzikana* Akida anakumbuka jinsi ambavyo askari walimfadhilia alipokuwa katika jela wala hawakumtesa. Vifungu hivyo vinashadidia kwamba askari wanalo jukumu muhimu la kuwalinda na kuwafadhilia wananchi katika mambo mengi pakiwemo kuwajibika katika kusuluhisha mizozo ya ardhi.

Hata hivyo, kupitia riwaya teule, inabainika kuwa baadhi ya askari hawatekelezi wajibu wao kama inavyotarajiwa kwani huzidisha madhara yanayotokana na mizozo katika jamii badala ya kuleta suluhisho. Hivyo, waandishi wa riwaya teule wamesawiri baadhi ya askari kuwa waovu na wasiowajibika katika kazi yao. Aidha husababisha maafa

mengi miongoni mwa wananchi hasa waadhiriwa wa mizozo ya ardhi. Kifungu kifuatacho kinashadidia jambo hili:

> … "sema lililokuleta," polisi alimwambia Boke. `*Nilinajisiwa na polisi,"* Boke alisema. "Polisi yupi?" mkuu wa kituo alimuuliza…Boke alipigwa na butwaa kuona yule polisi aliyemnajisi ndiye yule yule pale kituoni anayefanya kazi…Boke aliganda pale kitini kama jiwe. Alikumbuka usiku ule yule mwanamume aliyefaa kumlinda na madaraka yake yote yale alivyomnajisi na hata kumsababishia kuvuja damu… (*Kovu Moyoni*, uk 146, msisitizo wangu)

Kupitia dondoo lililonukuliwa, mhusika Boke katika *Kovu Moyoni* anaenda katika kituo cha polisi cha Sabasaba kupiga ripoti kuhusu jinsi alivyonajisiwa na askari Onyango. Mwandishi anawakejeli askari ambao wanapaswa kuwalinda wananchi dhidi ya watu wenye tabia kama hizo lakini badala yake ndio wanaowadhulumu wananchi.

Vilevile, udhaifu wa Jeshi la taifa unajitokeza katika *Kovu Moyoni* kupitia kifungu kifuatacho:

> …aliienda akasema nao lakini sikio lililomsikia halikutaka kuelezwa jambo tofauti. Kinywa kilimbeza akarudi nyumbani akiwa ameudhika. Alishindwa kuona tofauti baina ya Jeshi la Taifa na Jeshi la Vijana.Kama Jeshi la Vijana, **hili Jeshi la Taifa lilipiga watu na kushika vijana bila uchunguzi mzuri**. Baada ya kuondoka kwa Jeshi la Vijana, kulikuwa na kibarua kigumu kwa Jeshi la Taifa. Boke na wenzake walilala wakiwa na woga. **Walitembea na wakalala kwa woga hata baada ya Jeshi la Taifa kutia guu lake pale Rama. (***Kovu Moyoni*, uk 46, msisitizo wangu)

Kupitia mfano wa hapo juu, inadhibitika kuwa licha ya kuwepo kwa Jeshi la Taifa Rama, amani haikurejea kwani Jeshi hili lilipiga watu na kuwashika vijana bila hata uchunguzi mzuri. Hii ndio maana Boke na wenzake walilala kwa woga. Ndiposa Muchiri (2016) anahoji kuwa hata walinda usalama ambao huenda katika maeneo ambayo mizozo hutokea, iwe ni mlima Elgon, Kisumu, Bonde la Ufa au Pwani, huonekana kama ambao huendeleza uoga na vitisho badala ya kuwa chanzo cha usaidizi kwa waathiriwa. Kwa hivyo, licha ya kuwa Jeshi la Taifa limesawiriwa kuwa na mchango mwafaka katika kusuluhisho mizozo ya ardhi, waandishi wa riwaya teule wanaonyesha wazi udhaifu wake ambao hauna budi kurekebishwa.

### 6.7 Vyombo vya Habari

Kwa mujibu wa waandishi wa riwaya teule, vyombo vya habari vinaweza kutumika kueleza wananchi kuhusu masuala ya kijamii. Vyombo hivi vinaweza kuwa redio, magazeti au majarida na televisheni. Kwa mfano:

> Meja-K alikaa katika kiti cha plastiki akisoma gazeti la siku, *The Daily Telegraph.* Alirauka leo asubuhi ili kupokea msaada ulioletwa kwa ndege ya helikopta kutoka kwa wahisani na wafadhili. …**alipata kusoma kuhusu zogo la kitaifa lililofuatia kuhusu viongozi kugombania kura. Lo! Kilikuwa kivumbi kweli. Fahali hao wawili walipopigana nyasi ndizo zilizoumia. Watu waliuana**. *Watu walilaumiana.* (*Kovu Moyoni*, uk 24, msisitizo wangu)

> "…Habari zinazotufikia hivi punde," alisema mwanamke mtangazaji, "zasema, mamia ya watu wameonekana wakikimbilia usalama-wengine wao kwa miguu-kwenye miji mbalimbali nchini Kiwachema, baada ya kufumuka vita vya kikabila katika Wailaya ya Koroshp nchini humo. **Mwandishi wa BBC aliyeko Tandika, jiji kuu la Kiwachema, amearifu kuwa watu takriban themanini wameuawa na mia tatu wakajeruhiwa, wengine wao vibaya sana,** katika vita baina ya makabila ya Wakorosho na Wakanju vilivyoanza siku chache zilizopita. (*Kufa Kuzikana*, uk 61, msisitizo wangu)

Dondoo hizo zinadhihirisha mchango wa vyombo mbalimbali vya habari katika kuarifu umma kuhusu hali ya mambo hasa kunapotokea mizozo. Katika *Kovu Moyoni,* Meja-K aliyekuwa kiongozi wa`Jeshi la `Vijana anasoma Gazeti la Siku. Anapata maelezo kuhusu zogo la taifa baina ya viongozi wawili waliogombana kwa sababu ya kura, ambapo watu wanauawa na kulaumiana. Vilevile katika *Kufa Kuzikana,* Akida na Tim wanapata habari kuhusu hali ya mambo ilivyokuwa nyumbani kwao Wilayani Korosho kupitia matangazo ya redio ya Sauti ya Kiwachema. wanasihiwa, kuhimizwa, kushauriwa na pia kukumbushwa na kutahadharishwa. Hii ndio sababu Akida anachelea kurejea nyumbani kumjulia hali babake kwa sababu ya ukosefu wa usalama.

Hata hivyo, wasanii wa riwaya teule wanadhihirisha kuwa wakati mwingine vyombo vya habari hunyimwa haki ya kuarifu wananchi kuhusu hali ya mambo ilivyo hasa wakati wa mizozo ya ardhi. Haya yanadhihirika kupitia dondoo hizi:

> Mapema wiki hii **wahariri wakuu wa magazeti mawili nchini Kiwachema walitiwa nguvuni baada ya kuchapisha habari za vita hivyo**. Matokeo ya Jumatano ya magazeti nchini humo yalinaswa yote na polisi…mkuu wa wilaya ya Korosho, bwana Erastus Adaulo **amevishutumu vyombo vya habari vya kigeni kwa kupiga chuku hali ya usalama wilayani**… (*Kufa Kuzikana*, uk 61, msisitizo wangu)

> … kila siku akawa anatazamia kusafiri lakini kila kulipokucha alikuwa akisikia kadhia za watu kuuawa na hata kunajisiwa. Siku zote **alitegea taarifa ya habari lakini hakusikia matangazo yoyote kuhusu mashambulizi ya Rama**. Eneo hili likawa ni kama eneo lililo ughaibuni lisilo katika nchi ya Tandika… (*Kovu Moyoni*, uk 79-80, msisitizo wangu)

Katika riwaya ya *Kovu Moyoni*, wahariri wakuu wa magazeti wanatiwa mbaroni baada ya kuchapisha habari kuhusu vita wilayani Korosho. Hii inadhihirisha unafiki miongoni mwa viongozi na ndio maana mkuu wa Wilaya ya Korosho bwana Erastus Adaulo anavishutumu vyombo vya habari na kusema kuwa vinatilia chuku hali ilivyo. Hata hivyo, wananchi wanaonekana kuelewa unafiki wa viongozi. Hii ndio maana katika *Kufa Kuzikana*, Tim anamwambia Akida kuwa hao viongozi wanaficha ukweli na kuwa utajulikana hatimaye. Aidha, katika *Kovu Moyoni*, Mali ya Mungu akiwa Dunga, anaelezwa na rafiki yake Yoko kuhusu kuuawa kwa babake Kanja na pia kunajisiwa kwa mamake na 'Jeshi la Vijana'. Licha ya kusikia kadhia za watu kuuawa na hata kunajisiwa, siku zote anategea taarifa ya habari lakini hapati matangazo yoyote kupitia vyombo vya habari kuhusu mashambulizi ya Rama.

Kwa hivyo, inabainika kuwa vyombo vya habari ni muhimu katika taifa ili kuonya kushauri na kutahadharisha wananchi wakati kunapozuka mizozo ya ardhi. Hata hivyo, wasanii wa riwaya teule wanakashifu serikali na wote wanaohusika katika kuzuia vyombo vya habari kutangazia wananchi kuhusu hali ya usalama au ukosefu wa usalama kila mizozo inapotokea. Ndiposa Nyukuri (1997) anakashifu hatua ya serikali nchini Kenya ya kuzuia vyombo vya habari katika kuwapasha wananchi kuhusu hali ya usalama nyakati za mizozo ya ardhi.

Katiba ya Kenya (2010) inavipa vyombo vya utangazaji na vyombo vingine vya habari na vya kielektroniki uhuru wa kujiendeleza kwa kuongozwa na taratibu za leseni ambazo zimeratibiwa kuhakikisha udhibiti wa mawimbi ya hewa na aina nyingine za usambazaji wa mawimbi, wala haviingiliwi na Serikali, maslahi ya kisiasa au ya kibiashara. Kwa hivyo, vyombo vya habari vina wajibu mkubwa wa kuripoti taarifa zinazohusiana na masuala ya kijamii kama vile mizozo ya ardhi. Kadhalika, vyombo vya habari hususan redio na televisheni zinatakiwa kutanguliza uzalendo na kutetea maslahi ya taifa ili kuliepusha taifa katika migogoro na mitafaruku inayoweza

kusababisha machafuko nchini hasa katika vipindi vya Uchaguzi Mkuu. Isitoshe, vyombo vya habari vina nguvu kubwa kuchambua na kutengeneza mustakabali wa taifa na hasa vijana iwapo itatumika vizuri badala ya kuwa chanzo cha matatizo na uchochezi, mambo ambayo yanaweza kulisambaratisha taifa.

### 6.8 Wapatanishi

Mpatanishi ni mtu anayesuluhisha watu au pande mbili zinazogombana (TUKI, 2014). Kwa mujibu wa waandishi wa riwaya teule, wapatanishi hutekeleza jukumu muhimu katika kuleta suluhisho kwa mizozo ya kijamii hasa suala la ardhi. Hili linadhihirika kupitia dondoo lifuatalo:

> Meja–K alisoma **kuhusu washauri wa kimataifa waliokuja kuwasuluhisha viongozi hawa wawili waliokuwa mithili ya majogoo kizimbani.** Kila mmoja akidai ndiye mshindi. Yule msichana waliyegombania walipewa watu wawili kummiliki na kumdhibiti. Mwafaka huo ukawafanya hao ndugu na marafiki wa muda mrefu watupilie mbali silaha wakaanza mashauriano… (*Kovu Moyoni*, uk 24, msisitizo wangu)

Katika *Kovu Moyoni*, Meja-K anasoma gazeti ambapo anapata habari kuhusu zogo la kitaifa lililofuatia kuhusu viongozi kugombania kura. Aidha anasoma kuhusu washauri wa kimataifa wanaokuja kuwasuluhisha viongozi hao waliogombana na baada ya mashauriano wanaafikia mwafaka ambao unawafanya hao ndugu na marafiki wa muda mrefu watupilie mbali silaha. Walibora katika *Kufa Kuzikana* anasema:

> … "vitimbi vya dadako siviwezi," nikampasulia mbarika Tim. "hataki kunitia machoni, tutaishije pamoja hapa?" **"hilo tumelizungumza naye tukiwa na Pam. Lisikutie wasiwasi.** Amemchunuka Pam, anamsikia sana." … "Nakuomba radhi," alisema Tamari. "Nisamehe kwa ufedhuli wangu majuzi yale. Ama ebu tuseme uhasama wangu kwako tangu tukiwa shuleni. Nimetupa jongoo na jiti lake. Nadhani hasada na msukumo wa kikabila ndivyo vilivyonifanya kukuchukia. (*Kufa Kuzikana*, uk 115-117, msisitizo wangu)

Kwa mujibu wa dondoo hilo, Tamari dadake Tim anamchukia sana Akida kwa sababu yeye ni *Mkanju*. Anamfanyia kila aina ya vitimbi hadi Akida anaamua kuondoka katika nyumba waliyoishi. Lakini Tim anaingilia kati wakiwa na mpenziwe Pam ambapo wanazungumza na Tamari. Hatimaye Tamari anamwomba Akida amsamehe kwa makosa aliyomtendea tangu wakiwa shuleni. Kwa mujibu wa vifungu vilivyonukuliwa, waandishi wa riwaya teule wanadhihirisha kuwa wapatanishi wa kimataifa wanaweza kutumika katika kusuluhisha mizozo ya ardhi katika jamii ili kuleta mwafaka baina yao.

Isitoshe, inadhihirika kuwa, sio tu wapatanishi wa kimataifa bali wanajamii wenyewe katika jamii yoyote ile wana jukumu la kuleta mwafaka miongoni mwa kabila au watu wanaozozania mambo mbalimbali katika jamii kama vile suala la ardhi.

Nchini Kenya, kuanzia mwezi wa Desemba mwaka wa 2007 hadi Februari mwaka wa 2008 kulishuhudiwa mizozo ya kikabila ambayo ilichochewa na matokeo ya Uchaguzi Mkuu uliofanyika mwezi wa Desemba tarehe ishirini na saba mwaka wa 2007. Kutangazwa kwa matokeo ya uchaguzi huo kukawa kichocheo cha vurugu ambapo zaidi ya watu elfu moja waliuawa na kufurushwa kwa watu zaidi ya elfu mia tano. Ilibainika kuwa mizozo hiyo ilizidi katika eneo la Bonde la Ufa kulikomilikiwa na Wakikuyu. Kwa hivyo mizozo hiyo ilihusishwa na suala la umilikaji wa ardhi baina ya Wakikuyu na Wakalenjin.

Hata hivyo, ilithibitika kuwa mizozo hiyo ilipangwa na wanasiasa pamoja na viongozi wengine pakiwemo pia polisi wa taifa la Kenya. Kupitia juhudi za wapatanishi wa kimataifa, Kofi Annan alifaulu katika kuwapatanisha Mwai Kibaki na Raila Odinga katika kuafikia mwafaka wa mashauriano (Kareithi na Lucheli, 2007). Kwa hivyo, inabainika kuwa wapatanishi wa kitaifa na pia kimataifa wanaweza kuwa nyenzo mojawapo ya kusuluhisha mizozo ya ardhi kama inavyodhihirika katika riwaya teule.

### 6.9 Mielekeo Chanya ya Wananchi

Kulingana na wasanii wa riwaya teule, mielekeo chanya ya wananchi inaweza kuleta suluhisho kwa mizozo ya ardhi. Madai haya yanadhibitika kupitia matamshi ya baadhi ya wahusika katika riwaya za *Kufa Kuzikana* na *Kovu Moyoni*. Wanasema:

> …usalama gani? Mbona vinywa vya watu bado vinalalamika? Ubakaji bado ungaliko. Unyang'anyi ungaliko. Rushwa ingaliko na imeshamiri. Wakati ndio utakaoamua hali yetu," ***… lazima tulete usalama sisi wenyewe. Mtu wa nje hataweza kuleta usalama.*** Hajui mkosaji. Sisi ndio tunaojua… (*Kovu Moyoni*, uk 133, msisitizo wangu)
>
> "Umekasirika?" alicheka na kutikisa kichwa. "**Nilitaka tu kukusaidia kujielewa mwenyewe na kuielewa nchi yako Kiwachema. Kukusaidia uone jinsi utakavyoifanya Kiwachema iwe `kiwachema` kweli- kisiwa cha amani, udugu na ustaw***i,* nchi yenye makabila mengi lakini bila ukabila. (*Kufa Kuzikana*, uk 159, msisitizo wangu)

Kutokana na vifungu vilivyonukuliwa, waandishi wa riwaya teule wanadhihirisha kwamba wananchi wenyewe wanaweza kuwa nguzo kuu katika kusuluhisha tatizo la ardhi, iwapo watakuwa na mitazamo na mielekeo chanya kuhusu nchi yao kwa kudhamini upendo na amani huku wakiziasi tofauti zao za kikabila. Kwa mfano, katika *Kovu Moyoni*, Nifreda anamweleza Eddah kuwa ili kuwepo na usalama nchini, lazima uletwe na wananchi wenyewe. Hii ni baada ya kukosekana kwa usalama na amani hata baada ya Jeshi la taifa kwenda Rama wakati wa mashambulizi. Nifreda anatambua kuwa hata baada ya Jeshi la Taifa kuwasili, bado vinywa vya watu vinalalamika, ubakaji bado ungaliko, unyang`anyi ungaliko, rushwa ingaliko na umeshamiri.

Vilevile, katika *Kufa Kuzikana*, Jerumani anamweleza Akida kuwa nchi yao ya Kiwachema ilihitaji mapinduzi. Aidha, alimfafanulia kuwa mapinduzi yaliyohitajika sio ya serikali bali mapinduzi ya mioyo, ya ada na mila, ya mitazamo, misimamo na mikabala. Kwa hivyo, inadhihirika kuwa wananchi wenyewe wanaweza kuleta usalama na hivyo kuleta suluhisho kwa mizozo ya ardhi iwapo watabadili mielekeo na mitazamo yao kuhusu maisha kwa jumla, kama inavyodhihirika katika riwaya za *Kovu Moyoni* na *Kufa Kuzikana*. Zaidi ya hayo, waandishi wa riwaya teule wanadhihirisha kuwa mizozo ya ardhi inaweza kutatuliwa iwapo wananchi watatambua athari za ukabila na kuasi chuki inayochochewa na viongozi. Kwa mfano:

> Mulota alikaa mwembeni akiwaza kwa nini wale wazee walimwambia na kumtisha vile. Alikumbuka majuto aliyokuwa nayo kuhusu visa vya Wasululu vilivyomfanya kutaka hata kuacha kazi ya kuwa polisi. Alikumbuka alivyotumiwa na Mwamba na Meja-K kutesa watu kwa sababu hawakuwa Wasululu. **Mulota aliona hali kama ile haifai**. Yeye, kama mtu mzima aliye katika taifa huru, alikuwa na uhuru wa kuamua mambo aliyotaka. (*Kovu Moyoni*, uk 142, msisitizo wangu)

Mulota, polisi aliyetumiwa kutesa watu anakumbuka maovu yote ambayo yeye na wenzake waliweza kutekeleza. Anahuzunishwa na matendo yake na ndio maana licha ya kuamua kuacha kazi ya kuwa polisi, anamchumbia Eddah ambaye hakuwa *Msululu* na hatimaye kumuoa. Kwa hivyo, mhusika Mulota anadhihirisha kuwa inawezekana kumaliza tofauti za kikabila ambazo ni msingi wa mizozo ya ardhi, hasa nchini Kenya ambapo mizozo mingi ya ardhi hutokea baina ya makabila tofauti baada ya uchochezi wa wanasiasa na viongozi wengine nchini. Kadhalika, ni muhimu wananchi kutambua na kukubali kuwa tatizo la ardhi ni la kihistoria. Kwa hivyo, kupata suluhu lake ni lazima wafuate sheria zifaazo. Vilevile, wananchi wanafaa kushiriki katika utatuzi wa

mizozo ya ardhi kwa kuwasilisha tetesi kuhusu ardhi kwa Tume ya Kitaifa ya Ardhi (NLC).

### 6.10 Hitimisho

Sura hii imeangazia mchango wa asasi mbalimbali katika kusuluhisha mizozo ya ardhi kama ilivyosawiriwa katika *Kufa Kuzikana* na *Kovu Moyoni*. Matokeo ya utafiti yamebainisha kuwa asasi mbalimbali zinaweza kuchangia katika kusuluhisha mizozo ya ardhi. Miongoni mwa asasi hizo ni serikali, dini, mashirika yasiyo ya serikali, viongozi wa kisiasa, korti na magereza, vyombo vya habari na pia wapatanishi. Vilevile, matokeo ya utafiti huu yamebainisha kuwa mielekeo na mitazamo chanya ya wananchi katika taifa lolote lile kuhusu mizozo ya kijamii kama vile mizozo ya ardhi ni muhimu katika kuleta suluhisho lake. Kwa hivyo, mabadiliko yanayohitajika sio ya serikali bali mabadiliko ya mioyo, ya ada na mila, ya mitazamo, misimamo na mikabala ya wananchi ili kuweza kurejesha amani katika nchi yao.

# SURA YA SABA

# MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 7.0 Muhtasari

Utafiti huu ulihusu uchanganuzi wa suala la ardhi katika riwaya teule za Kiswahili. Riwaya zilizoteuliwa ni *Kovu Moyoni* (Habwe, 2014) na *Kufa Kuzikana* (Walibora, 2003). Madhumuni yalikuwa kubainisha jinsi waandishi wa riwaya teule wamesawiri mizozo ya ardhi, kubainisha namna waandishi wa riwaya hizo walivyotumia fani za lugha kuwasilisha athari za mizozo ya ardhi na vilevile kutathmini mchango wa asasi mbalimbali katika kusuluhisha matatizo ya ardhi kama inavyosawiriwa katika *Kufa Kuzikana* na *Kovu Moyoni*.

Umuhimu wa utafiti huu ulikuwa kuwanufaisha wahakiki wa fasihi katika kushadidia mtazamo kwamba, fasihi inaakisi kikamilifu matatizo yanayoibuka katika jamii ilimoibuka na ni chombo madhubuti kinachoweza kutumiwa kutatua matatizo hayo. Isitoshe, utafiti huu ulikuwa wenye manufaa kwa waundaji sera na idara zinginezo za serikali zinazohusika ili kuibuka na sera madhubuti zitakazokuwa na uwezo wa kusuluhisha tatizo la ardhi nchini. Ulikuwa utafiti wa maktabani ambapo mtafiti alisoma riwaya za *Kovu Moyoni* na *Kufa Kuzikana* ili kupata data iliyochanganuliwa.

Utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya Baadaukoloni ambayo inahusishwa na kazi za Cesaire (1950), Fanon (1961) Said (1978) na Babha (1994). Nadharia ya baadaukoloni ilitumika ili kufafanua jinsi waandishi wa riwaya za *Kovu Moyoni* na *Kufa Kuzikana* walidhihirisha athari za ukoloni katika suala la ardhi pamoja na kuonyesha msingi ambao jamii ya Kenya imejengeka kuhusu athari zinazotokana na umiliki wa ardhi, ikiwa ni njia mojawapo ya uzalishaji mali nchini Kenya. Katika utafiti huu, Uchanganuzi wa kimaelezo wa data umefanywa na kuwasilishwa kwa maandishi ya kinadhari. Uchanganuzi wa data umeegemezwa katika madhumuni ya utafiti ili kubainisha mtazamo wa waandishi wa riwaya teule kuhusu suala la ardhi.

## 7.1 Hitimisho

Lengo kuu la utafiti huu lilikuwa kuchunguza jinsi ambavyo waandishi wa riwaya za *Kufa Kuzikana* (Walibora, 2003) na *Kovu Moyoni* (Habwe, 2014) wameliangazia suala la ardhi ili kuibua mjadala wa kitaifa kuhusu suala hilo na kuinua viwango vya mishikamano ya kijamii, amani na umoja, masuala ambayo ni muhimu katika maendeleo endelevu nchini Kenya. Kupitia ukusanyaji na uchanganuzi wa data, utafiti

huu umebainisha kuwa fasihi na hasa utanzu wa riwaya ni nyenzo ya kuangazia masuala ya jamii pakiwemo suala la ardhi.

Imebainika kuwa waandishi wa riwaya za *Kovu Moyoni* na *Kufa Kuzikana* wamerejelea suala la ardhi nchini Kenya kama tatizo la jamii ambamo riwaya hizo ziliibuka huku wakiwasawiri Wakenya kama wahusika katika kazi zao kwa mujibu wa vipindi mbalimbali vya kihistoria. Aidha wametumia fani mbalimbali za lugha ili kubainisha athari za mizozo ya ardhi. Zaidi ya hayo, imegunduliwa pia kuwa wasanii wa riwaya teule wametoa suluhisho mbalimbali ambazo zinaweza kutumiwa katika kutatua mizozo ya ardhi.

Kulingana na matokeo ya utafiti huu, imeafikiwa kuwa utanzu wa riwaya ya Kiswahili umeakisi suala la ardhi kama mojawapo ya matatizo ya kijamii ambamo riwaya hiyo imeibuka. Kwa hivyo, ni nyenzo mwafaka ambayo inaweza kutumiwa katika kutatua matatizo hayo kama ilivyobainishwa kupitia riwaya za *Kovu Moyoni* na *Kufa Kuzikana*. Zaidi ya hayo, imebainika kuwa mizozo ya ardhi ya mara kwa mara ilitokana na athari za kikoloni katika masuala ya ardhi ambazo hazijaweza kutatuliwa kwa njia mwafaka.

**7.2 Mapendekezo ya Utafiti wa Baadaye**

Utafiti huu umeshughulikia suala la ardhi katika riwaya teule za Kiswahili mfano wa *Kovu Moyoni* na *Kufa Kuzikana*. Kwa kuwa suala la ardhi ni suala nyeti ambalo limekuwepo tangu enzi za ukoloni na lingali linaathiri watu katika mataifa mengi hasa barani Afrika, mtafiti anapendekeza uchunguzi zaidi ufanywe katika tanzu zingine za fasihi kama vile tamthilia, ushairi na hadithi fupi ili kubainisha jinsi wasanii wa kazi hizo wameangazia suala la ardhi kwani utafiti huu ulijikita katika utanzu wa riwaya.

Matokeo ya utafiti huu yamebainisha kuwa fasihi huangazia masuala ya kijamii na ni nyenzo madhubuti ambayo inaweza kuchangia katika kusuluhisha masuala hayo. Kwa kuwa utafiti huu uliangazia suala la ardhi, mtafiti anapendekeza utafiti ufanyiwe masuala mengine nyeti ya kijamii kama vile suala la usalama na ufisadi ili kuchunguza jinsi wasanii wa fasihi wameangazia masuala hayo na namna ya kuyasuluhisha.

Utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya Baadaukoloni ili kufafanua jinsi waandishi wa riwaya za *Kovu Moyoni* na *Kufa Kuzikana* wamedhihirisha athari za ukoloni katika

suala la ardhi. Mtafiti anapendekeza utafiti zaidi ufanywe kuhusu suala la ardhi kwa kuongozwa na nadharia tofauti ili kuchunguza jinsi ambavyo suala la ardhi lilivyoangaziwa.

Kadhalika, utafiti huu ulijikita katika fasihi ya Kiswahili. Hivyo, utafiti zaidi unaweza kufanyiwa fasihi ya kiingereza hasa utanzu wa riwaya ili kubainisha jinsi ambavyo waandishi wa kazi hizo wameangazia suala la ardhi katika jamii.

## MAREJELEO


Ake, C. (1996). *Democracy and Development in Africa*.Washington, DC: Brookings Institution.

Arua, A. & Eka, J. (2002). Tribal Fighting: Land Disputes. *Melanesian Journal of Theology (18-2, 2002).*

Barasa, L. (2013). Why Land is the Main Cause of Conflict. *Daily Nation*, 22nd June page 22. Nairobi: Nation Media Group.

Calas, B. (2008). *From Rigging to Violence. The General Elections in Kenya, 2007*.Dar es Salaam: Mkuki na Nyota Publishers, Limited.

Chege, S.N. (2013). Limitations of the Current Land Laws in Addressing the Squatter Land Problem in Kenya. Unpublished Masters Thesis, University of Nairobi.

Childs, P. & Williams, R.J. (1997). *An Introduction to Post-Colonial Theory*. London New York: Prentice Hall, Harvester Wheatsheeaf.

Chirere, M. (2012, 9, Dec). Where is Literature on Land Reform? Available at www. Herald.co.zw/where- is- literature-on-land-reform/. Accessed 20/05/2017.

Eagleton, T. (1996). *Literary Theory: An Introduction*. United States of America: The University of Minnessota Press.

Fanon, F. (1961). *The Wretched of the Earth*. New York: Grove Press.

Gagnon, G. (2008). Kenya Army and Rebel Militia War Crimes in Mt. Elgon (Human Rights Watch, 3-4-02).

Gatimu, S. (2014). *Governance, Crime and Justice Division*: Nairobi: Institute of Security Studies.

Goffard, C. (2011). *Court Sheds Light on Scary Kenya Gang*. A Hague Tribunal Examines the Secretive Mungiki`s Alleged Role in Election Violence. Nairobi: Government Printer.

Gonye, J. et al. (2012). Representations of the Land Reform Programme in Selected Zimbabwean Short Stories and Mutasa`s Sekai, Minda TaveNayo (Sekai, We Now Have the Land): A fait accompli? *Journal of Africa Studies and Development* vol.4 (9), pp. 207-217, December 2012

Habwe, J. (2014). *Kovu Moyoni.* Nairobi: Bookmark African Publishers.

Hermunen, T. (2004). Land Use Policy in Kenya: Experiences from Taita Taveta District. Unpublished Master`s Thesis, University of Helsinki.

Internal Displacement Monitoring Centre (2014). *People Displaced by Disasters* Nairobi: Government Printer.

Institute of Security Studies (2015). *East Africa Report*: *The Nature and Drivers of Insecurity in Kenya.* Nairobi: Government Printer.

Joseph, M. &Lucinda, H. (2001). *The Companion to Southern Literature*: Themes, Genres, Places, People, Movement and Motifs. United States: Louisiena State University.

Kanogo, T. (1987). *Squatters and the Roots of Mau Mau 1905-1963*. Nairobi: Heineman.

Kareithi, A & Lucheli, I (2007). SLDF Militia a Force to Reckon with. The Standard, 10th April: Nation media Group.

Kihara, S. I. (2016). Nafasi ya Vijana Katika Riwaya za *Pendo la Karaha* na *Kovu Moyoni*. Tasnifu ya Uzamili (M.A) Isiyochapishwa: Chuo Kikuu cha Nairobi.

Kimenyi, M.S & Ndung'u, S.N (2005). Sporadic Ethnic Violence: Why Has Kenya Not Experienced a Full- blown Civil War? In p/ Collier and N. Sambanis (Eds), Understanding Civil War (Vol. 1: Africa), World Bank: Washington D.C.

Leftie, P. (2009). Cabinet Approves Land Policy. New Laws to Correct Historical Injustices to Pastoralists and Coastals. 26th June, Nairobi: Nation Media Group.

Lumumba, O. (2005,). *Land–related Conflicts in Kenya: Policy and Legal Implications.* Available at www.pambazuka.org/human-security/land-related- Conflict- kenya- Policy-and-Legal-Implications. Accessed on 07/03/2017.

Maina, M.W. (2015). Land Disputes Resolution in Kenya: A Comparison of the Environment and Land Court and the Land Disputes Tribunal. Unpublished Master`s Thesis: University of Nairobi.

Makunike, B. (2014). Land Reform and Poverty Alleviation in Mashonaland East, Zimbambwe. Philosophiae Doctor Thesis, University of Free State: Bloemfontein.

Manji, A. (2015). *Whose Land is it Anyway? The Failure of Land Law Reform in Kenya*. Nairobi: Africa Research Institute.

Masibo, S. (2015). Uchanganuzi wa Diskosi Za Ardhi Katika Kazi Za Fasihi: Mtazamo wa Waandishi wa Kenya Kati ya 1980-2012. Tasnifu ya Uzamili (M.A) Isiyochapishwa: Chuo Kikuu Cha Moi.

Mayieka, N. M. (2012). Masuala Ibuka Yanayosawiriwa Katika Riwaya Za Kisasa. Tasnifu Ya Uzamili Isiyochapishwa: Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Messah, B.O. & Gachaba, L. M. (2013). Factors Leading to Squatter Problem in Rift Valley Province in Kenya: *Journal of Law and Conflict Resolution,* Kenya Methodist University, 6 (3), 48-55.

Miguna, M. (2012). *Peeling Back the Mask*: *A Quest for Justice in Kenya*. London: Gilgamesh Africa.

Mlacha, S. A. (1995). *Riwaya ya Kiswahili*. Tanzania: Dar Es Salaam University Press.

Muchiri, J. (2016). *The Burden of Tribal Clashes Lies Heavily on Kenyan`s Hearts. Daily Nation on 3rd* July.Nairobi: Nation Media Group.

Mugenda, O. & Mugenda, A. (1999). *Research Methods*. Nairobi: Acts Press.

Mutua, M. (2008). *Kenya's Quest for Democracy*: *Taming the Leviathan*. London: Lynne Rienner Publishers.

M`Ngaruthi, T. K. (2015). Usawiri wa Mwanasiasa wa Afrika katika Ushairi wa Kiswahili. Tasnifu ya Uzamifu (Ph.D) isiyochapishwa: Chuo Kikuu cha Chuka.

Mwathane, I. (2010). *The Contribution of Land on the Recent Violence in Kenya: Implications for the Ongoing Land Policy Dialogue*. Nairobi: Land Development and Governance Institute.

Mworia, L. K. (2009). An Evaluation of Continuous Conflict between Related Communities: A Case of Tharaka and Tigania Communities. Unpublished (MA)Project Report: Nairobi University.

Mworia, L & Ndiku, J. M. (2012*).* Inter Ethnic Conflict in Kenya: A Case of Tharaka-Tigania Conflict, Causes, Effects and Intervention Strategies. *Journal of Research in Peace, Gender and Development*. vol.2 (7) pp. 162-170, July 2012.

National Crime Research Centre, (2012). *A Study of Organised Criminal Gangs in Kenya*. Nairobi: Government Printer.

Njogu, K. na Chimerah, R. (1999*). Ufundishaji wa Fasihi*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Njogu, K. (1997). *Uhakiki wa Riwaya za Visiwani Zanzibar*. Nairobi: Nairobi University Press.

Njogu, K. et al (2015). *Elections and the Possibilities of Land in Kenya*. Nairobi: Twaweza Communications Limited.

Njuguna, H. K. & Mbaya, M. M. (2009). *Land Reforms in Kenya* Nairobi: An Institute of Surveyors of Kenya.

Nyiri, J.K (2014). The Impacts of Ethnic Conflict on Economic Development: The Case of Post-Election Violence in Kenya, 2007-2008. (M.A) Masters Project: University of Nairobi.

Nyukuri, B.K. (1997). The Impacts of Past and Potential Ethnic Conflicts on Kenyan`s Stability and Development, University of Nairobi: USAID Conference Paper on 10th-12th June.

Ochieng, R. (2011). Maigizo Kama Mbinu ya Maudhui Katika Riwaya Mbili Za Ken Walibora. Tasnifu ya Uzamili (M.A) Isiyochapishwa: Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Odhiambo, A.S.E (1974). *The Paradox of Collaboration and Other Essays*. Nairobi: East African Literature Bureau.

Ogendo, O. (1991). *Tenants of Crown Evolution of Agrarian Law and Institutions in Kenya*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Republic of Kenya. (2003). *Kenya Vision 2030*. Nairobi: Government Printer.

Republic of Kenya. (2010). *Constitution of Kenya*. Nairobi: Government Printer.

Republic of Kenya. (2007). *Report on Tharaka, Tigania Conflic*t by Njuri Ncheke Boundary Arbitration Committee. Pp 30-35

Said. E. (1978). *Orientalism*. London: Routledge.

Tugume, B.G. (2013). A Comparative Study of Human Rights Issues in The Novels of Ngugi Wa Thiong'o, Alex La Guma and Chinua Achebe. Unpublished (M.A) Masters Thesis: Makerere University. Kampala.

TUKI (2014). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Kenya: Oxford University Press.

Wachira, M. (2014). Bonde Hatari Zaidi Kutokana na Silaha Hatari, Siasa na Umaskini. Katika *Taifa Jumapili*, 9th November. Nairobi: Nation Media Group.

Wafula, M. (2013). Narrative Voice and Focalization in the Narration of Generational Conflicts in Selected Kiswahili Novels. Unpublished Doctor of Philosophy Thesis: University of Bayreuth.

Wafula, P. K. (2015). Mwingilianomatini katika *Cheche za Moto* na *Kidagaa Kimemwozea*. Tasnifu ya Uzamili (M.A) Isiyochapishwa: Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Wakhungu, J. Nyukuri, E. & Huggins, C. (2008). Land Tenure and Violent Conflict in Kenya, Nairobi.: African Centre for Technology Studies, Consultative Conference Proceedings.

Walibora, K. (2003). *Kufa Kuzikana*. Nairobi: Longhorn Publishers Limited.

Wa Thiong`o, N. (1981). *Writers in Politics*. Nairobi: Heinemann Kenya Limited.

Wamitila, K.W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers Limited.

Wamitila, K.W. (2003). *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Publications Limited.

Wayua, C. (2015). *Causes and Effects of Insecurity in Kenya*. Available at Www.Zakenya.Com/Politics/Causes-And-Effects-Of-Insecurity-In-Kenya.Html. Accessed On 27/06/2017

Wellek, R. & Warren, A. (1954). *Theory of Literature*. London: Harcourt, Brace, and Company.

## KIAMBATISHO 1: IDHINI YA UTAFITI

**NATIONAL COMMISSION FOR SCIENCE, TECHNOLOGY AND INNOVATION**

Telephone:+254-20-2213471,
2241349,3310571,2219420
Fax:+254-20-318245,318249
Email:dg@nacosti.go.ke
Website: www.nacosti.go.ke
when replying please quote

9th Floor, Utalii House
Uhuru Highway
P.O. Box 30623-00100
NAIROBI-KENYA

Ref: No. **NACOSTI/P/17/75196/16150**

Date: **27th March, 2017**

Mary Kanyua Njeru
Chuka University
P.O. Box 109-60400
**CHUKA.**

**RE: RESEARCH AUTHORIZATION**

Following your application for authority to carry out research on ***"Suala la ardhi katika riwaya teule za Kiswahili: Tathmini ya kovu moyoni na kufa kuzikana,"*** I am pleased to inform you that you have been authorized to undertake research in **Tharaka-Nithi County** for the period ending **27th March, 2018.**

You are advised to report to **the County Commissioner and the County Director of Education, Tharaka-Nithi County** before embarking on the research project.

On completion of the research, you are expected to submit **two hard copies and one soft copy in pdf** of the research report/thesis to our office.

**BONIFACE WANYAMA**
**FOR: DIRECTOR-GENERAL/CEO**

Copy to:

The County Commissioner
Tharaka-Nithi County.

The County Director of Education
Tharaka-Nithi County.


# KIAMBATISHO 2: KIBALI CHA UTAFITI

**THIS IS TO CERTIFY THAT:**
***MS. MARY KANYUA NJERU***
**of CHUKA UNIVERSITY, 69-60401**
**CHOGORIA,has been permitted to**
**conduct research in *Tharaka-Nithi***
***County***

**on the topic: *SUALA LA ARDHI KATIKA RIWAYA TEULE ZA KISWAHILI: TATHMINI YA KOVU MOYONI NA KUFA KUZIKANA***

**for the period ending:**
***27th March,2018***

**Permit No : NACOSTI/P/17/75196/16150**
**Date Of Issue : 27th March,2017**
**Fee Recieved :Ksh 1000**



**...............................**
***Applicant's***
***Signature***

**...............................**
***Director General***
***National Commission for Science, Technology & Innovation***

## CONDITIONS

1. You must report to the County Commissioner and the County Education Officer of the area before embarking on your research. Failure to do that may lead to the cancellation of your permit.
2. Government Officer will not be interviewed without prior appointment.
3. No questionnaire will be used unless it has been approved.
4. Excavation, filming and collection of biological specimens are subject to further permission from the relevant Government Ministries.
5. You are required to submit at least two(2) hard copies and one (1) soft copy of your final report.
6. The Government of Kenya reserves the right to modify the conditions of this permit including its cancellation without notice

**REPUBLIC OF KENYA**

NACOSTI

**National Commission for Science, Technology and Innovation**

**RESEACH CLEARANCE PERMIT**

Serial No.A 13444

**CONDITIONS:** see back page